UWAKILISHAJI WA UTANDAWAZI KATIKA RIWAYA MPYA YA KISWAHILI ILIYOANDIKWA NA SAID A. MOHAMED NA WADI K. WAMITILA

SETH OCHIENG' ALOMO

Tasnifu inayowasilishwa kwa Shule ya Mafuzu ya Chuo Kikuu cha Egerton ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili.

CHUO KIKUU CHA EGERTON

AGOSTI, 2016

UNGAMO NA IDHINI

Ungamo

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na wala haijawahi kuwasilishwa na yeyote kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu chochote.

Sahihi: ..... Tarehe: .....

Seth Ochieng' Alomo

AM12/2882/11

Idhini

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton.

Sahihi: ..... **Tarehe:** .....

Prof. Wendo Nabea

Idara ya Mawasiliano na Mtaala wa Fasihi, Chuo Kikuu cha Laikipia.

Sahihi:.....**Tarehe**.....

Dkt. Mayaka, Gwachi.

Idara ya Mawasiliano na Mtalaa wa Fasihi, Chuo Kikuu cha Laikipia.

HAKILINZI

© 2016 Seth Ochieng' Alomo

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupigisha chapa, kutafsiri au kuitoa tasnifu hii kwa jinsi yoyote bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa waelekezi wangu, Prof. Wendo Nabea na Dkt. Mayaka Gwachi.

SHUKRANI

Kwanza kabisa, ningependa kutoa shukrani kwa Maulana kwa afya njema katiki kipindi cha kuandika tasnifu. Pili, ningependa kushukuru Chuo Kikuu cha Egerton kwa kuniwezesha kuhitimu na shahada ya uzamili. Wasimamizi wangu: Prof. Nabea Wendo na Dkt. Mayaka Gwachi, asanteni kwa kuvumilia udhaifu wangu. Mlisimama nami tangu mwanzo, hamkunikemea japo nilikuwa mwanafunzi 'hafifu' mwenye wingi wa makosa. Kwa hakika, nawaombea dua njema. Aidha, waadhiri wangu walionielekeza wakiwemo Dkt. Furaha Tchai, Prof. Onyango Ogola, Prof. Kitetu, jopo lililoshughulikia kazi yangu kwenye idara na kitivo, wote ninawashukuru. Bw. Mathew Kwambai, nimekosa maneno ya kukushukuru. Ulibinafsisha kazi yangu, ukazama kwenye nafsi yangu, ukanielewa, ukanielekeza, ukanilisha, ukanilaza! Ufanisi wa kazi hii ulikutegemea, maneno yako ya busara, ukarimu wako, maombi yako ndiyo kiini cha tasnifu hii. Mungu akubariki. Grace Njagi, changamoto zako zilinichanganua nikajikagua, nikajielewa, nikafahamu maana ya kuwa mtu mbele ya utu. Nilipokosa ulinikosoa, ulivumilia na kukosoa kazi yangu katika changamoto zako, kwa ukarimu wako nikaona mwangaza, nashukuru. Shukrani zangu vilevile, ni kwa familia yangu: Kidosho changu: Lilian Alomo, ahsante kwa kuwa mfadhili wa kweli, katika harakati za kukosa ulinibugia peni, wakati wa kutikisika, ulinisimamisha imara. Langu ni kukurejesha kwa Mola, akubariki. Watoto wangu wapendwa: Troon-Williams na Earl-Peters; ninawaenzi sana. Mmekuwa msingi wa furaha yangu duniani, japo mlirarua kazi yangu na hata kumimina maji; siwezi kuwakemea kamwe. Milele mlinipumbaza akili hasa baada ya kutoka kwenye shamba la mawe, mlinifariji kwa nyimbo zenu, maombi yenu na hata usumbufu wenu. Mola awalinde mje muwe wahenga hai.Wazazi wangu wapendwa Bw. Ezra Alomo na Grace Alomo: nimepiga magoti chini, mikono yangu i juu, uso wangu u juu. Lengo nikuwashukuru na kuwaombea mzidi kuishi ili muone jinsi Mungu atazidi kubariki vizazi vyenu. Mlikuwa jiwe la msingi, maombi yenu, ufadhili wenu na hata mapenzi yenu yalimulika nuru katika kiza. Mimi ni mimi leo kwa sababu ya maneno yenu ya busara. Sitawakosea. Sahibu wangu Lydia Okinyi, asante kwa ukarimu wako hasa mwanzoni mwa kazi yangu. Ulijitokeza, ukanisaili, ukanikosoa, ukanifunza na hata kunipa moyo. Uliyonitendea katika kipindi hicho yangali hai kwenye akili. Ahsante. Wanafunzi wa uzamili mwaka wa 2011wakiwemo: Anne, Michemi, Cherop, Carolyne, Alex, Ruth, Grace na wengine, ahsanteni kwa ushurika wenu katika kipindi hicho. Mwalimu Okinyi Richard, ahsante kwa kunipa wakati mwafaka wa kuendeleza masomo yangu chini ya uongozi wako.

IKISIRI

Utandawazi ni suala ambalo kwa kipindi kirefu lilisawiriwa na waandishi wa riwaya kama wakala wa maendeleo. Maendeleo haya yalifasiriwa kama utangamano wa watu kimataifa kwa misingi ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hata hivyo, uwakilishi wake katika Riwaya Mpya ya Kiswahili umechukua mkondo mpya. Hii ni kwa sababu ya waandishi kuuangaza kwa kutumia vipengele vya Usasaleo na Udenguzi. Nia ya kutumia vipengele hivi katika Rawaya Mpya si wazi. Aidha, sababu ya kuvitumia kuwakilisha utandawazi si bayana. Utafiti huu ulihakiki matumizi ya elementi za Usasaleo katika kujenga maudhui ya utandawazi na nia ya matumizi yao. Nadharia ya Usasaleo iliongoza utafiti huu kwa sababu ya mihimili yake. Nadharia ya Usasaleo inapinga na kuyaumbua masuala mengi yaliyozingatiwa katika enzi ya Usasa. Inampa mtumizi wake uhuru wa kujaribu mbinu mpya bila ya kubanika katika sheria za sanaa zilizozingatiwa katika enzi za Usasa. Uteuzi wa sampuli ulikuwa wa kimaksudi ili kushughulikia uwakilishi wa waandishi kuhusuutandawazi. Riwaya hizi zilijumuisha: *Bina- Adamu* (Wamitila, 2002) *Musaleo!* (Wamitila, 2004) *Dunia Yao* (Mohamed, 2006) na *Babu Alipofufuka* (Mohamed, 2001). Mbinu ya uchanganuzi ilihusu yaliyomo katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Uchanganuo wa yaliyomo ulimwezesha mtafiti kuchanganua maudhui yaliyoingiliana na utandawazi ili kuonyesha uwakilishi wake. Utafiti huu ulibainisha kuwa; suala la utandawazi limewasilishwa kupitia maudhui mbalimbali ya Riwaya Mpya. Uwasilisho huu ulikuwa wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja. Vilevile, maudhui haya yaliwasilishwa kwa kutumia vipengele vya Usasaleo. Vipengele hivi vilijumuisha; uhalisia-ajabu, uasi, na mwingiliano matini, Aidha, mitazamo ya waandishi kuhusu suala la utandawazi ilidhihirishwa kupitia matumizi ya lugha yakiwemo tamathali mbalimbali za fasihi.Utafiti huu utafaidi wanafunzi, walimu, wataalam wa fasihi na Taasisi ya kuendeleza mitaala ya Kenya.

ABSTRACT

Globalisation is a phenomenon that for a long time, different literary writers have portrayed as an agent of rapid development. These developments are perceived to be eminent in the economic, political and social arena of people. Kiswahili novel writers have portrayed the concept of globalisation as integration of people, ideas, culture and values. However, some of Kiswahili novels have taken a new twist in expressing the same concept by using Postmodern elements. These elements which includes; black humor, magical realism, pastiche among others, have complicated the understanding of globalisation making it unclear. Furthermore, the intention of using these techniques in regard to globalisation has added more confusion than clarification. This study therefore, reviewed critically how postmodern techniques had developed themes in relation to globalisation and the intension of the writers towards the same. This research used Postmodernism theory: it deconstructs and refutes many aspects and guidelines that were upheld during the modernist era. This is achieved through the themes and techniques like irony, metafiction, magic realism, intertextuality among others, as used in the novels studied. The methodology involved library study and the sampling procedure was purposive. The novels studied included: *Bina- Adamu!* (Wamitila, 2002) *Musaleo!* (Wamitila, 2004) *Dunia Yao* (Mohamed, 2006) and *Babu Alipofufuka* (Mohamed, 2001). The internet was also of great significance in data collection for this study. Data analysis was done using content analysis method. The researcher used literary criticism and analysis to study these novels. It was evident in this research that globalisation was presented in different themes of new Kiswahili novel, directly or indirectly. These themes were built in different elements of postmordenism which included magical realism, fabulation, matafiction, intertextuality among others. Furthermore, their intentions about globalisation were evidenced strongly in their figurative language and the techniques of expression used. This research will be beneficial to students, teachers, researchers and the Kenya Institute of Curriculum Development.

YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI ..... **i**
HAKILINZI ..... **iii**
TABARUKU ..... **iv**
SHUKRANI ..... **v**
IKISIRI ..... **vi**
ABSTRACT ..... **vii**
YALIYOMO ..... **viii**
UTANGULIZI **1**
1.1 Usuli wa Mada 1
1.2 Suala la Utafiti 2
1.3 Madhumuni ya Utafiti 2
1.4 Maswali ya Utafiti 3
1.5 Umuhimu wa Utafiti 3
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti 3
1.7 Maelezo ya Istilahi 5
MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA **6**
2.1 Utangulizi 6
2.2 Dhana ya Riwaya Mpya na Ujenzi wa Maudhui ya Utandawazi 6
2.3 Mbinu Zinazotumika Kuangaza Utandawazi Katika Riwaya Mpya 11
2.4 Mitazamo ya Utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili 13
2.5 Misingi ya Nadharia 18
MBINU ZA UTAFITI **22**
3.1 Utangulizi 22
3.2 Muundo wa Utafiti 22
3.3 Mahali pa Utafiti 22
3.4 Ukusanyaji Deta 23
3.5 Uteuzi wa Sampuli 23
3.6 Uwasilishaji wa Deta 23
UCHANGANUZI WA DETA **27**

4.1 Utangulizi 27
4.2 Uhakiki wa Maudhui ya Utandawazi 27
4.2.1 Uongozi na Utandawazi 27
4.2.2Teknolojia na Sayansi 37
4.2.3 Utamaduni 42
4.2.4 Umaskini 44
4.2.5 Utandawazi Kuleta Mabadiliko 47
4.3 Tathmini ya Mbinu za Kuangaza Utandawazi 50
4.3.1 Uhalisia-ajabu 51
4.3.2 Vurugu la kiwakati 54
4.3.3 Mbinu ya Uasi katika Kufafanua Utandawazi 55
4.3.4 Kinaya, Masihara na Ucheshi-bwege 58
4.4 Tathmini ya Mitazamo ya Waandishi kuhusu Utandawazi 59
4.4.1 Lugha ya Mkemeo 60
4.4.2 Matumizi ya Mazungumzo 62
4.4.3 Falsafa ya Ukinzani na Kinaya 64
4.4.4 Matukio na Hali za Kiajabu 67
4.4.5 Matumizi ya Nyimbo 69
4.4.6 Sifa za Wahusika 70
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 72
5.1 Utangulizi 72
5.2 Muhtasari wa Matokeo 72
5.3 Matatizo yaliyomkumba Mtafiti 75
5.4 Mapendekezo ya Ujumbe 75
5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi 77
5.6 Hitimisho 78
MAREJELEO 80

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Utandawazi umeweza kuelezwa na wataalam mbalimbali kama utangamano au ufungamano wa watu, utamaduni, biashara na siasa (Husseini, 2010, Beerkens, 2006). Katika Riwaya Mpya ya Kiswahili, maana ya utandawazi si bayana kwa sababu waandishi wanauangaza katika misingi ya Usasaleo na Udenguzi. Utandawazi uliweza kuzuka katika miaka ya 1980 na kuanza kutumika katika fasihi miaka ya tisini (Khamis 2007). Katika riwaya ya Kiswahili, utandawazi ulianza kushughulikiwa katika miaka ya 1980 japo haukutambulika waziwazi. Miaka ya 1990 ndipo utandawazi ulibainika katika riwaya ya Kiswahili. Utandawazi ulionyeshwa katika riwaya kama mfumo wa uhusiano wa Kimataifa katika nyanja mbalimbali zikiwemo biashara, uchumi, siasa, na utamaduni. Haya yaliwezeshwa na maendeleo ya kiteknolojia ya habari yaliyofanya mataifa kuwasiliana kwa urahisi.

Tangu miaka ya 1990, waandishi mbalimbali wa riwaya wameweza kueleza mikondo mbalimbali kuhusu dhana hii. Kwa hakika, waandishi kama vile Malamg (2001), Crafts (2000) na Jauch (2001 katika kazi zao wameweza kuonyesha utandawazi kama wakala wa maendeleo hasa kwa nchi zinazoendelea. Hii ni kwa kufafanua malengo ya utandawazi kama; kuboresha maisha ya watu, kuondoa umaskini na kuimarisha uchumi. Hivyo, utandawazi umefungua milango ya biashara, masoko huru ya bidhaa na kuufanya utamaduni wa taifa moja kuingiliana na tamaduni za mataifa mengine.

Hata hivyo, waandishi wengine wa fasihi wanatofautiana na mtazamo huo na kusema kuwa utandawazi umekuwa kiini cha matatizo katika nchi hizo zinazoendelea. Kwa mfano, madhara yake yamezua matatizo chungu nzima kuliko manufaa yake. Madhara haya hujumuisha kunyonywa rasilmali za nchi hizi zinazoendelea na kuwaacha maskini zaidi. Vilevile, huhusu kuchafua uchumi, tamaduni, mazingira na kubadilisha maisha ya wananchi hao kuwa mabaya zaidi. Baadhi ya wataalam (Pilai, 2011; Kulkami, 2011; na Khamis, 2007) wanauona utandawazi kama janga kubwa hasa katika nchi zinazoendelea.

Wandishi wa Riwaya Mpya ya Kiswahili wametumia njia tofauti kueleza mitazamo yao kuhusu mchakato wa utandawazi. Mbinu hii ambayo hutumia vipengele vya Usasaleo na Udenguzi kueleza ujumbe imezua utata zaidi katika msuko wa masimulizi. Sababu ya kutumia vipengele hivi si bayana, hivyo suala la utandawazi katika Riwaya Mpya si ya moja kwa moja. Mabadiliko

katika uwakilishaji ndiyo kiini cha Riwaya Mpya. Utanzu huu umepata mtekenyo wa mabadiliko ili kuepuka kupooza na kushindwa kushawishi kwa fikra na umbuji. Khamis (2005) anaeleza kuwa kanuni ya mabadiliko haya ni kuwa chenye mwanzo (riwaya ya uhalisia) kina mwisho-sharti kichoke, lazima kipoteze nguvu na msisimko wake. Hivyo, Riwaya Mpya ikaibuka.

Madumulla (2009) kwa upande wake anaeleza kuwa mtindo huu wa Riwaya Mpya ni mbinu ya kuepuka kushtakiwa na vyombo vya serikali kwa sababu ya kushughulikia masuala tata au matatizo yanayokumba jamii. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuhakiki maudhui ya utandawazi, kutathmini mbinu zinazotumika kuangaza utandawazi kisha kutathmini mitazamo ya waandishi kuhusu utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Madhumuni haya, yalikuwa na msingi katika makisio kuwa suala kuu ambalo hurejelewa katika Riwaya Mpya ni utandawazi. Suala hili linarejelewa kwa njia mbalimbali ambazo ziliweza kubainishwa katika utafiti huu.

1.2 Suala la Utafiti

Utandawazi ni suala ambalo kwa kipindi kirefu, waandishi wa riwaya wamelisawiri kama wakala wa maendeleo. Maendeleo haya yanafasiriwa kama utangamano wa watu kimataifa kwa misingi ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hata hivyo, uwakilishi wake katika Riwaya Mpya ya Kiswahili umechukua mtindo mpya. Hii ni kwa sababu ya waandishi kuuangaza kwa kutumia vipengele vya Usasaleo na Udenguzi. Vipengele hivi vimeweza kubadilisha mtindo sahili uliozoeleka katika uendelezaji wa ploti. Aidha, sababu ya kuvitumia kuwakilisha utandawazi si bayana. Hivyo, uwakilishi wa utandawazi si sahili katika Riwaya Mpya. Kazi mbalimbali zinapendekeza utafiti zaidi kuhusu mitindo hii ya Riwaya Mpya ili kubainisha kama hadhira ya riwaya ya Kiswahili inachangamkia Riwaya Mpya na kuchangamkia sanaa hii mpya. Utafiti huu uliangaza uwakilishi wa utandawazi kwa njia hii mpya kwa ajili ya kuweka wazi namna waandishi wanavyoujenga na kuuchukulia. Utafiti huu basi ulilenga kuhakiki matumizi ya elementi za Usasaleo katika kujenga maudhui ya utandawazi na mbinu zilizotumika kuujenga na kisha kutathmini mitazamo ya waandishi wa riwaya hii.

1.3 Madhumuni ya Utafiti

i. Kuhakiki ujenzi wa maudhui ya utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili.
ii. Kuchunguza mbinu zilizotumika kuangaza utandawazi.
iii. Kutathmini mitazamo ya waandishi wa Riwaya Mpya ya Kiswahili kuhusu utandawazi.

1.4 Maswali ya Utafiti

i. Maudhui ya utandawazi yamewasilishwa vipi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili?
ii. Ni mbinu zipi zilizotumika kuangazia suala la utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili?
iii. Mitazamo ya waandishi wa Riwaya Mpya kuhusu suala la utandawazi ni ipi?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Mtindo mpya wa uwakilishaji wa Riwaya Mpya si bayana hasa walivyojenga suala la utandawazi. Hii ni kwa sababu ya vipengele vingi vinavyotumika. Kwa kuhakiki maudhui ya utandawazi na kutathmini mbinu zilizotumika katika uwakilishaji, wanafunzi, walimu na wataalam mbalimbali wataweza kunufaika haswa wanapofuatilia jinsi suala la utandawazi limebainika katika maudhui mbalimbali.

Katika kutathmini mbinu mbalimbali zilizotumika kuwakilisha utandawazi, utafiti huu uliweza kurahisisha kueleweka kwa ujumbe katika Riwaya Mpya. Hii ni kwa sababu mbinu hizi ambazo labda ni changamano kwa wanafunzi, walimu na watafiti mbalimbali zilichanganuliwa. Vilevile, suala nzima kuhusu utandawazi litaeleweka kwa wengi.

Matumizi ya lugha kisanaa ni njia mojawapo ya kuonyesha hisia za ndani za mwandishi. Hii imebainika katika kutathmini mitazamo ya waandishi wa Riwaya.

Mpya kuhusu suala la utandawazi. Ujumbe unaowasilishwa hukolea kwa fikra ya hadhira kutokana na ufundi wa lugha. Hivyo, washikadau wataimarisha ufundi wao wa lugha kwa kutumia vipengele mbalimbali vya usasaleo. Kazi hizi inaamika zitavutia wanafunzi, walimu na watafiti kuendeleza fasihi ya Kiswahili kwa jumla.

Wajibu wa Taasisi ya kuendeleza mitalaa wa kupendekeza vitabu vya fasihi katika viwango mbalimbali vya elimu utarahisishwa. Itakuwa na mawazo mapana kuhusu maudhui, uhusika na mbinu mbalimbali za kuangazia katika mapendekezo yao.

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza uwakilishi wa utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili: *Bina-Adamu!, Musaleo!, Babu Alipofufuka* na *Dunia Yao.* Riwaya hizi ni riwaya zilizoandikwa kwa mtindo mpya; mtindo wa Usasaleo na Udenguzi. Kwa kutumia mtindo huu mpya wa uandishi, waandishi wa riwaya hizi wameweza kushughulikia masuala mazito kama vile umaskini,

uongozi, ukoloni na ukoloni mamboleo. Masuala haya yanakisiwa kufungamana na utandawazi moja kwa moja. Utafiti huu ulifanyika katika maktaba za vyuo vikuu na umma. Mtandao ulikuwa wa manufaa kupata mapitio ya maandishi.

1.7 Maelezo ya Istilahi

Riwaya Mpya: Istilahi hii ilibuniwa kurejelea riwaya ya Kiswahili ambayo imechukua mkondo tofauti katika uandishi. Mkondo tofauti hujumuisha usimulizi, uhusika, mtindo na hata maudhui. Masuala haya yanawasilishwa kwa njia ya kinaya, fantasia, ucheshi, uhalisiamazingaombwe, uasi, ubunulizi mkuu miongoni mwa mengine. Aidha, ni riwaya ambayo huongozwa na Usasaleo na Udenguzi.

Riwaya tangulizi: Hurejelea riwaya ambayo; vipengele vyake kama vile; usimulizi, uhusika, maudhui na mtindo, vimeandikwa kwa njia sahili na yenye mtririko wa mawazo na mantiki. Katika riwaya hii kuna uhalisia, uwazi na mtiririko wa masimulizi.

Udenguzi: Ni istilahi inayotumiwa kurejelea udhahania wa mambo au vitu vinavyorejelewa katika kazi ya sanaa. Katika utafiti huu, udenguzi umetmika kujenga maswala mazito mazito kama vile uongozi mbaya, umaskini, ufisadi, mabadiliko katika mazingira. Aidha, udenguzi hudhihirika katika ujenzi wa wahusika ambao si binadamu bali ni mizuka na roho.

Uhalisiajabu: Kazi ya fasihi ambayo mpaka kati ya uhalisia na udhahania umefutwa na huchanganya masuala ya kihalisia na yale ya kiajabuajabu. Mambo yanayumbishwayumbishwa baina ya ulimwengu wa kihalisia na ule wa kufikirika na wa kimiujizamiujiza.

Usasaleo: Ni tapo la fasihi linayopinga na kuyaumbua masuala mengi yaliyozingatiwa katika enzi ya Usasa. Inampa mtumizi wake uhuru wa kujaribu mbinu mpya bila ya kujifunga katika sheria za sanaa zilizozingatiwa katika enzi za Usasa. Vipengele vya usasaleo vilisaidia katika kuelewa uwakilishaji wa utandawazi. vipengele hivi vilijumuisha mwingiliano matini, uchanganyishi na vurugu la kiwakati.

Uwakilishi: Jinsi jambo au kitu fulani kimedhihirishwa. Katika muktadha wa utafiti huu uwakilishi ni jinsi ambapo utandawazi umesawiriwa na wandishi wa riwaya mpya. Usawiri huu unadhihirika katika ujenzi wa maudhui, maendelezo ya wahusika, usimulizi na pia mbinu za uandishi.

Utandawazi: Istilahi hii ilibuniwa katika miaka ya themanini kurejelea ‘mfungamano’ au ‘utangamano’ wa watu, utamaduni, biashara miongoni mwa mengine. Utafiti huu ulirejelea maana ya utandawazi Kisosiolojia ambapo hufafanuliwa kama mahusiano ya kimataifa ya binadamu na taasisi mbalimbali unaorahisishwa na teknolojia ya mawasiliano.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti alipitia maandishi mbalimbali yaliyorejelea Riwaya Mpya ya Kiswahili na ujenzi wa maudhui ya utandawazi. Vilevile, mbinu ambazo zilitumiwa na waandishi wa Riwaya Mpya katika kuusawiri utandawazi zimeangaziwa katika sehemu hii. Mbinu hizi zilijumuisha uasi, kinaya, fantasia, mwingiliano matini na vurugu la kiwakati. Mitazamo ya waandishi kuhusu suala la utandawazi imerejelewa kwa kuonyesha maoni kwa ujumla na kisha kulinganisha na waandishi wa Riwaya Mpya. Michango na pengo katika mapitio hayo ya maandishi mbalimbali ilifafanuliwa. Hatimaye nadharia ya Usasaleo, mihimili yake na jinsi ilivyoongoza utafiti huu imejadiliwa.

2.2 Dhana ya Riwaya Mpya na Ujenzi wa Maudhui ya Utandawazi

Fasihi ni sanaa inayomhusu binadamu kwa namna maalum na kipekee. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa fasihi ni sanaa itumiayo maneno ili kutoa picha halisi ya mwanadamu akiwa maishani mwake; mahusiano yake na viumbe vingine, migogoro yake na mazingira, shida zake, raha zake, matumaini yake na jinsi anavyopiga hatua katika maendeleo yake, (Ameir, 1983). Ntarangwi (2004) anatambua matawi ya fasihi kama andishi na simulizi. Khamis (2005) anazua dhana ya riwaya tangulizi na Riwaya Mpya katika fasihi andishi. Mawazo ya wataalam hawa yalikuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti hasa katika kuweka wazi lengo la fasihi na riwaya ya Kiswahili kwa jumla.

Khamis (2010) anamnukuu Kettle (1959) ambaye anatetea mapinduzi katika uandishi wa riwaya kuwa mapinduzi makubwa katika jamii za watu hubadilisha urazini; na si kupindua hisia zao za kijamii tu bali pia mitazamo, falsafa na sanaa zao, (dhana ya Riwaya Mpya). Kazi hii ya Khamis (2010) inaelezea mtindo wa uandishi katika fasihi kuwa umechukua mkondo ambao ni tofauti na ule wa kawaida. Mabadiliko haya yanachochewa na utumwa wa mfumo wa uongozi, ambao ulisisitizia waandishi kuandika kwa kusifu au kueleza matatizo ya jamii kwa njia sahili. Khamis (2010) anaonyesha mapinduzi au mabadiliko katika uandishi wa riwaya kwa jumla. Mabadiliko haya vilevile, yameathiri usawiri wa maudhui mbalimbali katika riwaya hii. Jambo ambalo si wazi katika maoni haya ya Khamis, ni kiini na sababu ya mabadiliko haya hasa katika karne ya 21. Utafiti huu uliangaza jinsi mabadiliko katika uandishi wa riwaya yanaathiri mawazo au

maudhui mbalimbali katika Riwaya Mpya. Aidha, ikiwa mabadiliko haya huathiri mitindo ya maisha ya wanaolengwa katika jamii. Hili limeshughulikiwa kwa kuhakiki masuala makuu katika Riwaya Mpya ya Kiswahili na mahusiano yao na utandawazi.

Bergonzi (1972) anaelezea kuwa awali uhalisia katika kazi za fasihi ulikuwa njia bora ya kuwasilisha maudhui. Hii ni kwa sababu ya uwazi na mtiririko wake wa mantiki. Bergonzi anafafanua uwazi huu kuwa ulikuwa njia bora ya kufichua na kueleza umma matatizo ya kijamii na kisiasa kinagaubaga. Pia, uhalisia huu ulisaidia wananchi wa kawaida katika riwaya tangulizi. Mawazo haya ya Bergonzi yana umuhimu katika kuelewa histroria ya riwaya tangulizi. Hata hivyo, swali kuu ni: Je, pasipo na uhalisia ujumbe hauwezi kufikishwa? Wataalam wengine kama vile Walibora (2010) na Khamis (2010) wanakubaliana kuwa riwaya tangulizi zilikita katika uhalisia mkavu. Kwao, Riwaya Mpya ni utanzu wa fasihi uliopata uamuzi wa mabadiliko ili kuepuka kupooza na kushindwa kushawishi kwa fikra na umbuji. Mabadiliko haya ni kuondoka kwa kazi ya fasihi kutoka sura iliyozoeleka na kwenda sura mpya. Upya huu umo kwenye usanii na maudhui. Maoni ya Walibora na Khamis yanathibitisha kuweko kwa mabadiliko katika uandishi wa riwaya. Maswali mengi yanaibuka katika maoni yao, kwa mfano; kuna umuhimu gani katika kubadilisha usanii na maudhui? Je, mabadiliko haya yanabadilisha ujumbe na mitazamo ya wanaolengwa? Na je, upya huu wa usanii na maudhui yanalenga kuumba au kuumbua nini katika Riwaya Mpya ya Kiswahili? Utafiti huu uliweza kuhakiki upya wa maudhui katika Riwaya Mpya na jinsi upya huu huathiri uwasilishaji wa ujumbe lengwa hasa kwa kuzingatia suala kuu la utandawazi.

Khamis (2005) anatafsiri maoni ya Roth (1982) katika kueleza upya wa kisanaa kuwa ni mambo ambayo yanazua mshangao na woga, pia kiini cha kukata tamaa. Anaorodhesha majungu kashfa na kasheshe, kichaa, upumbavu, usalihina wa uwongo, kelele, kama vitu vilivyomo katika ukweli na ndoto wakati mmoja na nguvu za kubadilisha karne hii. Aidha, hubadilisha maisha ya wanajamii. Roth anafafanua upya wa usanii na maudhui unaoangaziwa na Khamis (2010) Walibora (2010) na Bergonzi (1972). Wazo hili la Roth huzua mtafaruku hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya riwaya tangulizi zilikuwa na mitindo hiyo ya uwasilishaji maudhui na usanii. Kwa mfano, riwaya za Shaban Robert zilikuwa na kasheshe, kichaa, upumbavu, miongoni mwa

mengine: ilibainika katika kuhakiki ujenzi wa maudhui katika Riwaya Mpya. Aidha, utafiti huu uliweka wazi nia na athari ya mabadiliko kwa lengo la kuelewa uwakilishaji wa utandawazi.

Kichocheo cha Riwaya Mpya ni kipindi cha mwamko sanaa ambapo kulitokea ongezeko la hamu ya utafiti na ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia. Madumulla (2009) anaeleza kuwa utafiti na ugunduzi haukuhusu viwanda na zana bora zaidi tu bali pia juhudi za kuutalii na kufahamu vizuri zaidi ulimwengu. Juhudi hizi ziliakisiwa kuwa nyenzo za kuufagilia ubepari wa kawaida. Hivyo, utaratibu wa kusawiri kwa kina maisha ya jamii katika uhalisia wake kwa kutumia lugha ya kila siku na mazingira yaliyozoeleka uliimarishwa. Utaratibu huu ulikuwa wa kina na mpana ukilinganishwa na ule wa maandiko tangulizi. Hii iliwezekana kutokana na elimu, ukomavu wa uchumi, maendeleo ya sayansi na teknolojia na kusetirika kwa jamii. Japo maoni haya ya Madumulla ndiyo yalikuwa msingi wa utafiti huu, suala la utandawazi kama kiini cha mabadilko halikuwekwa wazi. Utafiti huu uliweza kuonyesha jinsi utandawazi ulivyoathiri mabadiliko katika uandishi wa Riwaya Mpya, hasa katika usanii na maudhui.

Ujenzi wa maudhui katika Riwaya Mpya umechukua mkondo mpya, hasa kwa sababu ya kuangaziwa katika misingi ya Usasaleo na Udenguzi. Kezilahabi (1990) anafafanua kuwa lengo la mtindo huu ni kuchanganua matatizo ya jamii kwa jicho la ndani. Anaonyesha mikondo miwili ya kutazama maisha katika riwaya hii: Kiafrika na mkondo wa mtazamo wa matatizo haswa ya Kimataifa. Maudhui haya huwasilishwa kwa njia ya mazingaombwe. Mitazamo katika tasnifu yake ya uzamifu, Kezilahabi (1985) anaonyesha wazi kuwa Riwaya Mpya ina hali ya kupotosha kwa maksudi, muundo, sura au umbo la riwaya ya uhalisia tunayoijua kwa kupunguza au kuingiza vitu kama vile nambari, picha, orodha, herufi yombo, herufi-mlazo na kadhalika, au kuingiza vitu ambavyo kwa kawaida haviketi katika mwili wa riwaya tuliyozoea (riwaya tangulizi). Maoni ya Kezilahabi yanazua utata zaidi hasa anapokosa kueleza nia ya Riwaya Mpya kupotosha wasomaji kwa maksudi, sababu ya kuingiza visivyostahili katika riwaya hii na kutumia mbinu kadha katika ujenzi wa maudhui. Vilevile, si bayana kinachopotoshwa kwa maksudi na vitu vipya vinavyoingizwa katika riwaya hii. Ni kutokana na mtazamo wa Kezilahabi kuhusu ujenzi wa maudhui katika Riwaya Mpya ndipo utafiti huu ulibainisha nia ya kuingiza visivyo mtindo katika riwaya hii na mbinu mbalimbali zilizotumiwa kuwasilisha ujumbe. Haya yalibainika kwa kuhakiki maudhui mbalimbali ya utandawazi.

Kipengele cha uhusika vilevile kimeweza kuumbuliwa upya katika Riwaya Mpya. Mara nyingi wahusika wanaobuniwa si wahusika wa mwili na roho. Khamis (2005) anaeleza kuwa sababu ya uhusika huu ni kumwezesha mwandishi kutoonyesha hamu yeyote ya kumchora sura, wasifu na tabia zake katika kutimiza maudhui fulani. Hili linatumiwa na waandishi kama chombo cha kusukuma mbele hadithi. Maswali ya kimsingi katika maoni ya Khamis ni kuwa: Ni jinsi gani mwandishi anapima kufaulu kumchora sura, wasifu na tabia za mtu katika uhalisia anapotumia wahusika ambao si wa mwili na roho? Na je, majina ya wahusika hawa wasio wa mwili na roho, yana uhusiano na majina ya watu halisi? Utafiti huu uliweza kuhakiki kama kweli ujumbe unaolengwa hufikishwa hasa mwandishi anapokosa kutumia wahusika wasio wa mwili na roho. Aidha, iwapo majina ya wahusika kama vile K, na Ndi, mashiko katika kuendeleza na kuwasilisha ujumbe unaolengwa.

Gromov (1998) anaeleza kuwa kila mhusika ni chombo cha kusaidia mwandishi kukamilisha lengo lake. Hivyo, wahusika wengine hupewa nguvu za kichawi na miujiza. Mtindo huu wa uhusika katika Riwaya Mpya ni mchanganyiko wa zao la Kiafrika, mbinu za Kimataifa na vilevile, mbinu ya usasa na kuingia usasabaadaye. Gromov anazua hoja ya mwandishi wa Riwaya Mpya kuwa na uwezo wa kuumba na kuumbua mhusika jinsi anavyopenda. Uumbaji wa aina mbalimbali wa wahusika katika Riwaya Mpya uliwezesha utafiti huu kuhakiki maudhui ya utandawazi. Mtazamo huu ulikuwa wa manufaa katika kutathmini maudhui hayo. Khamis (2005) kwa upande wake anaonyesha kwamba mbinu hiyo ya uhusika si mpya katika Riwaya Mpya bali imevumbuliwa au kuumbuliwa upya ili kuonyesha dhana ya historia, dhana ya sasa na dhana ya usoni. Mawazo haya ya Gromov (1998) na Khamis (2005) yalidhihirika katika utafiti huu hasa katika kukamilisha ujenzi wa maudhui kupitia tabia na majukumu waliopewa wahusika hawa.

Kando na uhusika, upya wa maudhui katika Riwaya Mpya hudhihirishwa kwa simulizi. Gromov (1998) anaelezea kuwa simulizi za Riwaya Mpya zinaonyesha tabia ya kutofuata mtiririko sahili moja kwa moja. Khamis (2007) anatambua simulizi za Riwaya Mpya kama za kuoanisha sauti mbalimbali katika mchangamano mkubwa usioshikana kabisa na mantiki ya wakati na pahala kama hadhira zetu zilivyozoea. Usimulizi humwaga na kufululiza matukio, mawazo, falsafa na siasa ya mwandishi na kuyaacha yashikane na mtiririko wa hadithi- bila ya kiungo bayana cha ploti kupitia visababisho na athari za visababisho katika mtiririko wa wakati na mahali.

Walibora (2010) anarejelea usimulizi wa riwaya hizi kama matatamatata kwa kuwa kazi za sanaa zinatumia sifa bainifu za uhalisiamazingaombwe kama nyenzo za kuakisi hali halisi ya udhaifu, kuyumbayumba na ukosefu wa uthabiti na udumu katika maisha Bara la Afrika na Ulaya. Utafiti huu ulihakiki jinsi usimulizi huu wa kimatatamatata huchangia katika uwasilishi wa maudhui yanayoingiliana na utandawazi.

Khamis (2007) anaelezea kwa undani kuwa, maudhui ya Riwaya Mpya yanalenga kusawiri ukosefu wa udhati wa kijamii, kisiasa na kiuchumi hasa katika mataifa ya Afrika Mashariki. Haya yanaelezwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja (fantasia) ili kuwaruhusu waandishi kujitakasa hasira yao kwa mtindo wenye fujo na haiba, ili kujaribu kuakisi mitafaruku na uozo katika maisha ya kisasa nchini Kenya na Tanzania. Williams (1999) ana maoni sawa na hayo anapoeleza kwamba mikakati ya kimajaribio katika sanaa hulenga kuchanganua ukosefu wa uthabiti katika michakato ya kijamii. Kwa ufupi, waandishi hawa wanaonyesha jinsi matini huingiliana katika vipengele vingi vya kiujumi, kimtindo, na kimaudhui. Isitoshe, riwaya hii mpya imeandikwa kwa kuzingatia kaida na kunga za uhalisia-mazingaombwe ambao umejenga jumuia pana na inayoendelea kupanuka kote duniani kila uchao. Hili linaacha hadhira nyingi kuchanganyikiwa zaidi. Utafiti huu ulihakiki yanayosababisha mitafaruku na uozo katika maisha ya kisasa, kwa kuzingatia maudhui ya utandawazi.

Vilevile, riwaya hii inaonyesha mikakati ya kimajaribio katika sanaa, uozo na ukosefu wa udhabiti katika mchakato wa kijamii; hivyo, ni njia bora ya waandishi kutoa hasira zao. Maoni ya wataalam hawa kuhusu simulizi za Riwaya Mpya yaliweza kuongoza utafiti huu hasa kuhakiki ujenzi wa maudhui ya utandawazi. Walibora (2010) anatoa mfano wa riwaya ya *Dunia Yao* kama mfano wa misukosuko na mawimbi ya mabadiliko na ukosefu wa uthabiti Afrika Mashariki na hasa visiwani Zanzibar baada ya uhuru na katika vuguvugu la siasa za vyama vingi. Usimulizi katika Riwaya Mpya ulikuwa msingi wa maudhui yaliyochaguliwa katika kupambanua uwasilishi wa utandawazi. Maoni ya wataalam hawa yalisaidia utafiti huu kuhakiki ujenzi wa maudhui ya utandawazi.

2.3 Mbinu Zinazotumika Kuangaza Utandawazi Katika Riwaya Mpya

Uhalisia-ajabu ni mtindo wa uandishi unaotawala Riwaya Mpya. Masuala yanayorejelewa yanaangaziwa kupitia njia za kiajabuajabu. D'Haen (2005) anarejelewa na (Walibora, 2010) anapofafanua maoni ya Roth kuhusu uhalisiamazingaombwe kama mtindo unaotumika katika kazi za fasihi. Anaonyesha sifa za Usasaleo kama vile kujirejelearejelea, uziada uliopindukia, uanuwai, mseto wa vitu, mwingiliano matini, kucheza na kuyumbisha uthabiti wa wahusika na usimulizi. Vilevile, kumchanganya msomaji kwa maksudi na hali kadhalika kufuta mipaka ya dhana, vitu, au hali tofauti (ibid: 2001). Khamis anarejelea mabadiliko haya kama mengi ya kushangaza na kutatanisha (Khamis, 2007). Muundo na vitomeo vyake vya fani na umbuji katika mbinu inayojaribu kuasi kwa maksudi uhalisia mkongwe, uhalisia mkavu. Ni wazi kuwa mtindo huu huzua taswira fulani katika kujenga dhana au wazo fulani. Japo yana umuhimu katika kazi za fasihi, nia ya kutumia mbinu si wazi hasa katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Utafiti huu uliweza kuweka bayana nia na athari za kutumia mbinu hizi haswa suala la utandawazi linaposhughulikiwa.

Mbinu ya fantasia kwa mfano, hujitokeza katika kipengele cha riwaya hii mpya. Mbinu hii hudhihirika katika usimulizi, uhusika, mwingiliano wa wahusika, mwanya wa kisaikolojia ndani ya vichwa vyao, ndoto zinazoingiliana na ukweli wa mambo, matukio katika mshikamano wa uzoefu na ugeni wa mambo, mazingira na jinsi yanavyoshikana na matukio na kufungamana na wahusika kihistoria, umataifa, usayansi na mabaki ya uchawi, ushirikina na mazingaombwe; na hatimaye mwingiliano matini na mchezo wa lugha, kupelekea wakati mwingine hata kuingia katika uga wa kimataifa. Scholes na Kellogg (2006) wanakubaliana kuwa, utanzu wa riwaya ni mchanganyiko vuguvugu yaani usio na mashiko thabiti, vilevile, ni mchanganyiko wa ubunifu na sayansi na ngano kwa upande mmoja na kwa upande wa pili, wa historia na uigaji. Mawazo ya wataalam hawa ni ya kijumla, hayaonyeshi umuhimu wa matumizi ya fantasia na malengo yake katika Riwaya Mpya. Japo inaaminika kuwa zilikuwa mbinu zilizotumiwa kuwasilisha fasihi simulizi, kuingizwa katika Riwaya Mpya imeleta utata zaidi. Utafiti ulitathmini jinsi mbinu hii ilitumika katika uwakilishi wa suala la utandawazi.

Usasaleo haulengi tu mwanzo mpya. Hulenga pia maana ya uasi dhidi ya kaida zilizopo au zilizokuwepo (Walmsley, 2006). Becket ni mfano wa mtunzi bwege aliyevunja kaida hizi katika riwaya, tamthilia na ushairi. Walmsley anasema kuwa Usasaleo hudunisha mantiki ya muumano wa kazi kama vile msuko, uhusika, matumizi ya lugha, muundo wake miongoni mwa mengine.

Huwa unaumbua au unaasi kaida ambazo zimekuwa zikizingatiwa kama sheria katika utunzi. Vilevile, huasi mpangilio kiwakati, uhusika unaohalalika kisaikolojia na msuko rasmi. Mawazo haya kwa hakika ndiyo huongoza ujenzi wa Riwaya Mpya. Warren na Wellek (1986) wanatambua kuwa katika Usasaleo pana uasi wa kauli na kuwa, fasihi huzingatia au huiga yaliyomo maishani. Hivyo, huwa kuna upingaji wa baadhi ya mawazo. Mathalani, muundo wa tangu zamani wa riwaya au jukumu la msimulizi. Aidha, huhusisha mbinu nyingine za kusimulia hadithi yakiwepo matumizi ya fantasia kama viroja na visasili au vipengele vya bunilizi pendwa kama vile zile za sayansi. Mbinu hii ya uasi ilikuwa muhimu katika kutathmini uwakilishishaji wa utandawazi katika riwaya hii mpya. Warren na Wallek wanathibitisha kuwa uasi ni mojawapo ya mbinu katika fasihi. Utafiti huu ulihakiki jinsi uasi unavyojitokeza katika riwaya hii. Vilevile, swali la kipi kinachoasiwa na sababu ya uasi huu katika riwaya hii limejibiwa na utafiti huu.

Hutcheon (1989) anatambua kuwa Usasaleo umevamiwa na mazingaombwe ambao hutambulika na matini ya kinaya ambayo huwasilishwa kwa utani. Japo hazikuanza na Usasaleo, zimetumika sana katika vuguvugu hili. Hutcheon anaonyesha kuwa mbinu hii ya Usasaleo huangazia masuala mazito kwa njia ya mchezo. Utafiti huu ulitambua masuala mazito yanayorejelewa katika Riwaya Mpya. Masuala haya yalirejelewa kwa kuhakiki maudhui mbalimbali na jinsi yalivyowasilishwa. Utafiti huu vilevile, ulibainisha jinsi masuala haya mazito yanavyoshughulikiwa kwa njia ya mchezo au kwa njia ya kejeli. Nia ya waandishi hawa kutumia mbinu ya kinaya, masihara na ucheshi kuangaza utandawazi pia ilibainishwa.

Wamitila (2003) anaonyesha dhana ya mwingilianomatini katika Usasaleo. Hii ni dhana inayotumiwa kueleza kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya kifasihi. Barthelme (1983) anarejelea mwingilianomatini katika Usasaleo kama hekaya au hadithi ambazo zinahusiana na kazi iliyoandikwa kwa namna moja au nyingine. Tylor (2004) anaonyesha kuwa Usasaleo huhusisha wingi matini pale kazi ya fasihi imehusisha masuala mbalimbali kama vile ya kifalsafa, ya kilimo, ya uchawi miongoni mwa mengine. Aidha, pale mkondo wa wazo la kazi fulani ya kifasihi unategemea pia mawazo ya nje yanayofungamana na kazi yenyewe kama vile historia au ngano fulani.

Tylor (2004) pia, anaeleza kuwa wingi matini hurejelea matini za awali na kuzirekebisha ili ushauri wa mwandishi ubaki pekee. Hivyo, katika Riwaya Mpya, hakuna kazi huru. Wamitila (2003) anatoa mfano jinsi ya kushughulikia mwingiliano matini katika Riwaya Mpya kwa

unukuzi au kudondoa, wizi wa uandishi na wigobezi. Anaonyesha kuwa wafuasi wa mbinu hii wanashikilia kuwa kazi za fasihi huingiliana na kuhusiana katika kile kinachoitwa ‘mwanda wa kimwingiliano matini’. Mbinu hii iliwezesha utafiti huu kuangazia mawazo sawa baina ya waandishi kuhusiana na ujenzi wa maudhui ya utandawazi na kutathmini mitazamo yao. Hutcheon (1989) Cooper (2003) na Wamitila (2003) wanatambua mbinu za uhalisia-ajabu pamoja na vurugu la kiwakati: mbinu ambazo ni za kimsingi katika kutambua mitazamo na uhakiki wa maudhui ya waandishi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Maoni ya wataalam hawa, yalisaidia utafiti huu kutathmini uhusiano wa mbinu ya mwingilianomatini na suala la utandawazi katika Riwaya Mpya teule: *Bina-Adamu!, Musaleo!, Babu Alipofufuka* pamoja na *Dunia Yao*.

2.4 Mitazamo ya Utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili

Tafiti kadha zimefanywa haswa kuhusu: maudhui, uhusika, mitindo, usimulizi na fani katika riwaya ya Kiswahili. Mabadiliko katika utanzu huu wa riwaya yameweza kuangaziwa na wataalam wachache. Watalaam hawa wemeweza kutoa ulinganisho wa Riwaya Mpya ya Kiswahili na riwaya zingine kama za Kiingereza. Aidha, upya wa usanii na maudhui umefafanuliwa na wataalam. Japo utandawazi umegusiwa na wataalam katika kazi zao kuhusu Riwaya Mpya, maelezo yao yamekuwa ya kijumla na hayajaonyesha uzito unaopewa suala hili katika Riwaya Mpya. Khamis (2005) anaeleza kwa kina mabadiliko katika riwaya yakiwemo usanii, mtindo, uhusika, usimulizi na maudhui. Mabadiliko haya yana msingi ya kuendeleza usanii katika kiwango kipya na pia, kutalii vionjo mbalimbali ya usanii. Mabadiliko katika kuangaza maudhui pia, hudhihirika katika kazi hii. Kazi hii ya Khamis ilikuwa dafina kubwa katika utafiti huu hasa katika kutambua mabadiliko hayo yanayorejelewa. Hata hivyo, kazi hii ilikosa kubainisha nia halisi ya mabadiliko haya haswa katika kuangazia masuala mazito katika jamii. Utafiti huu uliweka wazi sababu za mabadiliko haya na nia ya upya wa usimulizi na maudhui kwa mintarafu ya utandawazi.

Ulinganisho wa Riwaya Mpya ya Kiswahili na riwaya ya lugha zingine umezua mjadala kuhusu upya wa riwaya ya Kiswahili. Walibora (2010) analinganisha riwaya ya *Dunia yao* na riwaya ya *The Tin Drum.* Ulinganisho huu unazua masuala kadha hasa ya kimaudhui, nadharia, masuala ya falsafa, usimulizi na uhusika. Inabainika kuwa riwaya hizi mbili zinaakisi ukosefu wa udhabiti wa kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kazi hii ya Walibora pia, ilikuwa kichocheo cha utafiti huu. Katika ulinganisho huo, si bayana kinachosababisha ‘ukosefu wa udhabiti wa kijamii, kisiasa na

kiuchumi'. Mapendekezo yake ya utafiti zaidi kuhusu iwapo hadhira ya riwaya za Kiswahili inachangamkia riwaya hizi za kimajaribio na kutambua ubora wa kisanaa kwenye kazi hizi, ilichochea utafiti huu. Hivyo, utafiti huu ulitathmini mbinu zinazotumika katika uwakilishi wa utandawazi katika Riwaya Mpya. Utafiti huu uliweka bayana kisababisho cha ukosefu wa udhabiti katika jamii, kisiasa na kiuchumi kwa kuhakiki maudhui za utandawazi. Utafiti huu uliainisha mbinu mbalimbali zilitumika kuwasilisha mawazo makuu ambayo labda yanaweza kufanya hadhira ichangamkie au ichukie usanii huu mpya.

Suala la nguvu na utambulisho linakisiwa kuwa chanzo cha utandawazi katika Riwaya Mpya. Diegner (2005) katika mahojiano yake na Wamitila, ni dhahiri kuwa suala la utandawazi limekithiri katika Riwaya Mpya. Matumizi ya ishara yametawala kwa lengo la kuwakilisha ufalme au utawala fulani. Katika mahojiano haya, maswali mengi yanaibuka katika kuelewa suala la utandawazi katika Riwaya Mpya. Kwa mfano, Wamtila ambaye ni mwandishi wa Riwaya Mpya hana uhakika na jinsi suala la utandawazi lilishughulikiwa. Anakisia kuwa nguvu na utambulisho huenda ikawa kichocheo cha kuenea kwa utandawazi. Wamitila katika mahojiano yake na Diegner, anawapa changamoto wahakiki kutegua nafasi ya Riwaya Mpya kwa jumla katika jamii. Utafiti huu ulihakiki nafasi ya nguvu na utambulisho katika uwasilishi wa utandawazi. Hivyo, maoni ya Diegner na Wamitila yalisaidia utafiti huu kutambua nafasi ya Riwaya Mpya kwa kuhakiki maudhui mbalimbali yanaoingiliana na utandawazi.

Khamis (2007) anarejelea matumizi ya lugha katika Riwaya Mpya. Anafafanua lugha ya usasabaadaye, ujenzi wa fantasia na uhalisia mazingaombwe, lugha ya mchanganyondimi, lugha na falsafa, lugha na mvunjiko wa utambulishao na lugha zenye mnasaba na utandawazi kama lugha ya Riwaya Mpya. Kazi hii ya Khamis, ilidhihirisha jinsi lugha ni nyenzo ya msingi ya kubuni na kuwasilishia kazi ya fasihi. Hivyo, haina budi kukidhi kimaumbo, kimuundo na kikazi, mahitaji ya kazi ya fasihi na mahitaji ya jamii yenyewe inayobadilika. Khamis (2005) amefasiri mawazo ya Kettle (1959) kuwa, mapinduzi makubwa katika jamii za watu hubadilisha urazini na si kupindua mahusiano yao ya kijamii tu, bali pia mitazamo, falsafa na sanaa zao (utandawazi katika muktadha huu). Utandawazi katika riwaya hii unaibua matatizo ya kisaikolojia na kisosholojia, mkondo mzima anachukua mwanadamu kubadilika na kuwa mnyama.

Ni kutokana na matumizi ya lugha yaliyotajwa na Khamis, ndipo utafiti huu ulitathmini mbinu zilizotumika katika kuwasilisha suala la utandawazi. Kazi hii ya Khamis ilisaidia utafiti huu kuweza kutambua jinsi utandawazi ulivyodhihirishwa katika Riwaya Mpya. Japo ilirejelea matumizi ya lugha kwa jumla, lengo la matumizi hayo ya lugha hayakujitokeza wazi hasa katika kushughulikia kwa kina matatizo ambayo yanaukabili ulimwengu wetu leo. Utafiti huu ulipiga hatua ya kuhakiki nia ya matumizi hayo ya lugha katika kushughulikia masuala mazito katika jamii yetu, haswa kwa kutathmini mitazamo yao kuhusu suala la utandawazi.

Umuhimu wa utandawazi umeshughulikiwa na wataalam mbalimbali katika kazi zao za fasihi. Wamitila ameonyesha utandawazi kama chombo muhimu cha kufupisha masafa (Wamitila, 2003). Hii imefanya dunia kuwa kama kijiji kidogo hasa katika uwanja wa mawasiliano na uchukuzi. Watu husafiri bila tatizo na kwa muda mfupi na hata kuwasiliana wakati wowote bila kujali masafa kati ya mpokeaji. Mtazamo huu kwa hakika ni bayana katika riwaya tangulizi za Kiswahili. Riwaya hii huonyesha jinsi utandawazi umeleta faida kubwa sana katika mawasiliano na uchukuzi. Kwa mfano, kufanikiwa kwa mhusika mkuu katika riwaya ya *Siku Njema* (Kongowea) ni zao la utandawazi. Siku njema hujiri kwa mhusika huyu kwa sababu ya utandawazi. Mawazo haya ya Wamitila yameweza kutatanisha hasa kutokana na ujumbe kuhusu utandawazi katika riwaya zake. Mawazo yake hapa ni kama upanga ukatao kuwili. Utafiti huu uliweza kubainisha ufaafu wa mawazo haya kwa kutathmini mitazamo ya waandishi wa Riwaya Mpya ya Kiswahili kuhusu utandawazi.

Wataalam wengine kama vile Ruigrok na Tulder (1995) Jauch (2001) na Offiong (2001) wameweza kuangazia suala la utandawazi katika fasihi kijumla. Wataalam hawa wamesifia mchakato wa utandawazi hasa katika nchi zinazoendelea. Hii ni kwa sababu hatimaye utaboresha maisha ya watu wote duniani. Pia, wanatambua utandawazi kama ngazi ya biashara baina ya nchi, masoko huru ya bidhaa, na kutangamanisha tamaduni mbalimbali jinsi inavyodhihirika katika tanzu mbalimbali za fasihi. Offiong (2001) anatambua kuwa utandawazi umepata kasi kubwa ya kuwekeza na kuendeleza mitaji katika biashara mbalimbali na kupata faida kubwa kiuchumi na kiutamaduni; ukisaidiwa na maendeleo makubwa ya kiteknolojia yaliyopatikana karibuni, hasa ya vyombo vya mawasiliano ambavyo vimefupisha au kuondoa vikwazo vya masafa na wakati. Vyombo hivi vya habari hukisiwa kuwa ni vitabu vya fasihi. Utafiti huu uliweza kutathmini ikiwa uwakilishi wa utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili una mtazamo huu. Aidha, mawazo ya wataalam hawa yalichochea umakinifu wa kutaka kujua ukweli

wa maoni yao kwa kutathmini maudhui ya utandawazi na mitazamo ya waandishi wa Riwaya Mpya.

Khamis (2007) anaonyesha hisia zake kuhusu kuvunjika kwa utambulisho wa kila kitu kwenye Riwaya Mpya, uharibifu mmoja mkubwa sana wa utandawazi ni ule wa nguvu zake za kuvunja na kuharibu utambulisho wa watu katika viwango mbalimbali: kibinafsi, kiinchi au taifa, kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kidini. Mtu binafsi hajielewi tena kwa sababu hana pahala pa kusimama katika kudai haki zake za msingi kama vile kuweza kupata kazi ya kumwendeshea maisha yake kwa sababu utandawazi umesababisha kununuliwa kwa viwanda, benki kuchukuliwa, machimbo ya madini na rasilmali nyingine kuhodhiwa, vyombo vya huduma vya wananchi kama mashirika ya usambazaji umeme vimebinafisishwa, huduma za maji na mafuta na sehemu ya shule na hospitali hazimo tena mikononi mwa serikali za wananchi. Kiinchi au kitaifa utandawazi umevunja nguvu na uwezo wa maamuzi ya nchi kiuchumi na kijamii. Nchi na taifa lazima zifuate masharti ya vyombo vinavyotetea utandawazi kama vile WTO. Kwa maneno mengine nchi changa ambazo haziwezi kujitegemea, hazina tena sauti katika mambo ya kiuchumi bali pia katika yale ya kisiasa na ya kidunia. Kiutamaduni, nchi changa zimekuwa nchi pokezi za tamaduni za wageni na hasa zile mbaya, hata maana ya utandawazi inageuka kuwa utanda-upande-mmoja. Mawazo haya yalisaidia utafiti huu katika kuhakiki jinsi utambulisho ulivyovunjika hasa kwa kuzingatia maudhui ya utandawazi.

Malamg (2001) anashikilia kuwa maudhui mbalimbali katika tanzu za fasihi yanatokana na utandawazi. Anaeleza kuwa kando na tanzu hizi, fasihi ya Kiswahili husawiri utandawazi kama kiini cha mashindano ya jumuiya haswa katika kuzalisha rasilmali na kutoa bidhaa. Mashindano haya huwezesha kuundwa kwa bidhaa zenye thamani na hata huduma wa hali ya juu kwa wateja. Malamg anaonyesha kuwa wahusika wanaumbwa kuonyesha kuwa ajira nyingi katika nchi zinazoendelea ni matunda ya utandawazi. Kampuni mbalimbali kwenye masimulizi zimeweza kuwaajiri watu na kuwapa kiinua mgongo. Kando na hayo, uwekezaji umeimarishwa baina ya wananchi. Talanta zimetekwa na kuimarishwa kwenye kampuni hizi. Mtaalamu huyu pia, anazua hoja kuwa uvumbuzi na usambazaji wa ujuzi ni zao la utandawazi kupitia elimu. Mtazamo huu wa Malamg unaendelezwa na Khamis (2007) kama ukweli japo utandawazi huo hauna neema kwa nchi za dunia ya tatu pekee. Mawazo ya Malamg yanaegemea katika matunda ya utandawazi, mawazo ambayo yalikolea katika riwaya tangulizi. Utafiti huu uliweza kutathmini

ikiwa malengo ya utandawazi ya kueneza maarifa na talanta ni halali hasa kwa muktadha wa Riwaya Mpya.

Crafts (2000) anaonyesha jinsi majukumu makuu ya utandawazi yameweza kuathiri uandishi wa riwaya hasa katika maudhui na uhusika. Malengo matatu makuu yakiwemo: kuboresha maisha ya watu, kuondoa umaskini na kuimarisha uchumi. Anajadili kuwa malengo hayo yameweza kujengeka katika sehemu nne: kwanza ni biashara ambapo huzua ushirikiano wa uuzaji bidhaa toka nchi moja hadi nyingine (kuimarisha uchumi). Pili ni uwekezaji mitaji, ambapo watu wenye uwezo duniani huwekeza mitaji yao katika nchi maskini. Tatu ni uhuru wa kusafiri, ambapo watu huruhusiwa kutoka nchi moja hadi nyingine kutafuta ajira na maisha bora. Mwisho ni kuenea kwa maarifa (Teknolojia) ambayo huboresha mawasiliano na mfumo wa upashanaji habari. Maoni haya ya Crafts yanaambatana na yale ya wataalam wengine Jauch (2001) Offiong (2001) Malamg (2001) Kulkarni (2011) Christian (2010) na Ruigrok na Van Tulder (1995). Katika utafiti huu, majukumu haya makuu ya utandawazi yalitathminiwa na kulinganishwa na mitazamo ya waandishi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili.

Murray (2000) anaonyesha kwamba utandawazi si dhana kongwe yenye sifa mpya kamwe, bali ni upeo wa dhana kongwe yenye sifa mpya ya kutumia maendeleo. Maendeleo yanaakisiwa kupatikana kiteknolojia, ambapo hatimaye hunyonya utajiri wa nchi zinazoendelea. Madhara ni kuwaacha watu wa nchi hizo kuwa maskini zaidi kuliko walivyokuwa zamani. Isitoshe, pia huchafua uchumi, tamaduni, mazingira na maisha yao watu hao vibaya, hadi kufikia nchi hizo kudharauliwa na kuonekana si lolote si chochote katika fikra ya dunia hivi leo. Khamis (2007) anaunga mkono maoni haya katika kurejelea maudhui mbalimbali katika Riwaya Mpya za Kiswahili. ILRIG (1998) linabainisha kuwa, mabadiliko yanatokana na upeo wa matatizo ya kiuchumi ya kimataifa. Haya yaliyotoka mwanzoni mwa miaka ya 1970 ambayo yalisababishwa na maslahi ya kibiashara na utashi wa mataifa makubwa yanayolenga kila siku kupata faida kubwa kupita kiasi. Utafiti huu ulidhihirisha uhalali wa mawazo haya kwa kurejelea Riwaya Mpya ya Kiswahili.

Gromov (1998) anafafanua kuwa waandishi wa Riwaya Mpya wanapinga kwamba utandawazi hauna neema yoyote. Wanaonyesha hasira zao kwa kile ambacho wao wanaona ni ujinga wa viongozi au serikali zetu kukubali kiholela kuhonga nchi kwa mataifa makubwa. Kwa mujibu wa waandishi wa riwaya hizi, kukubali kudanganyika kirahisi na mambo haya, kumesababisha kuporomoka vibaya sana kwa nchi zetu katika sekta zake zote, ingawa takwimu za ukuaji wa

uchumi zinazotolewa na wakubwa, zinawekwa juu. Wamitila (2003) analirejelea kama utandawizi badala ya utandawazi kama kijiji cha *Global Villain, global pillage.* Mawazo ya Gromov na Wamitila yanashabihiana hasa katika kuzingatia mabadiliko ya jinsi masuala mazito hushughulikiwa katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Mawazo haya yaliongoza utafiti huu katika kuhakiki na kutathmini uwakilishi wa utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili.

2.5 Misingi ya Nadharia

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni Usasaleo. Nadharia hii ni ya utata hasa kueleza asili yake kiwakati na hata maana yake. Hata hivyo, sifa zake kuu ndizo zilikuwa mihimili ya utafiti huu. Walmsley (2006) anarejelea William Blake na James Joyce wanaposema kuwa Usasaleo hauwezi kurejelewa kiwakati, bali unafaa urejelewe kama njia ya kuwasilisha mawazo ya kipindi maalum katika historia. Wanasema kuwa hata kama mtu atafanya utafiti kiasi gani, hakuna maelezo faafu yanayoeleza maana kamili ya Usasaleo. Walmsley anasema kuwa kama mwanzo wa historia ya ujumi, mwanzo wa utamaduni mpya au falsafa, Usasaleo ni mfumo unaotambua msimamo au mawazo mbalimbali, ugiligili na uwazi. Walmsley anasisitiza kuwa kujaribu kueleza maana ya Usasaleo hudunisha na kudhoofisha thamani yake, misimamo yake na kazi zake. Hii ina maana kuwa Usasaleo hubadilikabadilika, si huru, na usio wa udhabiti imara. Walmsley anatamatisha kwa kusema kuwa Usasaleo ni kituo cha mtafaruku, makubaliano na mjadala.

Baadhi ya wataalam hawakubaliani kuhusu maana ya Usasaleo. Hii ni kwa sababu Usasaleo ni njia ya kufikiria; na hivyo, ni vigumu kufasili kiwakati. Wamitila anakubali kuwa aghalabu huwa ni vigumu kuweka mipaka wazi kati ya usasa na Usasaleo kutokana na kuingiliana kwa sifa zake (Wamitila, 2003). Butler (2003) anaeleza dhana ya Usasaleo kuwa ni mwisho wa usasa na maendeleo yake. Maendeleo kutoka kwa Umaksi kwa kupinga na kukanusha misingi yake kama vile kimamboleo. Aidha, ni kiini cha mapinduzi ambacho, husisitiza kuharibika au kuoza kwa masimulizi makuu na mwisho wake masimulizi makuu ni Usasaleo. Butler Anatambua kuwa Usasaleo ni makisio ya ujumi katika utamaduni kwa lengo la kuimarisha na vilevile, ni maantiki ya utamaduni wa ubepari. Isitoshe, Usasaleo ni kupotezwa kwa uhalisia; kukiuka kwa hakika za falsafa na vilevile, kiini cha uhakiki wa falsafa na uwanja wa uwasilishaji.

Walmsley (2006) anaonyesha Usasaleo kama upinzani wa usasa. Anasema, wakati ambapo Usasa husisitiza ufafanuzi; Usasaleo hukataa ufafanuzi. Mawazo haya ni sawa na ya Fiedler anayerejelewa na Walmsley, anayesema kuwa Usasaleo ni kikomo cha Usasa. Njia ambayo

Usasa unaeleza ujumi na kuipanga imetupiliwa mbali na kupanguliwa upya na usasaleo. Hassan anavyotajwa pia na Walmsley anasema kuwa Usasaleo ni kama msukumo wa kugutua madaraka, kuzua hofu kuhusu asili ya maisha na elimu ya fahamu kuhusiana na yale tunayoyafahamu.

Usasaleo hufafanua 'ukiwa' wa uhalisia katika ubunulizi mkuu ambao umeweza kuleta kielelezo cha jinsi binadamu hufikiria (Lyotard, 1979). Lyotard badala ya kujumuisha kwamba Usasaleo hauna maana au hauleti manufaa na pia, suala moja lisilopingwa, anaonyesha mtazamo mwingine wa usawa na haki za mchezo wa lugha za kienyeji. Hapa, anamaanisha mseto wa sheria zinazoongoza matumizi ya lugha fulani. Lyotard anazua tetezi kuwa, mjadala wowote lazima uwe kwa kuzingatia kielelezo na sheria za mchezo fulani.

Nguzo za nadharia zilitumika kupambanua mfumo wa utandawazi jinsi ulivyowakilishwa katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Aidha, mihimili hii ilidhihirisha mitazamo ya waandishi katika riwaya hizi mpya teule. Mihimili hii hujumuisha: uasi, kinaya, mwingiliano matini, uchanganyishi, ubunulizi mkuu, vurugu la kiwakati na matumizi ya kazi za awali kwa njia mpya.

i. **Uasi** ni mojawapo ya mihimili ya Usasaleo. Walmsley anaonyesha kuwa Usasaleo haulengi tu mwanzo mpya. Hulenga pia maana ya uasi dhidi ya kaida zilizopo au zilizokuwepo, (Walmsley, 2006). Mwandishi Becket ni mfano wa mtunzi bwege aliyevunja kaida hizi katika riwaya, tamthilia na ushairi. Walmsley anafafanua kuwa, Usasaleo hudunisha mantiki ya muumano wa kazi kama vile msuko, uhusika, matumizi ya lugha, muundo wake miongoni mwa mengine. Usasaleo huwa unaumbua au unaasi kaida ambazo zimekuwa zikizingatiwa kama sheria katika utunzi. Pia, huasi mpangilio kiwakati, uhusika unaohalalika kisaikolojia na msuko rasmi. Warren na Wellek (1986) wanabainisha kuwa katika Usasaleo pana uasi wa kauli na pia fasihi huzingatia au huiga yaliyomo maishani; hivyo huwa kuna upingaji wa baadhi ya mawazo kuhusu fasihi, mathalani, muundo wa tangu zamani wa riwaya au jukumu la msimulizi. Usasaleo huhusisha mbinu za kusimulia hadithi zikiwemo matumizi ya fantasia kama viroja na visasili au vipengele vya bunilizi pendwa kama zile za sayansi. Kupitia mhimili huu, utafiti huu uliweza kutathmini jinsi kutofuata sheria za utunzi ulijenga maudhui ya utandawazi. Hii ilifaidi utafiti huu katika kuhakiki maudhui ya waandishi wa Riwaya Mpya. Aidha, kupitia mbinu zilizotumika, uasi ulidhihirika na kusaidia utafiti huu kutathmini mitazamo ya waandishi katika Riwaya Mpya.

ii. **Kinaya, masihara na ucheshi** ni mhimili mwingine wa Usasaleo**.** Hutcheon (1989) ana mtazamo kuwa Usasaleo umevamiwa na mazingaombwe ambayo hutambulika na matini ya kinaya ambayo huwasilishwa kwa utani. Japo hazikuanza na Usasaleo, zimetumika sana katika vuguvugu hili. Hutcheon anasisitiza kuwa mbinu hii ya Usasaleo huangazia masuala mazito kwa njia ya mchezo. Mhimili huu ulisaidia utafiti huu kutathmini masuala yanayoelezwa kwa njia ya kinaya au ucheshi. Sababu ya masuala hayo kuelezwa kwa njia hiyo ilisadia kutathmini mitazamo ya waandishi. Ilibainika kuwa waandishi hawa wametumia mbinu ya kinaya, masihara na ucheshi kusawiri suala la utandawazi.

iii. Kwa upande mwingine, **Mwingiliano matini** umekuwa nguzo muhimu katika nadharia hii ya Usasaleo. Wamitila (2003) anarejelea mwingiliano matini kama dhana inayotumiwa kueleza kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya kifasihi. Barthelme (1983) anarejelea mwingiliano matini katika Usasaleo kama hekaya au hadithi ambazo zinahusiana na kazi iliyoandikwa kwa namna moja au nyingine. Tylor (2004) anaonyesha kuwa Usasaleo huhusisha wingi matini pale kazi ya fasihi imehusisha masuala mbalimbali kama vile kifalsafa, kilimo na uchawi. Aidha, pale mkondo wa wazo la kazi fulani ya kifasihi unategemea pia mawazo ya nje yanayofungamana na kazi yenyewe kama vile historia au ngano fulani. Tylor vilevile, anaeleza kuwa wingi matini hurejelea matini za awali na kuzirekebisha ili shauri la mwandishi libaki pekee. Hivyo, katika Usasaleo, hakuna kazi huru. Wamitila (2003) anatoa mfano jinsi ya kushughulikia mwingiliano matini katika Usasaleo kwa unukuzi au kudondoa, wizi wa uandishi na wigobezi. Anaonyesha kuwa wafuasi wa mbinu hii wanashikilia kuwa kazi za fasihi huingiliana na kuhusiana katika kile kinachoitwa ‘mwanda wa kimwingiliano matini. Mhimili huu ulisaidia utafiti huu kutathmini maudhui ya utandawazi yanayoingiliana, uhusika katika Riwaya Mpya na jinsi mawazo ya waandishi wa Riwaya Mpya yanavyohusiana katika kueleza dhana ya utandawazi. Aidha, utafiti huu ulilinganisha matini mbalimbali katika Riwaya Mpya kwa ajili ya kupata uwakilisho wa utandawazi.

iv. **Ubunulizi Mkuu** ni mhimili muhimu katika nadharia hii. Hutcheon (1989) anarejelea mbinu hii kama ambayo hutia mazingaombwe katika historia halisi ya tukio au nambari. Usasaleo huhusu uandishi (Cooper, 2003). Hii huhusu kufanya ugushi wa fasihi au ugushi wa bunulizi uonekane kwa msomi. Ubunilizi unawekwa wazi kwa msomaji badala ya kufichwa ili uonekane kama ukweli. Kawaida, hutumika kudunisha nguvu za mwandishi kwa kusudi la kueleza hadithi kwa njia ya kipekee au kama tahariri kuhusu shughuli ya kuandika au kusimulia. Yaliyomo kwenye mbinu hii yaliongoza mtafiti kutambua mitazamo ya waandishi kuhusu utandawazi.

v. Pia, **Vurugu la kiwakati** hudhihirika katika nadharia ya Usasaleo. Japo mbinu hii hutumika katika kazi za usasa, imekita katika Usasaleo pia. Wamitila (2003) anaeleza kuwa mbinu hii hutumika katika Usasaleo kwa ajili ya kujenga kinaya. Mathalani kufanya ubunilizi wa visa halisi vya kihistoria. Pia, nyakati huweza kubadilika, zikarudiana na kutengana na kuwa na uwezekano kadhaa. Kadhalika mtunzi anaweza kusawiri visa kadha wa kadha vyote vikijiri wakati mmoja. Katika kueleza masuala mazito, vurugu la kiwakati lilisaidia utafiti huu kutambua masuala tofauti tofauti ya kihistoria. Aidha, mhimili huu ulikuwa muhimu katika kutathmini mitazamo ya waandishi kuhusu uwasilisho wa utandawazi.

Kwa jumla, nadharia ya Usasaleo ilisaidia utafiti huu kutambua usuli wa falsafa, msuko wa matukio, uendelezaji wa wahusika pamoja na matumizi ya lugha ilivyovunjwavunjwa na kusheheni taswira na ishara. Nadharia hii ilisaidia utafiti huu kutambua nostajia na prognosia yaani ndoto ya maisha yaliyopita na ndoto za wakati ujao katika kujenga wazo kuu. Hili lilitambulika katika wahusika mviringo na wale wenye ufahamu wa nguvu au kanuni zinazodhibiti mahusiano ya jamii. Nadharia hii ilisaidia utafiti huu kusaili masaibu yaliyopoteza mwelekeo katika kustaarabisha jamii. Pia, ilibainisha lilipotatizo kwa kurejelea mtu wa kawaida wa mtaani katika shughuli zao za kila siku. Haya, yalifanikishwa kwa kuhakiki maudhui ya utandawazi, kutathmini mbinu zilizotumia kuwasilisha utandawazi na kisha kutathmini mitazamo ya waandishi wa riwaya hii kuhusu suala zima la utandawazi.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea kwa jumla kuhusu mbinu mbalimbali zilizotumika katika utafiti huu. Mbinu hizi zilijumuisha ukusanyaji deta: uteuzi wa sampuli, mahali pa utafiti na uchanganuzi wa deta hizo. Utafiti ulikuwa wa kimaktaba. Kwa hivyo, ulikuwa wa kimaelezo na wa kiuthamano. Aidha, ulitumia ufafanuzi na maelezo ili kufanikisha uchanganuzi. Utafiti ulihusu kuzuru maktaba mbalimbali ili kupata deta iliyofanikisha uchunguzi. Katika ukusanyaji wa deta, maktaba na mtandao ulikuwa muhimu. Deta ilisomwa na kuchanganuliwa.

3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuhakiki maudhui yanayoingiliana na utandawazi, kuchunguza mbinu zilizotumika kujenga maudhui na kutathmini mitazamo ya waandishi kuhusu suala la utandawazi katika Riwaya Mpya. Waliolengwa katika utafiti huu ni wanafunzi wa shule za upili na vyuo vikuu, walimu wa fasihi, watafiti katika fasihi kwa jumla pia Taasisi ya elimu inayojihusisha na kupendekeza vitabu vya fasihi vinavyotumika katika viwango mbalimbali vya elimu.

Utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo uliohitaji kusoma riwaya teule kisha kuhakiki, kuchunguza na pia kutathmini mintarafu ya madhumuni. Deta zilikusanywa kwa usaidizi wa nadharia ya usasaleo na kuongozwa na madhumuni ya utafiti. Katika ukusanyaji deta, changamoto ya kufasiri vipengele vya nadharia vikiwemo; uhalisiajabu, mwingiliano matini, uchanganyishi, uasi. Usaidizi wa waelekezi ulikuwa muhimu katika kutatua changamoto.

3.3 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani hasa maktaba za vyuo vikuu na Umma pamoja na mtandao. Hii ni kwa sababu riwaya huhitaji kusomwa kwa makini na kisha kupambanuliwa. Mahali hapa palichaguliwa kutokana na kuwepo kwa matini yaliyohusiana na masuala ya Riwaya Mpya na uwakilisho wa utandawazi, kama ilivyodhihirika katika mapitio ya maandishi. Pia, mtandao ulikuwa muhimu kama sehemu ya kupata matini yaliyohitajika kufanikisha utafiti huu. Kutokana na deta iliyopatikana kutoka kwa maktaba na mtandao, deta iliyohitajika kufanikisha uchunguzi ilikidhiwa.

3.4 Ukusanyaji Deta

Ukusanyaji wa data uliongozwa na nadharia ya Usasaleo. Nadharia ya Usasaleo ilisaidia kukusanya data kuhusiana na uhakiki wa maudhui ya utandawazi, mbinu zilizotumiwa kuwakilisha utandawazi na pia mitazamo ya waandishi kuhusu suala la utandawazi. Mihimili kama vile: uasi, mwingiliano-matini, vurugo la wakati, uandishi ndani ya uandishi pamoja na kinaya zilizingatiwa. Haya ni masuala muhimu sana na hayawezi kuepukika katika kudondoa data katika kazi yoyote inayohusiana na enzi ya Usasaleo. Nadharia hii ina mihimili na vipengele vingi vikiwemo vitano vilivyochaguliwa kuongoza ukusanyaji wa data uliofanikisha uchunguzi huu.

Ukusanyaji wa deta uliongozwa na madhumuni ya utafiti huu ya kuhakiki maudhui ya utandawazi, kutathmini mbinu zilizotumika kuwasilisha utandawazi na pia kutathmini mitazamo ya waandishi wa Riwaya Mpya kuhusu suala la utandawazi. Ukusanyaji huu ulihusu mambo matatu: mahali ambapo palikuwa ni maktaba za vyuo vikuu na mtandao, mbinu za utafiti ambazo zilijumuisha kusoma na kisha kuteua sampuli za kimaksudi na vyombo vya ukusanyaji wa deta:

3.5 Uteuzi wa Sampuli

Benard (2000) anafafanua mbinu ya maksudi kama inayotumiwa kuteua deta yenye sifa fulani kwa lengo la kutimiza madhumuni ya utafiti. Utafiti ulitumia mbinu hii ya kimaksudi katika kuteua sampuli ya Riwaya Mpya ya Kiswahili kwa lengo la kutimiza madhumuni ya utafiti. Utafiti huu ulitumia riwaya ya *Bina- Adamu* (Wamitila, 2002) *Musaleo!* (Wamitila, 2004) *Dunia Yao* (Mohamed, 2006) na *Babu Alipofufuka* (Mohamed, 2001). Mtafiti alichagua kazi hizi kwa sababu kwanza ni riwaya ambazo zinalingana yamkini kwa njia nyingi kama vile mtindo, uhusika, usimulizi na maudhui. Riwaya hizi hushughulikia maudhui ya utandawazi kwa njia tofauti kabisa. Pili, riwaya hizi zinaeleza maudhui mengine utandawazi, jambo ambalo hukanganya. Tatu, waandishi hawa ni watajika katika fasihi ya Kiswahili. Aidha ni baadhi ya waandishi wanaoendeleza Riwaya Mpya ya Kiswahili, hivyo mitazamo yao ilikuwa muhimu. Utafiti huu uliteua maudhui yanayoingiliana na utandawazi kisha kuchanganua kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya Usasaleo.

3.6 Uwasilishaji wa Deta

Uwasilishaji wa deta ulikuwa kwa mintarafu ya madhumuni ya utafiti huu. Deta iliainishwa kulingana na mrengo wa tathmini hasa utokanao na nadharia ya Usasaleo. Uwasilishaji huu ulijumuisha uhakiki wa ujenzi wa maudhui ya utandawazi. Uwasilishi ulizingatia mbinu,

sentensi na maneno yaliyotumika kwa kurejelea matumizi ya; kinaya, mwingiliano matini, ucheshi miongoni mwa mengine ili kutathmini mitazamo ya waandishi katika Riwaya Mpya.

Khamis (2005) ana tia shaka urazini wa utandawazi katika riwaya mpya ya Kiswahili. Kwa mujibu wa madhumuni ya kwanza; kuhakiki ujenzi wa maudhui ya utandawazi katika Riwaya Mpya, utafiti huu ulizingatia maudhui yaliyoingiliana na kukamilishana na utandawazi kwa lengo la kutathmini usawiri na urazini wa utandawazi. Kwa mfano, uongozi wakati wa wakoloni ulitambulikana kama wa mgawanyiko ambapo jamii iligawanywa katika vikundi mbalimbali na hata mipaka kubuniwa baina ya vijiji. Vilevile, kiongozi wa kila kijiji aliteuliwa na wakoloni kwa mfano, machifu. Katika kipindi hiki, jamii iligawika kwa misingi ya vigezo vya kijamii kama vile mali, elimu, dini miongoni mwa mengine.

Kupanda na kushuka kwa uchumi wa mataifa mbalimbali ni suala la kiulimwengu. Bei za bidhaa za kimsingi kubadilika, ni suala la kiulimwengu. Thamani ya sarafu kama vile dola kubadilika ni suala la kiulimwengu. Kwa mujibu wa uhakiki wa maudhui ya utandawazi, Riwaya Mpya ya Kiswahili ina majibu kwa matatizo haya ya kiuchumi. Kwa jicho la ndani, mabadiliko haya ni ya kimaksudi kwani uchumi hudhibitiwa na mataifa yenye uwezo na mamlaka yaani *super-power*. Nguvu hizi zimo kwenye Benki ya dunia na mashirika mbalimbali kama vile WTO. Vilevile, mabadiliko haya husingiziwa uongozi mbaya kwenye nchi zinazazoendelea. Mifano ya deta inayoonyesha haya katika Riwaya Mpya ni pamoja na:

> Nyie mtatambua lini kuwa mambo yamebadilika? Mishahara midogomidogo, watu hawana tena uwezo wa kununua. Hali ya kiuchumi ya mtu haina mategemeo tena, uhusiano nao unaathiriwa. Sitaki kusikia habari za mjomba, jirani ya binamu au mkaza mwana wala mpwa hapa! Hii ni awamu nyingine! **New World economy**. (Wamitila 2002: 65).

Umaskini umekuwa janga la kimataifa, hasa mataifa ya bara la Afrika. Katika Riwaya Mpya ya Kiswahili, janga hili huendelezwa na mataifa yenye nguvu na uwezo. Mataifa haya ambayo yanamiliki kampuni na mashirika mbalimbali hunyonya rasilmali na uwezo wa nchi zinazoendelea. Kwa mfano, Mohamed (2006: 29) anaeleza jinsi machimbo yaliyokuwa na madini kama vile shaba, dhahabu, fedha na ulanga, humilikiwa na kampuni za kigeni ambazo huajiri wenyeji kuyachimba lakini hawalipwi. Hili linazua umaskini katika sehemu hizo.

Uongozi mbaya barani Afrika kwa upande mwingine hukisiwa kuendeleza umaskini zaidi. Hii ni kulingana na sera za serikali husika, ufisadi, ukabila, chuki miongoni mwa mengine. Katika Riwaya Mpya, haya yanaangaziwa kwa njia ya ucheshi, kinaya, na hata kejeli. Kwa mfano, hali ya maisha ya watoto viditia hutisha hasa kutokana na mararu waliyoyavaa, hali yao ya maisha inayosheni matatizo kutokana na lishe bora. Hii inawalazimisha wagonge madirisha ya magari kuomba msaada wa hela. (Mohamed 2001: 27).

Walibora (2010) alipendekeza utafiti zaidi kuhusu mitindo hii ya riwaya mpya ili kubainisha kama hadhira ya riwaya ya Kiswahili inachangamkia riwaya mpya na kuchangamkia sanaa hii mpya. Mintarafu ya madhumuni ya pili: kuchunguza mbinu zilizotumika kuangaza utandawazi, uwasilishaji wa deta uliangazia jinsi mitindo hii: mwingiliano matini, kinaya, vurugu la kiwakati, ucheshi, uhalisia-ajabu miongoni mwa mengine zinavyotumika kuwasilisha suala la utandawazi. Mbinu hizi ndizo hutofautisha Riwaya Mpya na riwaya tangulizi, hivyo, jinsi zinavyotumika kujenga utandawazi ni muhimu katika utafiti huu. Kwa mfano, katika matumizi ya uhalisia-ajabu waandishi wamebuni ulimwengu mbadala kwa lengo la kukosoa masuala ambayo uhalisia wa kijamii hutegemea ili kuwepo. Haya, hujumuisha kintotolojia, kisiasa, kijiogorafia au kiutanzu. Katika riwaya hizi, wahusika wengi ni roho tu au mizuka. Wanaongozwa na sauti, mwangaza au wanyama fulani katika safari zao. Vilevile, mambo mengi hufanyika katika ndoto tu. Mfano, Wamitila (2004: 48) anaeleza nafuu wa kutofuata ndege bali binadamu wenzake.

Vurugu la kiwakati limetumika katika Riwaya Mpya kwa lengo la kujenga kinaya. Nyakati hurudiana, hubadilika na hata kutengana. Katika uchanganuzi wa deta, mbinu hii hutoa mtazamo wa mwandishi na hata kujenga taswira ya jambo husika linalorejewa. Kwa mfano,

> ...Aaa-nilipotazama tena Magharibi ya Kaskazini, na tena Kusini na Mashariki, nilisema kimoyomoyo: mwanya wa milioni ya miaka unayatenga makundi haya mawili. (Mohamed 2006: 212).

Mahojiano mafupi na Lutz Diegner juu ya nafasi ya riwaya ya *Bina-Adamu!* ilibabaisha hasa mwandishi mwenyewe (Wamitila) aliposema kuwa hana uhakika na nafasi yake na hivyo wahakiki ndio wanao jibu. Uwasilishaji wa deta ulitathmini mitazamo ya waandishi wa Riwaya Mpya kuhusu utandawazi. Uchanganuzi huu ulijiegeza katika madhumuni ya kwanza na madhumuni ya pili; kwa kutathmini jinsi waandishi walivyojenga maudhui ya utandawazi na mtindo uliotumiwa kusawiri maudhui ya utandawazi. Ujenzi wa maudhui ya utandawazi na

mbinu zilizotumika zitadhihirisha mitazamo mbalimbali kama vile chuki, dharau, mapenzi, uchochezi miongoni mwa mengine. Kwa mfano, matumizi ya kinaya katika kuonyesha kukosa maendeleo (uongozi mbaya) hata baada ya uhuru. Hili linaonyesha hisia ya kejeli kwa uongozi (Mohamed 2001: 96). Pia, kuna matumizi ya ucheshi kuonyesha madhara ya ukengeushi: jinsi utamaduni wa kigeni huathiri watu:

> Tazama...wanavalia masuti na kubeba mikoba ambayo ina gazeti la mwaka jana! Uzungu umewavaa watu... (Wamitila 2004: 29).

Mtazamo wa majuto kuhusu ubepari:

> ...si nyinyi mlioleta ufukara na balaa hapa petu! Kweli palikuwa na taabu, lakini si kama hii. (Mohamed 2006: 52).

Mtazamo wa majuto kuonyesha jinsi sheria na haki zinazolinda watu ni za kindoto:

> Mweleze (P.P) tunafurahia haki zetu na kwamba tunaishi katika ndoto. (Wamitila 2002: 120).

Sehemu hii ya mbinu za utafiti imeweza kushughulikia ukusanyaji wa deta na uchanganuzi wake. Katika ukusanyaji, imetambulika kuwa utafiti huu ulikuwa wa maktaba na hivyo maktaba ya vyuo mbali mbalimbali zilitumika. Aidha, deta ziliteuliwa kwa njia ya kimaksudi ambapo Riwaya Mpya zinazoingiliana ziliteuliwa na kisha kusomwa na kuchanganuliwa. Haya yaliongozwa na madhumuni ya utafiti. Uchanganuzi wa deta ulijumuisha kuteua maudhui yaliyo na uhusiano na utandawazi. Maudhui haya yalihakikiwa kuonyesha uwasilisho wa utandawazi katika Riwaya Mpya. Mbinu zilizotumika zilitathminiwa na kisha kufasiri yaliyomo kwenye mbinu hizo. Hivyo, mifano michache ikaonyeshwa kuthibitisha uwasilisho wa utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili.

SURA YA NNE
UCHANGANUZI WA DETA

4.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti aliweza kudondoa deta iliyofanikisha utafiti huu kwa kuhakiki maudhui mbalimbali katika Riwaya Mpya ya Kiswahili: *Dunia Yao*, *Babu Alipofufuka*, *Musaleo!* na *Bina-Adamu!*. Deta ilichanganuliwa kwa usaidizi wa vipengele vya nadharia ya Usasaleo vikiwemo: uasi, uhalisia-ajabu, mwingiliano matini na vurugu la kiwakati. Matokeo yamewasilishwa kwa kuzingatia sehemu tatu: uhakiki wa maudhui yanayoingiliana na utandawazi, kutathmini mbinu zilizofanikisha uwakilishi wa utandawazi na kutathmini mitazamo ya waandishi kuhusu suala la utandawazi.

4.2 Uhakiki wa Maudhui ya Utandawazi

Uwakilishi wa utandawazi umebainika katika maudhui mbalimbali kwenye Riwaya Mpya ya Kiswahili. Maudhui haya yamejengeka katika uhasi na uchanya wa suala zima la utandawazi. Kezilahabi (1985) anaeleza kuwa mtindo wa kuwasilisha ujumbe katika Riwaya Mpya imechukua mkondo tofauti. Mkondo huu ni wa kupotosha kwa maksudi na hata kuingiza vitu visivyo vya kawaida katika riwaya. Kwa mujibu wa madhumuni ya kwanza: kuhakiki maudhui ya utandawazi, maudhui matano yaliweza kuchanganuliwa na kisha kufasiriwa kwa lengo la kutambua uhusiano wao na utandawazi. Vipengele vingi vya Usasaleo vilitumika katika kudhihirisha uhusiano wa maudhui haya na utandawazi. Maudhui haya ni pamoja na: uongozi, sayansi na teknolojia, utamaduni, umaskini na mabadiliko. Ilibainika kuwa kuna uhusiano wa maudhui haya na utandawazi kama ifuatayo:

4.2.1 Uongozi na Utandawazi

Uongozi ni madaraka anayopewa mtu kusimamia shughuli au asasi. (TUKI, 2004). Uongozi pia, ni mojawapo wa taasisi za mahusiano. Mintarafu ya Riwaya Mpya, mara nyingi kiongozi huchaguliwa na watu kupitia kura ya maamuzi (hasa za kisiasa) au kupitia mchujo uliowekwa na taasisi maalum. Aidha, uongozi una sera zinazotawala, sera ambazo hubuniwa kutokana na ruwaza au maono ya asasi au shughuli fulani. Hivyo, uongozi ni taasisi ya mahusiano na huleta utangamano baina ya watu wenye nia na tamaduni mbalimbali. Katika Riwaya Mpya ya Kiswahili, maudhui ya uongozi yameshughulikiwa kwa njia ya udenguzi ambapo masuala ya uhalisia-ajabu na uasi yametumika kuzua dhana mbalimbali.

Kwa mujibu wa Walmsley (2006) uasi hulenga kutofuata kaida za uwasilishi wa kazi za fasihi. Uasi huu ulidhihirika katika mpangilio wa kiwakati, uhusika miongoni mwa mengine. Haya yalidhihirika katika suala la uongozi katika Riwaya Mpya. Uongozi umegawika katika sehemu tatu: uongozi kabla ya wakoloni, uongozi wakati wa wakoloni na uongozi baada ya wakoloni. Mhakiki amelinganisha na kulinganua uongozi katika vipindi hivi vitatu, na jinsi vinavyoingiliana na kuathiriwa na utandawazi. Kwa mfano, uongozi kabla ya wakoloni ulikuwa na utu, ujamaa na mapenzi baina ya wanajamii. Kiongozi alichaguliwa kwa msingi wa utendakazi na uwajibikaji wake kwa wanajamii. Katika kipindi hiki kulikuwa na amani na ushirikiano, (Mohamed 2006).

Uongozi wakati wa wakoloni ulitambulika kama wa mgawanyiko ambapo jamii iligawika katika vikundi mbalimbali na hata mipaka kubuniwa baina ya vijiji. Kiongozi wa kila kijiji aliteuliwa na wakoloni. Aliyechaguliwa, lazima alikuwa kibaraka wao, kwa mfano, machifu. Katika kipindi hiki jamii iligawika kwa misingi ya vigezo vya kijamii kama vile mali, elimu, dini, jinsia miongoni mwa mengine. Wakoloni walinyakua na hata kuiba ardhi na kuzimiliki. Mbegu za utandawazi ziliweza kupandwa katika kipindi hiki. Bergonzi (1972) anaeleza kuwa kipindi hiki kilikuwa cha uhalisia ambapo kazi za waandishi ziliwasilishwa kwa uwazi na mtiririko wa mantiki. Pia, ni kipindi hiki ambapo utumwa ulibuniwa. Usimulizi wa riwaya ya *Musaleo!* ulidhihirisha haya:

> Sasa tumeshaiba ardhi yao kilichobakia ni kuviiba na kuvimiliki viungo vyao. Hii ni hatua ya pili. Aliamua kuwafanya watu kadha aliowajua kwanza alipofika wakuu akawaita **Paramount Chiefs.** Huo ukawa mwanzo wa uchifu na uchafu na udufu wake! (Wamitila 2002: 27, 28)

Kipindi baada ya ukoloni ni kipindi ambacho Waafrika waliweza kumiliki ardhi zao na kuanza kujitawala. Inatambulika kama kipindi cha uhuru wa bendera. Vilevile, ni kipindi ambacho mbegu za utandawazi ziliweza kuota. Mawasiliano yakaimarika na shughuli mbalimbali za kisiasa, kidini na mwingiliano wa tamaduni mbalimbali ziliweza kushuhudiwa. Kipindi hiki kinarejelewa kama kipindi cha utandawazi ambapo ulimwengu ulikuwa kama kijiji. Kukawa na mwingiliano mkubwa baina ya mataifa mbalimbali. Isitoshe, ni kipindi ambacho viongozi wa Afrika waliendeleza sera za uongozi wa wakoloni: Ukoloni Mamboleo. Viongozi wakaiga mtindo wao wa uongozi, kujilimbikizia mali, kutumia nguvu na mamlaka kuwanyanyasa wananchi wenzao na hata kujitia uungu miongoni mwa mengine. Ni katika kipindi hiki ndipo

dunia ikawa kama kijiji kwa sababu ya teknolojia. Kwa mfano, Mohamed (2001:79) anaonyesha jinsi tabia ya viongozi ilibadilika, kukaongezeka ubinafsi, uchoyo, hali ya kutaka zaidi na zaidi na hata kuabudiwa na binadamu wengine.

Mwingiliano wa uongozi na suala la utandawazi ulidhihirika waziwazi katika mtindo wa uongozi, taasisi za uongozi, hali ya maisha ya viongozi, na jinsi taifa au kiongozi wa taifa hutangamana na mataifa au viongozi wa mataifa mengine. Riwaya Mpya ya Kiswahili inarejelea mbinu zinazotumiwa katika uongozi zikiwemo katiba ya nchi, matawi ya serikali kama vile bunge, mahakama na mamlaka ya kiongozi wa nchi. Matawi hayo ndiyo huelekeza taifa kwa kupitia kiongozi aliyechaguliwa na wananchi. Taasisi za uongozi hurejelea idara mbalimbali zinazomilikiwa na serikali kwa lengo la kuendeleza utendakazi wake. Hali ya maisha ya kiongozi katika riwaya hii inategemea uhusiano wa kiongozi na raia. Utangamano baina ya nchi unarejelea shughuli mbalimbali zinazofanywa na nchi husika kama vile biashara.

Riwaya Mpya hutambua tofauti iliyopo kati ya nchi changa zinazoendelea na nchi zilizoendelea. Tofauti hizi ni bayana katika uwezo wa kiuchumi, itikadi na mamlaka. Nchi changa zinazoenedelea kwa hakika, zinaamini kwamba kuendelea kwao kunategemea uongozi wa nchi zilizoendelea. Aidha, viongozi wa nchi hizi wanatambua kuwa hawana uwezo wa kiuchumi, itikadi zao ni hafifu na mamlaka dhaifu. Kwa upande mwingine, uongozi wa nchi zilizoendelea huchukua nafasi hiyo kuzamisha uwezo wao wa kiuchumi, itikadi na nguvu zao zilizoimarika kutawala nchi hizi changa. Mwingiliano wa nchi zilizoendelea na nchi changa zinazoendelea ndio chanzo cha uhasi au uchanya wa suala zima la utandawazi. Kwa mfano, uongozi wa nchi zilizoendelea hutambulika kwa majina ya viongozi au taasisi zao. Wamitila (2002: 14) hurejelea *UMERO-JAPA* kama mfano wa utawala wenye uwezo na itikadi imara. Pia, viongozi kama Churchil, ukoo wa Kaiser, ukoo wa Gulle, kina Franco, P.P ndio wenye mtandao wa uongozi unaodhibiti utawala. Hili, limezua masuala mengi mazito yanayoumiza wananchi katika nchi zinazoendelea. Kwa mfano:

4.2.1.1 Kutawaliwa

Mtandao wa uongozi umefanya viongozi katika nchi zinazoendelea kukosa kujitawala. Riwaya Mpya ya Kiswahili hudhihirisha mahusiano baina ya uongozi wa nchi zilizoendelea hutawala nchi zinazoendelea. Kwa hakika, hata baada ya uhuru wa bendera kupatikana, mataifa haya bado yanaendelea kutawala. Kwa uwezo wa kiuchumi na itikadi zao, wameweza kudhibiti sera za uongozi wa nchi changa. Hii ni kwa nia ya ‘kuwaendeleza’. Haya yameelezwa kwa njia ya

Udenguzi na kwa misingi ya Usasaleo. Kwa mfano kipengele cha uhalisia-ajabu kimetumika kudhihirisha jinsi wananchi wanatawaliwa. Walibora (2010) anafafanua maoni ya D'Haen (2005) kipengele hiki hurejelea mambo kwa uziada uliopindukia. Kezilahabi (1999) anaonyesha kuwa lengo la mtindo huu ni kuchanganua matatizo ya jamii (kwa muktadha huu ni uongozi) kwa jicho la ndani. Mawazo haya yanasadifu uongozi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Kwa mfano, utawala kupitia uongozi umeweza kuwapeleka vijana na wazee kwenye mafunzo maalum ya kuweza sio tu kutambua mienendo inayoishia kuwa ya kiuasi bali pia kuweza kuwaharibu akili walioenda kombo. Ukolongewe, mhusika katika riwaya ya *Musaleo!*, aliweza kubadilisha misamiati mbalimbali kwa lengo la kuwatawala Waafrika. Kwa mfano, neno 'uhuru' likawa '*kufuru',* neno 'uzalendo' likawa *'uvundo'.* Utawala wake vilevile, unadhihirika pale Mzee anaposifiwa kwa kutajwa kwa majina tofautitofauti kama; Mzee Mleta usomi, Mzee Mleta Mvua, bila yeye nchi haipo. Aidha, waliopigania uhuru waliahidiwa vinono kwa kuleta ukombozi kwa mfano, wangepewa mashamba, nishani na kujengewa minara katika Uwanja wa Uhuru na majina yao kuingizwa katika orodha ya waandika historia. Ajabu ni kwamba bado wanasubiri:

> Mzee, hawa ni wakongwe waliofanyia nchi hii kazi kubwa! Ni wapiganaji wa uhuru; unaweza kuwaita **War veterans.** Waliahidiwa mengi kama mashamba, nishani pamoja na kujengewa minara katika Uwanja wa Uhuru na majina yao kingizwa katika orodha ya waandika historia lakini bado wanasubiri. (Wamitila 2004: 14).

Pia, furaha na huzuni za kila mtu katika nchi zinazoendelea viko mikononi mwa viongozi wa nchi zilizoendelea. Mahusiano haya yameweza kuwafanya watu watumwa katika nchi zao. Hawana uhuru wa kujiamulia, kujieleza na hata kujiendeleza. Ni dhahiri shairi kuwa mitaji inayoweza kuingia na kutoka imo mikononi mwao. Kinachostajabisha ni kwamba, wanatumia viongozi wa nchi hizo. Maisha ya watu yamo mikononi mwao. Mohamed (2001: 163) anaonyesha jinsi utawala wenye uwezo wa kiuchumi na itikadi imara huwakilishwa na PRO-TEUS ambaye anaaminika kuwa na nguvu kama za ki-Ungu. Hivyo, maisha ya kila mtu yamo mikononi mwake. Utawala huo unadhibiti mwanzo na mwisho wa watu wote:

> Mimi ndiye ninayemiliki maisha yako. Nina uwezo wa kuchezea ninavyotaka bila hofu ya kudadisiwa na ye yote. Hii ni zamu yangu! Ndiwe chanzo cha dhiki wewe! Hapana! Umekosea. Mimi ndiye chanzo cha furaha ya kijiji. Vyakula vyote, ujuzi wote, elimu yote, tuseme raha zote na ndoto pia! (Wamitila 2002: 63).

Aidha, utawala huo unaonyesha kuwa yeye ndiye anayemiliki maisha ya kila mtu na kwamba ana uwezo kucheza anavyotaka bila hofu ya kudadisiwa na yeyote katika zamu yake. Utawala wa nchi zilizoendelea hutawala kila kitu katika nchi changa; vyakula vyote, ujuzi wote, elimu yote, raha zote na ndoto pia, Wamitila (2002).

4.2.1.2 Ukatili

Mwingiliano wa utawala umezaa hali ya kutokuwa na huruma; ujahili, uonevu na hata udhalimu. Haya yanadhihirika katika mahusiano au utangamano baina ya watawala na watawaliwa. Utawala wenye nguvu na uwezo hujiingiza katika sera za uongozi wa nchi zinazoendelea na kujifanya ‘wasamaria wema’. Riwaya Mpya inadhihirisha kuwa lengo lao ni kuwanyonya, kuwanyanyasa, kuwadharau na kunyakua au kuiba rasilmali za nchi hizi changa. Hii hufanywa kwa kupitia mashirika mbalimbali yaliyofadhiliwa na utawala wao. Kupitia mashirika haya, sheria za kulinda haki za utawala wao na mali zao hubuniwa. Kinaya ni kuwa viongozi wa nchi changa huweka sahihi baada ya kujifaidi wao wenyewe. Kwa mfano, machimbo ya madini katika nchi zinazoendelea humilikiwa na mataifa yenye uwezo. Bahari na mito yenye rasilmali hugeuzwa na kuwa rasilmali ya kimataifa. Hili linasababisha ukosefu wa rasilmali muhimu ambazo ni vitega uchumi katika nchi hizi changa na kusababisha umaskini mkubwa. Kwa mfano,

> Hawana samaki huko? Wanao lakini idhini ya kuwavua, sisi tunayo. Wanapatikana kwenye maji ya kimataifa, *international waters.* Tunawavua na kuwapakia kwenye makopo huko huko majini. Wanawapenda sana hawa wa makopo. Kwao ndiyo maendeleo hayo! Wakiyagomea nasi misaada ya kiuchumi kwao tunaizuia! (Wamitila 2002: 50).

Wanaotembelea nchi hizi changa hunyakua ardhi na kuwaacha wenyeji bila makao. Wanaendeleza ardhi hizi kwa zaraa na mapato kusafirisha kwao. Wenyeji wanazidi kuteseka kwa hali na mali. Aidha, kwa kushirikiana na viongozi wa nchi hizi changa, wanatumia nguvu za wananchi hawa kujinufaisha wao wenyewe. Kwa mfano, Mohamed (2001) anatambua jinsi wahusika hawa wa kigeni wanadhihirisha haya, kama vile Delpiero: ambaye anaelezwa kuwa alimeza eneo zima la ardhi pahala fulani tumboni, wavuvi wakamwona akitokomea pahali fulani na kisha kudondosha magunia yaliyojaa unga. Kwa upande mwingine, Miyazawa anahonga maafisa kwa kuwapa magari ili kufanya biashara yake ya haramu, alimpa gari kila ofisa mkubwa wa forodha bure. Pia, magari aliyokuja nayo yalikuwa kuukuu. Akayatumia kuyaotesha uwanda wa Mzogazoga na kuziuza kwa bei kubwa- ingawa kwao takataka. Mhusika mwingine ni Von Heim ambaye ana kazi zingine lakini za siri, hazijulikani na mtu yeyote. Di Livio pia ni mhusika anayecheza kamari, ananajisi wasichana, anaendeleza ushoga na kufanyisha wasichana mapenzi na mbwa, (Mohamed 2001: 13-14). Mawazo haya ni sawa na yale ya riwaya ya *Dunia Yao*:

> ... kwa jumla wanaendesha maisha ya kila mtu: sehemu ya viwiliwili na akili zao. Kwa ufupi wao kila kitu. Wengine ni mapipa matupu. Hawana rojo la uhai. Hawana supu ya maisha. Wala nyama ya ubinadamu. Hawana sehemu ya utu. Hawana rai. Hawana maoni. Hawana chao. Hawawezi kufikiri kama wao au zaidi ya wao. Hawatarajiwi kusema. Hawatarajiwi kushiriki hata mambo yanayohusu nafsi zao. (Mohamed 2006: 43).

Ukatili unadhihirika katika utendakazi wa mataifa haya yenye uwezo. Mohamed (2006) anaonyesha jinsi mtandao wa uongozi huwanyima wakazi wa nchi zinazoendelea usingizi. Kila kitu kimekuwa chao, wakawa ghala la maarifa, wanasema na kutenda watakavyo bila kupingwa. Wanajamii wamekosa haki za kibinadamu.

4.2.1.3 Biashara

Utawala wa nchi zilizoendelea hujishughulisha na biashara za bidhaa gushi katika nchi zinazoendelea. Kwa njia ya kinaya, Riwaya Mpya imekashifu biashara hii ambayo inafaidi wachache. Hutcheon (1999) anarejelea mbinu ya kinaya kama inayowasilisha masuala mazito katika jamii kwa njia ya utani au kwa njia ya ucheshi. Kwa mfano, mabovu yaliyoharibika yanatupwa kwa bei ghali katika nchi zinazoendelea. Nchi hizi zikawa kama biwi la takataka kwa

vyombo au vitu visivyohitajika tena katika nchi zao. Isitoshe, uhuru wa kufanya biashara umewekewa masharti. Kwa mfano, katika uvuaji wa samaki kwenye bahari za kimataifa, samaki huvuliwa kwa kibali kilichoidhinishwa na shirika teule la kimataifa. Hili, linaathiri uvuvi katika bahari mbalimbali hasa kwenye nchi ambazo zinaendelea. Ni bayana kuwa uvuvi ni tegemeo kubwa sana kwa taifa na wananchi wa nchi zinazoendelea. Hawana tena uwezo wa kubadilisha sheria hizi. Athari za sheria hizi hubainika katika hali ya maisha ya wanaotegemea uvuvi na vilevile vyombo wanavyovitumia kuvua.

Kuna nini hapa? Hiki ni kiwanda. Cha? Reconditioned cars. Mnazitumia? Ahh, deki masen! Haiwezekani asilan. Sheria zetu zinakataza matumizi ya maghari hayo! Basi mnayatengenezea nini? Kuna soko kubwa huko upande wa chini, huko ndiko tunakotupa tusivyovihitaji! Mnavitupa, ehh? Mmm, ni hivi tuseme, wanakubali wenyewe, karibuni tutaanza kuwauzia samaki wabichi. Yale machimbo uliyoyaona yalikuwa na madini: shaba, dhahabu, fedha na ulanga. Walihimizwa kuyachimba kwa ahadi ya kulipwa lakini mpaka leo hawana walichokiona! Waliofaidi ni waliopora madini yenyewe! (Wamitila 2002: 29, 50).

Biashara ghushi hufanya wananchi kuwa maskini zaidi. Hili ni wazi hasa wanapotazama rasilmali muhimu zinazotolewa katika nchi zao na kusafirishwa katika nchi zilizoendelea. Rasilmali hizi hutengenezwa na kuwa bora zaidi ndiposa zinarejeshwa na kuuzwa kwa bei ghali tena. Machungu zaidi ni kuwa, wageni hawa wanatumia nguvu kazi za wananchi kwa malipo duni ama bila malipo hata kidogo.

4.2.1.4 Utumwa

Utawala wa wenye uwezo kupitia mahusiano yao na viongozi wa nchi changa, wameingiza mfumo wa kijamii au hali ya kumiliki mtu kama mali na kutumiwa bila malipo yeyote. Mataifa haya, yanaendeleza utumwa hasa wanapochukua wanaume wenye nguvu kwenda kuwafanyia kazi katika nchi zao. Kwa mfano, utawala wa umero-jopa ulitambulika na utumwa. AMISTAD 1 lilikuwa jina la meli au chombo cha bahari kilichotumiwa kuwabeba watumwa kuwapeleka nchi fulani walikokwenda kuhudumu katika migunda ya mamwinyi zama za utumwa. Hii ni dhahiri katika riwaya ya *Bina-Adamu!* Riwaya ya *Musaleo!* huonyesha jinsi Wazungu waliwatia kazi waafrika katika mashamba yao baada ya kuiba mashamba yao. Hili, liliwakosesha Waafrika nafasi ya kujiendeleza kwa kuwa nguvu zao zilitumika kuwazalishia Wazungu mali. Lengo la utumwa kulingana na mabeberu lilikuwa ni kupunguza uzembe na pia uovu wa watu, (Wamitila

2004: 28). Kwa hakika, maendeleo katika jamii hizi walikotolewa watumwa hawa yalididimia kwa kukosa watu au nguvu za kuendeleza jamii. (Wamitila 2002: 28).

4.2.1.5 Kukosa utu

Utangamano baina ya mataifa mbalimbali kupitia uongozi wa nchi zinazoendelea umezorotesha ubinadamu uliokuwa ukithaminiwa katika nchi zinazoendelea. Utawala wao ndio huendeleza ushoga, ubasha, wizi wa kimabavu, umalaya, masuala ya ngono na wanyama kama vile mbwa, miongoni mwa mengine katika nchi zinazoendelea. Masuala ambayo huigwa bila kutafakariwa na wananchi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* marafiki zake K wanaendeleza ushoga, wizi, ufisadi miongono mwa mengine. Kwa mfano, mhusika Delpiero: anaelezwa kulimeza eneo zima la ardhi pahala fulani tumboni, wavuvi wakamwona akitokomea pahali fulani na kisha kudondosha magunia yaliyojaa unga. Kwa upande mwingine, Miyazawa alihonga maafisa kwa kuwapa magari ili kufanya biashara yake ya haramu, alishampa gari kila ofisa mkubwa wa forodha bure. Aidha, magari aliyokuja nayo yalikuwa kuukuu. Akayatumia kuyaotesha uwanda wa Mzogazoga na kuziuza kwa bei kubwa- ingawa kwao takataka. Mhusika mwingine ni Von Heim ambaye ana kazi zingine lakini za siri, hazijulikani na mtu yeyote. Di Livio pia ni mhusika anayecheza kamari, ananajisi wasichana, anaendeleza ushoga na kufanyisha wasichana mapenzi na mbwa, (Mohamed 2001: 13-14).

Kwa upande mwingine, mtindo wa uongozi katika nchi zinazoendelea hudhihirisha sura mbalimbali ya utandawazi. Sura hizi za utandawazi zinadhihirika katika mbinu wanazozitumia katika uongozi wao, sera za uongozi, taasisi mbalimbali na sheria za nchi hizi. Viongozi katika nchi hizi huchaguliwa na wananchi kwa njia ya kupiga kura. Wananchi huchagua viongozi wao kulingana na uwezo wa ushawishi hasa kwa ahadi wanazotoa viongozi hao wakati wa kampeni. Riwaya Mpya huonyesha taswira ya unafiki hasa wakati wa kampeni ambapo viongozi wanajifanya malaika watafutapo kura.

> Mtakula ma-apple kama mlivyokuwa mkila zamani...Watu wote watakuwa na vimo kadiri moja ... Hakutakuwa na hali ya mmoja miongoni mwenu kumwonea mwengine ... mtafanya kazi nyote na mtafaidi nguvu zenu nyote ... Msione dhiki iliyopo hapa tu, dunia yote ina dhiki hivihivi tu... (Mohamed 2001: 148).

Wanatumia mbinu mbalimbali katika kutafuta uungwaji mkono. Kwa mfano, wengine huwapa hongo wapiga kura. Lengo lao kuu ni kuweza kuwa na uwezo na nguvu kwa watu wao jinsi walivyofanya au wanavyofanya mabeberu. Wanaiga mtindo wa utawala katika mataifa yaliyo na uwezo. Pindi wanapopata uongozi, wanageuka mashetani. Hapo ndipo inadhihirika kuwa ahadi zao ni ghushi.

4.2.1.6 Ubinafsi wa viongozi

Baada ya kuchaguliwa na wananchi, viongozi wanaanza kujitafutia nguvu, ulwa na utambulisho. Wanajiingiza kwenye mtandao wa biashara na mataifa matajiri kwa lengo la kujinufaisha wao wenyewe. Tete za ubinafsi hukua na zikishakua, huota na kuvunja kuta za matamanio ya kawaida. Ubinafsi wao umezidishwa na mashindano ya nani tajiri kushinda mwingine. Sayansi na Teknolojia ambazo nazo zimekuza utashi wa pesa zimewezesha mashindano haya kunoga. Hili linadhihirika katika Riwaya Mpya ya Kiswahili haswa wanapowaalika na hata kuwapa kazi na makazi mabeberu hao. Mtandao wa ushirikiano baina yao hukuza ubinafsi wao na kudhulumu maendeleo ya nchi husika, (Wamitila 2002: 73). Wanajivinjari katika mahoteli makubwa makubwa na mabeberu hao bila kujali hatima ya nchi na wananchi wanaoongoza. Ushirikiano wao na mataifa yenye nguvu huzua ari ya ubinafsi. Kila mwamba ngoma huvutia kwake. Hili, linaleta mashindano ya utajiri baina ya viongozi. Viongozi walioshindwa kupata utajiri wanatumia mbinu zozote hata kama ni ya kuua wenzao, (Mohamed 2001: 67). Kila kiongozi anajizatiti kumiliki rasilmali na kujilimbikizia mali bila kujali mbinu za kupata mali hizo. Kiu ya mali imewafanya viongozi hawa kujiingiza katika ufisadi kwa lengo la kujitajirisha bila jasho.

Rasilmali za nchi zinatumiwa na viongozi hawa bila kujali raia, wanatumia vitisho kwa wapinzani wao ili kuleta uoga mkubwa baina ya wananchi. Hii husababisha uongozi wao kuonekana kama wa uungu. Wanasahau matatizo ya raia waliowachagua. Waliokwea juu hawataki kushuka, wanataka wabaki huko juu milele. Kila kiongozi anakaa huko juu paani, huko ndiko anakochumia matunda kwa urahisi na kuwatupia watu walioko chini ambao ndio waliomshikia ngazi ya kupanda juu.

> Imekuwa hivi kila wakati. Wote wanang'ang'ania kukwea paani. Walioshindwa wameamua kuichoma nyumba! Sasa hatuna pa kujishikiza... Tutalazimika kuanza mwanzo! Tutabakia kuchekwa milele

kutokana na upofu na viongozi! (Wamitila 2002:73). Kila mtu na lake dunia hii... (Mohamed 2001: 67).

Lakini kuna wengine ambao wanachofanya ni kula wakashiba kwanza kisha kuyatupa makaka, makokwa na maganda huko chini yanakong'ang'aniwa na umati mkubwa ulioko huko. Wengine wanaiba na kuhamishia kwingine, labda ughaibuni. Hii imekuwa mtindo wa viongozi hawa. Kando na hayo, cha kustaajabisha ni kuwa viongozi hawa wanafadhiliwa na wadhamini kutoka kwa mataifa yaliyoendelea. Watu wamegawika kikabila, kila kabila linahitaji cheo na ufanisi (Wamitila 2002: 88) ni kama kuna zawadi kwa mgawanyiko kikabila kwa baadhi ya viongozi wao. Mateso ya wanajamii hayashughulikiwi tena.

4.2.1.6 Utengano

Mfumo huo wa kuiga uongozi wa mataifa yaliyoendelea ndio husababisha matatizo mengi katika nchi zinazoendelea. Viongozi huwanyanyasa raia wakishirikiana na nguvu kutoka mataifa ya nje. Wananyang'anya wanyonge mashamba yao, kuwafanyisha kazi ngumu, raia kuwekewa masharti wanapotaka kuwaona viongozi, kukosa uhuru wa kujieleza miongoni mwa mengine. Raia wamefisidiwa nafsi zao, hawaheshimiki tena, utumwa umekithiri huku vijana wenye nguvu wakisombwa kupelekwa kufanya kazi kwenye mataifa yaliyo na uwezo, vifo vimekuwa wimbo wa nchi hizo changa. Hili ni dhahiri katika vilio vya wananchi waliochoka na mfumo wa uongozi.

Raia wamechoshwa na uongozi wa kidikteta na unyanyasaji. Wanahitaji yule ambaye anaweza kuingia katika shida zao na kuzama. Yule anayeweza kushuka daraja ya chini kabisa kukubali kuheshimu wengine. Yule ambaye anaweza kujua machungu ya watu wengi na kujitolea kunyanyua ili kunyanyuka kwake yeye mwenyewe kustahikike. Wanaamua kujikomboa baada ya kupitia mateso yanayosababishwa na uongozi wa utandawazi. Wanakashifu kutumiwa vibaya kwa nafsi zao, kuvunjwa kwa heshima zao, vijana kupotea na kungia kwenye mihadarati, vifo vinavyotokana na njaa, maradhi yanayosababishwa na ukosefu wa lishe bora, ardhi kunyakuliwa kwa nguvu miongoni mwa matatizo mengine. Ni wazi kwamba wananchi wanatambua utengano huu unaosababishwa na uongozi mbaya, wamechoshwa na wamechoka. Hawastahimili tena, (Wmitila 2002: 89, Mohamed 2001: 96). Kutokana na pengo hili kubwa baina ya utawala na wanaotawaliwa, mapinduzi yanatazamwa kuanza miongoni mwa wanajamii.

> M’MEZIFISIDI NAFSI ZETU...M’MEIVUNJA HESHIMA YETU... VIJANA WETU WANAPOTEA.. VIFO VYA NJAA NA MARADHI SABABU SI SISI... HATUNA NAFASI PANAPOSTAHIKI NAFASI ZETU.. . ARDHI INACHUKULIWA HIVIHIVI TUNAONA... KESHO YETU IMO KATIKA GIZA... TUNAANGAMIA... TUMESHAKWENDA KAPA... (Mohamed 2001: 154).

4.2.1.7 Utegemeaji wa misaada

Viongozi wa nchi hizi zinazoendelea hawana cha kujivunia. Baada kushirikiana na mabeberu kuiba na kunyakua rasilmali za nchi, wanabaki wakitegemea misaada kutoka kwa mabeberu hawa. Misaada hii ndiyo inakuwa uti wa mgongo wa nchi. Kila kitu kinakuwa msaada: vyakula, elimu, nguo, wafanyakazi, utafiti, utamaduni na kadhalika. Hii, inafanya nchi zenye uwezo kuzidi kudhibiti nchi zisizo na uwezo katika masuala kama vile kisiasa, kiuchumi, kielimu, na hata kimatibabu. Bila misaada ya mataifa haya shupavu, nchi zinazoendelea huweza kuporomoka. Hili limewapofusha wananchi, hawawezi kufikiria tena, wanangoja wafikiriwe na wanaotoa misaada.

> Walikuwa wamesimama na kuinua juu ile mikono iliyoshika vibuyu vyao wazi. Mbele la kundi hilo kulikuwa na masanamu makubwa. Moja la paka wa Kijapani anayeitwa Manekineko. La pili ni la tai la Kimarekani. Tatu ni la Gwaru kubwa ajabu la Euro, (Mohamed 2001: 130).

Ajabu ni kwamba imekuwa mirathi, kizazi ingia kizazi toka. Na kila kizazi kinaona hivyo ndivyo hasa. Matokeo yake ni kuwa: kuthubutu kumesagwasagwa, kipawa cha kufikiria kimeuliwa. Udadisi haupo, umefifilizwa. Isitoshe, watu wote wanagombania kitu kimoja: kutoa mtaji wa kuwapa wenye nguvu, nguvu zaidi kwa ridhaa zao wenyewe. Na sasa wakati rasilmali za dunia zinapokuwa zinakwisha, wao hawana nafasi katika ulimwengu. Kwa mfano, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, utegemeaji wa misaada hupiganiwa, ni kama mashindano kwa wenye nguvu.

4.2.2 Teknolojia na Sayansi

Kulingana na kamusi Tuki (2010) teknolojia hutambulika kama maarifa ya sayansi yaliyowekwa katika matumizi ya vitu kama vile zana au mitambo kwenye kiwanda, kilimo, ufundi au mawasiliano. Kwa mujibu wa Riwaya Mpya, maarifa haya ya kisayansi yamefupisha na kuondoa vikwazo vya masafa na wakati. Ni kutokana na teknolojia na sayansi ndipo mataifa mbalimbali

yameweza kushirikiana kwa lengo la kuimarisha utamaduni, biashara miongoni mwa mengine. Teknolojia imekuwa msingi wa utandawazi. Waandishi wa Riwaya Mpya wameweza kuonyesha jinsi teknolojia huathiri maisha ya binadamu kwa njia moja au nyingine. Athari zake ni bayana katika mtindo wa maisha na vilevile, mazingira wanamoishi watu. Uwakilishi wa teknolojia hudhihirika katika vipago mbalimbali katika Riwaya Mpya. Kwa mfano:

4.2.2.1 Teknolojia na utafiti

Teknolojia imefanikisha tafiti mbalimbali. Kila nchi inajizatiti isibaki nyuma katika masuala ya utafiti kwa lengo la kuvumbua vitu vipya. Vitu vipya ambavyo vinatarajiwa kuinua hali ya maisha ya binadamu. Nchi zilizoendelea zimepiga hatua sana katika utafiti. Kupiga kwao hatua hutegemea mambo mengi mintarafu ya Riwaya Mpya ya Kiswahili. Nchi zenye nguvu na uwezo wa kiuchumi zinatumia nchi zinazoendelea kama vyombo vya majaribio. Wanatumia nchi na wananchi kufanyia utafiti. Kwa mfano, katika majaribio ya dawa za kutibu, raia wa nchi changa ndio hutumiwa na Wazungu katika kufanya majaribio. Majaribio haya yanasababisha vifo vya halaiki. Wanaoteseka na kubaki na uchungu ni nchi hizi zinazoendelea. Wanaofaidika ni mataifa haya yaliyoendelea. Kwao, teknolojia imewasaidia kugundua vitu hatari na vitu vya manufaa katika maisha ya binadamu. Kwa upande mwingine, nchi zinazoendelea hupoteza wapendwa wao na kuzidi kuteseka kutokana na madhara ya majaribio haya. Kwa mfano, katika riwaya ya *Bina-Adamu!* masimulizi kuhusu mazishi ya halaiki ya watu waliokuwa ukitumiwa kama majaribio na wanasayansi yamesimuliwa. Hii ilitokana na magonjwa yaliyosababishwa na kemikali zilizokuwa zikitumika kwenye maabara, (Wamitila 2002: 124, 49).

4.2.2.2 Teknolojia na uvumbuzi wa silaha

Teknolojia imewezesha uvumbuzi wa silaha mbalimbali za vita. Waunda zana za vita hawaoni raha kukiwa na amani kwa sababu hawana soko wala njia ya kujua kama zana zao zinafaa. Hii imewafanya wawauzie wanaozitamani. Matokeo yake ni vita baina ya jamii, nchi, ndugu na ndugu na hata madhehebu mbalimbali. Uvumbuzi wa silaha hatari umesababisha uyatima, ujane na kufanya watu kuhama makazi yao kutafuta mahala pasipo vita. Umwagikaji wa damu na vifo ni mambo dhahiri katika uvumbuzi wa silaha hizi hatari.

Riwaya Mpya ya Kiswahili imeweza kuangazia mtandao huu wa silaha hatari katika mataifa yaliyo na uwezo na mataifa yasiyo uwezo. Historia ya mendeleo ya silaha ni wazi katika riwaya ya *Dunia Yao* ambapo kwanza kulichongwa rungu, kisha wakavumbua mishale, panga na mikuki. Baadaye teknolojia (utandawazi) ukavumbua magobari na bunduki katika mataifa

yaliyoendelea. Baada ya bunduki ya kawaida kukawa na bunduki mvua. Baadaye mizinga na vifaru kisha ndege za kivita. Na manowari na nyambizi, mabomu na atomiki na nyuklia. Ni wazi katika Riwaya Mpya kwamba uvumbuzi wa silaha hatari ni kiini cha vifo vya halaiki, vita, uharibifu wa rasilmali miongoni mwa mengine katika bara la Afrika. Wanaoendeleza uharibifu na vifo vya halaiki ni utawala wa mataifa yenye uwezo.

Pia, ni dhahiri kuwa silaha hizi hutumika katika kuwagonganisha watu katika nchi zao. Jamii na jamii hushambuliana, wageni haswa kutoka mataifa ya kigeni vilevile, huwagonganisha wenyeji kwa lengo la kumiliki rasilmali. Aidha, wanatumia silaha hizo kulinda ardhi au rasilmali walizozinyakua. Kwa mfano katika riwaya ya *Dunia Yao,* baada ya rasilmali kuchukuliwa na mataifa yenye nguvu, ulinzi unajengwa kulinda ardhi hizo. Vikosi vya askari na majeshi hutawala kwenye ardhi hizo. Lengo likiwa ni kuzifanyia utafiti huku wakizuia wenye ardhi kutochunguza au kutoelewa kinachovumbuliwa. Ni wazi kuwa nchi zenye rasilmali na madini ndizo hunga'ng'aniwa na mataifa haya yenye nguvu. Wanawagonganisha vichwa na kisha kuvua vita baina yao kwa lengo la kuleta 'amani' ili waonekane kama wasamaria wema.

> Ardhi inachukuliwa, ulinzi ukajengwa kulinda ardhi na vilivyomo ardhini. Vikosi vya askari na majeshi vikaundwa. *Kisha* elimu ikadhibitiwa. Sayansi na teknolojia, wakazuia wengine wasiwe na fursa nayo. *Kisha* wakapita kutangaza kuwa wengine washenzi. Wajinga hawana akili! East Timor ilionewa. Kosovo ilikandamizwa. Chechnya ina magaidi wa Kiislamu. Sierra Leone. Liberia. Congo. Rwanda. Burundi. Angola wajinga wanakubali kupiganishwa. Silaha zinatoka wapi? Almasi zinakwenda wapi? Wacha wauwane. Wakiwa hai wakifa ni mamoja kwetu. Tutatawala tutatawala tu. Wakitaka wasitake. (Mohamed 2006: 46, 47).

Uvumbuzi wa bomu kama zana za vita ni suala la teknolojia. Athari zake zimeweza kusababisha vifo vya watu na hata wengine kuathirika kiafya. Katika riwaya ya *Bina-Adamu!*, madhara ya bomu lililotupwa ni dhahiri. Bomu lilipotupwa watu wakafa wengi na wengine kuathirika. Tangu wakati huo watoto wazaliwao huwa vilema. Kuanzia siku hizo wenyeji waliamua kujiandaa na silaha zao kwa ajili ya kulipiza kisasi iwapo wangerushiwa tena. Ajabu ni kwamba, sehemu ilitupwa bomu watu walilemaa mikono na miguu. Palikuwa na watoto wengi waliokuwa na alama, alama kama walimwagiwa kitu fulani kilichowababua ngozi. Waandishi wa Riwaya

Mpya wanalaumu fujo na uvumbuzi wa silaha kama zao la mawasiliano na utashi wa kudhibiti. Hii imeweza kuweka mipaka ya raha katika maisha ya raia na kung'oa mipaka ya maafa. Kwa mfano Mohamed (2006) anadhihirisha jinsi fujo imekolea katika mipaka ya nchi mbalimbali. Ukweli ni kwamba, dunia imekuwa uwanja wa fujo kwa sababu ya usahili wa wazi wake na wepesi wa mawasiliano na utashi wa kudhibiti. Taathira ya utandawazi, mbaya kiasi kwamba hakuna tena mipaka ya maafa, lakini kuna mipaka ya raha. Yakitokea maafa pahala pamoja huenea duniani kote. Mazingira yamepotoka haswa kwa sababu ya uvumbuzi wa silaha hatari za kivita. (Mohamed 2006: 48).

4.2.2.3 Teknolojia na utumwa

Teknolojia imefanya watu kuwa watumwa kwa njia mpya. Hii ni dhahiri katika mtindo wa maisha ya vijana haswa wanapokimbilia nchi za nje kwa lengo la kujibadilisha rangi, jinsia na hata kuuza misuli zao. Aidha, utumwa ni wazi katika hali ya kutafuta mali ambapo watu hutumia mbinu nyingi hata zile za kuhatarisha maisha yao. Riwaya Mpya vilevile, hueleza jinsi raia wa nchi zinazoendelea wamewekwa watumwa na tamaduni za kigeni. Kwa upande mwingine, haya yamezua madhara chungu nzima. Watu wamekosa uhuru kwa sababu maisha yao yanatawaliwa na teknolojia mpya kupitia kwa nchi zilizo na uwezo wa kiuchumi. Watu wamekuwa watumwa katika nchi zao, wamewekewa masharti katika kila jambo wanalolifanya. Kwa mfano Mohamed (2001) anaeleza jinsi vijana wamekimbilia Uingereza na Amerika kubadilisha jinsia zao na kuuza nguvu zao katika utumwa mpya. Bahati mbaya tu hawangeweza kufanana na Wakosovo na Wabosnia kwa rangi zao, (Mohamed 2001: 146). Riwaya ya *Dunia Yao* huonyesha jinsi utumwa wa teknolojia umewazuzua wanaoufuatilia na kukosa uhuru katika mawazo na shughuli zao, wanaendeshewa maisha, viwiliwili na akili zao zimemilikiwa na utumwa. Hawatarajiwi kusema wala kushiriki katika mambo yanayohusu nafsi zao. Kwa hakika, teknolojia imefanya watu wa nchi zinazondelea kukosa maoni na pia kufikiri kama wavumbuzi au zaidi yao, (Mohamed 2006: 43).

4.2.2.4 Teknolojia na ajira

Teknolojia Pia, imeweza kuleta kazi nyingi za kimataifa na za kitaifa. Watu wameweza kuajiriwa na hata kujiajiri. Katika Riwaya Mpya ya Kiswahili, chanzo cha ubinafsi ni ajira. Watu wanajitakia makuu kwa sababu mtindo wa ajira au kazi zinazotokana na teknolojia. Watu wanatawaliwa na pesa. Kila kitu ni pesa na pesa hupatikana tu baada kufanya kazi.

> Palikuwa na watu waliojazana huko. Niliweza kuwaona Wazungu wengi na wasichana wengi wadogo ajabu. Baadhi ya Wazungu walikuwa wamevua nguo zao. Wasichana wenyewe walikuwa wamevalia viguo vilivyochupa magoti na viblauzi vilivyoachia vitumbo vyao vidogo wazi. (Wamitila 2002: 108). Kufa kwetu ndiyo nusura ya wengine. Hatupo sisi wala hatuishi mbele ya watu hawa. Mbele ya ubinafsi, sayansi, teknolojia na utashi wa pesa sisi ni ombwe tupu. Na haya ni matokeo ya kiji-Ungu kidogo ndani ya kila mtu. (Mohamed 2006: 47-48).

Hii imefanya watu katika nchi zinazoendelea kujiingiza katika kazi ambazo zinahatarisha maisha yao. Wazazi wamewaacha watoto wao kujiingiza katika kazi ambazo hawastahili kufanya kwa lengo la kujichumia. Watoto wengine wanalazimika kuacha shule na kujiingiza katika kazi za utaleleshi kama suala ambalo limezua pingamizi na hata kuleta madhara kwa watoto.

4.2.2.4 Teknolojia na biashara

Teknolojia kwa upande mwingine imefungua milango ya ununuzi na uuzajii. Watu wameweza kutangamana kwa ajili ya biashara. Hii imerahisishwa na mawasiliano. Masoko huru ya bidhaa yamefanya taifa moja likutane uso kwa uso na mataifa mengine. Japo biashara na masoko huru yana manufaa makubwa katika kubadilishana bidhaa na huduma, mataifa mengine huchukua nafasi hiyo kuuza bidhaa chapwa na bovu katika nchi changa. Riwaya Mpya imeweza kuonyesha jinsi mataifa yenye uwezo wa kiuchumi yananyanyasa mataifa changa kwa njia ya teknolojia na kujifaidi wao wenyewe. Kwa mfano,

> Haya ndiyo maendeleo, hatuwezi kuyakwepa! Ulimwengu sasa ni kijiji! Hii ndio maana ya **free market economy** na **liberation!** Tuko mbioni, nchi hii iko mbioni! Hapana haja ya kupitia hatua zote za ukuaji, tunaweza kuruka nyingine ili twende sambamba na wakati! (Wamitila 2002: 51).

Kinaya ni kwamba viongozi ndio wanaoendeleza biashara hizi. Viwanda vya serikali hubinafsishwa. Kwa viongozi hao, hayo ndiyo maendeleo na hawawezi kuyakwepa. Wanarejelea hayo kama matunda ya mitaji ya soko huru na uhuru wa biashara.

4.2.3 Utamaduni

Utamaduni hurejelewa kama mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani, TUKI (2010). Utangamano au mahusiano baina ya tamaduni mbalimbali umezaa utamaduni mpya. Utamaduni mpya huu hudhihirika kupitia mavazi, vyakula, mila, hadithi na mengine. Kwa mujibu wa Riwaya Mpya, suala kuu ni kuwa; utamaduni wa nchi zenye nguvu huathiri utamaduni wa nchi zisizo na nguvu na hivyo utamaduni wao hutawala. Utamaduni mpya unaotokana na mataifa yenye uwezo husawiriwa kama donda ndugu katika mataifa changa, haswa wanapoiga kila kitu kutoka kwa Wazungu bila kupiga msasa. Athari za kuiga kila kitu ni bayana katika Riwaya Mpya. Kwa mfano, Mohamed (2001) anadhihirisha jinsi Mzuka anashangaa kuona K anapokula Chatu wa kutokosa, nyoka wa kukaushwa, kijibwa kilichochomwa, nyama ya nyangumi aliyekaangwa na kukatwakatwa vipandevipande. Hili linamfanya Mzuka kushtuka kwani vyakula hivyo vingekuwa asili ya Kiafrika, bila shaka ingekuwa hadithi ya kima na tumbili wa Zaire.

Isitoshe, vyakula ambavyo vilijulikana kama vya kimsingi vimewekewa dawa kwa lengo la kuzidisha uzalishaji. Dawa hunyunyiziwa mimea hii na hata kuwekewa rutuba za kunawirisha afya yao. Kemikali katika mimea hii kutokana na dawa inayonyunyiziwa na rutuba imekatisha afya ya walaji. Aidha, vyakula vinavyotokana na mifugo vimekuwa tishio kwa afya ya binadamu. Utamaduni mpya unaoendeleza mbinu mbalimbali za kuimarisha uzalishaji umeweza kuzalisha kifo au magonjwa zaidi. Katika riwaya ya *Dunia Yao*, jinsi utamaduni mpya ulivyoathiri afya ya wananchi ni bayana. Miili ya watu inajazwa sumu kupitia nyama ya ng'ombe, kuku, kondoo, nafaka na mboga. Hizi zinadhihirika katika dawa za kunyunizia mimea na dawa za kuwapa mifugo, (Mohamed 2006: 49).

4.2.3.1 Kuzorota kwa tamaduni mbalimbali

Kando na vyakula kuathirika na utamaduni mpya, mwingiliano wa utamaduni umepoteza thamani ya mila na desturi ya baadhi ya jamii mbalimbali. Hili limezua masuala mengi ya kijamii yakiwemo: pengo baina ya vizazi ama umri, masuala ya jinsia na majukumu yao, masuala ya dini na kadhalika. Katika pengo la umri, vijana huwachukilia wazee kama waliopitwa na wakati kwa sababu ya kushikilia ukale. Wazee wanawatazama vijana kama

waliopotoshwa na utamaduni wa kigeni usio na utu. Kwamba wameacha mila zao na kuiga mila ya Wazungu usio wa mashiko yoyote. Haya ni Kwa mujibu wa 'Riwaya Mpya ya Kiswahili. Kwa mfano, katika riwaya ya *Musaleo!* ni wazi jinsi kumekuwa na mabadiliko kwenye mtazamo wa uhalisia wa vitu. Aidha, uhalisia umevunjika na kukosa mashiko imara katika dunia ya utandawazi. (Wamitila 2002: 41).

Athari za tamaduni mpya zimezua hali ngumu ya maisha, maisha ya kutumia nguvu au ukatili ili mtu afanikiwe. Pia, mwingiliano wa tamaduni mbalimbali umeweza kuzorotesha mila za nchi au jamii. Kwa mfano, FKK katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* ni klabu kama klabu yoyote ile ambako watu huenda kustarehe, kula, kunywa, kuogelea, kucheza disko, kujianika jua na kadhalika. Lakini katika FKK, watu wanaoingia katika klabu hiyo wote watakuwa wamevua nguo. Mila za Kiafrika kwa upande mwingine zimekosa thamani miongoni mwa wananchi wenyewe. Isitoshe, utamaduni huongozwa na utashi unaobainisha ukatili na uharibifu. Hii ndiyo maana ulimwengu umeharibika kupita kiasi, na bado hamna hata habari jinsi unavyoumia. Riwaya Mpya huonyesha bayana kuwa uzuri au ubaya wa tamaduni katika dunia hii unatokana na msingi wa utajiri na umaskini wa watu wa asili fulani. Ukiwa na uwezo unaweza kukigeuza kitu chochote kibaya kuwa kizuri na dunia nzima itakuitikia hewalla, na tena kukufuata kuhalalisha visivyohalalishika na tena kufuatwa kwa shangwe na gharama.

Riwaya Mpya hueleza jinsi kumekuwa na mabadiliko hasi kwa sababu ya utamaduni mpya, ikawa mipaka na ndoto na ukweli haipo tena. Aidha, inadhihirika kuwa, japo wanajamii hawataki tamaduni mpya, hawawezi kuizuia. Wanalazimishwa au kuhadaiwa kwa matunda yake. Kwa mfano, masuala ya ngono ambayo yalitambulika kama mambo ya faragha na siri, sasa ya wazi. Isitoshe, mavazi ya kuchekesha, wengine kutembea uchi, vileo miongoni mwa mengine, sasa yanapatikana kwa urahisi, ikawa ni vigumu kutambua mipaka ya ukweli na ndoto, (Mohamed 2006: 49, Wamitila 2002: 3).

Filamu na miziki mbalimbali zimeweza kusambazwa na kuwakengeusha watu wa nchi zinazoendelea. Hawataki tena filamu na miziki ya kwao. Inaaminika kuwa video na filamu hizi ni propaganda isiyokuwa ya moja kwa moja. Ajabu ni kwamba, wanaozitazama na kuzisikiliza wanaiga bila kuweka mpaka wa uhalisia na fantasia zilizopo kwenye filamu hizo. Riwaya ya *Bina-Adamu!,* inaonyesha jinsi mambo haya yameweza kuathiri wahusika vijana:

> ‘Hawa wanangojea kuangalia filamu za Star Wars, Rocky V na *Missing in Action*. Za huku hawatazami tena!’ Tupige durubini hivi vitu tunavyovikimbilia kutoka nje. Hizi video na filamu ni propaganda isiyokuwa ya moja kwa moja. Zinatumiwa kusambaza na kutangaza taswira maalum za utamaduni mmoja tu. Ni ubeberu huu! (Wamitila 2002: 40).

4.2.3.2 Uongozi wa tamaduni mpya

Utamaduni umeathiri uongozi wa nchi zinazoendelea. Viongozi huiga jinsi nchi zilizoendelea huongozwa na kisha kulazimisha mitindo hiyo ya uongozi katika nchi zao. Kwa hakika, hili ndilo chanzo cha baadhi ya matatizo katika nchi hizi zinazoendelea. Riwaya Mpya hutanguliza jinsi viongozi wamepoteza hisia ya kupima uwongo na ukweli. Wanangojea kusemewa na mataifa yenye uwezo. Hili linawafanya wapande mbegu ya mapuuza na kushughulikia mambo yasiyo na maana na kuacha yenye maana.

Viongozi wa nchi zinazoendelea hushirikiana na wageni kutoka nje ya nchi kuingiza utamaduni wao. K mhusika katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* anaungana na watu aliowaona kama adui kitambo: mazimwi aliwaita na hata kutangaza vita nao akisaidiwa na nyuki. Lakini leo K akiwatazama wale aliokuwa akiwaita mazimwi jana, huona kumbe sura zao zinafanana na yake. Na hilo si leo tu, kumbe tokea zamani. Wao tu akina K walikataa kuwatazama vilivyo hao waliokuwa wakiwaita mazimwi. Hii ni kwa sababu ya utamaduni wao na sasa anawaona kama watu wazuri na muhimu katika shughuli zake za kisiri. Anatumia watu hawa kudhulumu wananchi akidai kwamba wananchi wana vichwa vya kusahau. Ikawa viongozi hawa katika nchi zinazoendelea huimba wimbo sawa na wanyanyasaji wao. (Wamitila 2002: 12).

4.2.4 Umaskini

Umaskini umekuwa janga la kimataifa, hasa mataifa ya bara la Afrika. Katika Riwaya Mpya ya Kiswahili, janga hili huendelezwa na mataifa yenye nguvu na uwezo katika mchakato wa mfungamano. Mataifa haya ambayo yanamiliki makampuni na mashirika mbalimbali hunyonya rasilmali na uwezo wa nchi zinazoendelea. Uongozi mbaya umedhihirishwa kama kiini cha umaskini katika nchi zinazoendelea. Taswira ya umaskini inaonekana katika hali ya maisha ya wananchi, kwa mfano, mavazi, vyakula, makazi, kazi za watu, shughuli za eneo fulani miongoni mwa mengine. Umaskini katika Riwaya Mpya una msingi wake katika shughuli za utandawazi yakiwemo sayansi na teknolojia, uongozi wa ukoloni mamboleo, mawasiliano uliorahisishwa na

teknolojia. Kipengele cha vurugu la kiwakati kimeweza kutumika mara kwa mara kueleza jinsi umaskini unazidi kuhangaisha wananchi katika nchi zinazoendelea. Kwa mujibu wa Wamitila (2003) kipengele hiki cha Usasaleo husawiri visa kadha wa kadha vyote vikiajiri wakati mmoja. Pia, nyakati huweza kubadilikana, zikarudiana na kutengana. Kwa kupitia kipengele hiki, umedhihirika kuwa umaskini katika Riwaya Mpya ya Kiswahili umesabishwa na mambo mbalimbali. Kwa mfano:

4.2.4.1 Uongozi mbaya kama kiini cha umaskini

Uongozi wa mtaka yote, ambapo viongozi hujilimbikizia mali bila kujali maisha ya wengine ndiyo chanzo cha umaskini. Mfumo huu wa uongozi husababishwa na mashindano ya viongozi kutoka nchi mbalimbali ya kutaka kuwa na uwezo wa kiuchumi. Hii, hupelekea matajiri kuwakandamiza maskini kwa sababu ya nguvu walizonazo. Pia, wanatumia nguvu za wanyonge kujitajirisha. Jasho la wanyonge ndilo hunawirisha utajiri wao. Katika masimulizi mbalimbali, watu wanaelezea matatizo wanayoyapata siku hizi: karo ya watoto, upungufu wa chakula, magonjwa, matatizo ya kazi, hospitali kukosa dawa, wizi wa nguvu, watu kupigwa risasi na majambazi na polisi; yaani shida za kila aina. Nguvu hizi ni athari ya utandawazi. Kwa mfano, mhusika Biye katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, anahofu ya kupoteza kazi. Hana uhakika na kesho. Kazi hiyo ya nyumba aliitafuta kwa udi na uvumba. Alipohakikishiwa kazi na K, midomo ya Biye ilifunua tabasamu zaidi. Ikawa ni nafasi ya kupumzika leo na uhakika wa kubakia kazini kesho.

Uchumi umedorora kwa sababu ya uongozi mbaya unaowafanya wananchi kuhangaika, wasipate vyakula sokoni. Maisha yamekuwa magumu kiasi kwamba mwananchi wa kawaida hawezi kujimudu. Bei za bidhaa zote zimepanda isipokuwa mishahara ya wafanyakazi. Taswira hii hujidhihirisha katika Riwaya Mpya. Mohamed (2001) anajenga taswira katika Soko kuwa, watu wote walionekana wazee. Wote walisogelea chanja zilizoekewa biashara, walisimama wakitumbua macho, bila ya kuweza kununua chochote. Wengine kuvitumbulia macho vidaka vya nazi. Wengine vichungwa, vilimau, viembe na vipapai. Kwenye soko la samaki, mafungu ya dagaauronda na dagaaupapa yalikuwa yakishindana kutumbuliana macho na watu. Hakuna watu wa kununua kwa sababu ya bei ghali. Chanzo kikiwa ni uongozi unaojali maslahi na matumbo ya watu wachache. Chakula kimekuwa nadra, waliobahatika kupata wanalazimishwa kugawana. Hii ni kwa sababu waliporwa rasilmali na wageni waliokuja kama wasamaria wema.

Kinyume ni kuwa, katika nchi za Magharibi, wanyama kama mbwa huthaminiwa sana wakilinganishwa na binadamu. Chakula cha mbwa katika nchi zinazoendelea mara nyingi ni masalio ya vyakula vya binadamu. Suala la utandawazi limeathiri baadhi ya viongozi wa nchi zinazoendelea kiasi kwamba, mbwa amepewa nafasi ya ubinadamu. Wakati ambapo watu wengi wanakosa chakula, mbwa wa mhusika K katika riwaya ya *Babu Alipofufuka,* anapewa vyakula vya thamani. Babu anatafakari jinsi maisha yalivyokuwa wakati wao. Ajabu ni kuwa, wakati mbwa hupewa vyakula vya thamani, majirani wamekosa vya kimsingi, si chakula, si mavazi na hata makao wanakoita nyumbani. (Wamitila 2002: 101, Mohamed 2001: 2).

Makazi ya watu wengi maskini hutisha na hayatamaniki. Kwa upande mwingine, viongozi matajiri wanaishi kwenye majumba ya kifahari. Kwa mafano, mjengo wa kasri la mhusika K katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* ni aina ya zile za ndoto zinazoonyeshwa kwenye sinema za filamu za sayansi za kubuni. Kasri lenyewe limejaa watu wanaomhudumia: walinzi wa siri, walinzi dhahiri, makarani, wapishi, wasafishaji, waduhushibustani, waduhushi-mbwa-na- farasi; madereva, mayaya, madobi na kadhalika. Kwa upande mwingine, anaowatawala nyumba zao ni ovyoovyo kama uyoga zilizootea. Si nyumba kwa hakika. Hata si vibanda kwa maana ya vibanda. Vimejengwa kwa maboksi, majani, madebe, mabati na hata miti. Vyote ambavyo kwa umbali vinawezaitwa takataka. Ajabu ni kuwa, takataka hizi zimejengwa pembeni mwa njia sababu ikiwa ni kukosa au kufurushwa na hata labda kunyang'anywa ardhi zao.

Si majumba tu, hali ya maisha ya wanaoishi katika vibanda hivyo huashiri utepetevu wa viongozi wanaojitajirisha bila kujali raia wao. Watoto wamekosa nguo na hali yao ya maisha hutisha. Watoto viditia na vitumbo vyao, na nguo zilizowazidi vimo kufanya miili yao ya mifupa mitupu ipwae zaidi. Hii, ilifanya watoto wengine kuchokora mapipa na hata kugonga vioo vya magari na kunyoosha mikono kuomba pesa ya mahitaji yao, (Mohamed 2001: 27).

4.2.4.2 Mataifa yalioendelea kama chanzo cha umaskini

Ni wazi katika Riwaya Mpya kwamba, uchumi wa nchi hudhibitiwa na nchi zilizoendelea hasa nchi za Magharibi. Aidha, wanauwezo kuudhibiti uchumi wa dunia. Hivyo, nchi changa hazina uwezo wa kujikomboa katika mtego wa umaskini. Kila biashara au kampuni inayofunguliwa, wao ndio lazima washauriwe na kutoa kibali kulingana na matakwa yao. Hii imefanya nchi changa kutoendelea kwa kutegemea masharti na mashauri kutoka kwa nchi zenye nguvu. Wananchi wana shida, thamani ya Shilingi inafifia, dola imefutwa na ya kimataifa. Huu ndio uhalisia mpya wa mnyongemsongoe. Kwa hakika, wanamiliki maisha ya wananchi katika nchi

zinazoendelea. Wanachezea akili na mali bila hofu ya kudadisiwa na nguvu yoyote. Wanasema ni zamu yao kumiliki vya dunia. (Wamitila 2002: 63). Mfano ni katika kuvua samaki kwenye maziwa mbalimbali ambapo nchi lazima iwekewe masharti kabla ya kupewa kibali. Pasipo kibali basi utakuwa unavunja sheria za kimataifa. Kwa hakika, mambo yamebadilika. Mishahara midogomidogo, watu hawana tena uwezo wa kununua. Hii imezorotesha hali ya kiuchumi ya mtu. Athari ni kuwa, wananchi hawategemei furaha kutoka kwa serikali au uongozi wa nchi. Uhusiano uliokuwepo zamani nao haupo, unaathiriwa kwa sababu kila mtu anajitegemea. Jamaa hawataki kusikia habari za mjomba, jirani ya binamu au mkaza mwana wala mpwa. Hii ni kwa sababu ya New World economy**.** (Wamitila 2002: 65).

> Mimi ndiye ninayemiliki maisha yako. Nina uwezo wa kuchezea ninavyotaka bila hofu ya kudadisiwa na ye yote. Hii ni zamu yangu! Ndiwe chanzo cha dhiki ya kijiji wewe! Hapana! Umekosea. Mimi ndiye chanzo cha furaha ya kijiji. Vyakula vyote, ujuzi wote, elimu yote, tuseme raha zote hata na ndoto pia! (Wamitila 2002: 63).

Katika vyombo vya kupima, mataifa yenye uwezo yanasema kuwa kuna kitu kama mizani hivi ya kupimia vitu. Mizani hiyo imeundwa kiajabu. Upande mmoja kuna uzito fulani wa dollar. Fedha nyingine zinawekwa katika sehemu nyingine. Kazi za mataifa haya ni kuangalia uzani unavyoelekea na kudhibiti. Yakiona unainukia upande usio wa dollar wanawaarifu wakuu wake wa kazi. Kulingana na mataifa haya, lazima uchumi usawazishwe. Hii ni kwa sababu kuongeza kwa uzito kuna matokeo mengi sio tu ya kiuchumi, ya kisiasa na kijamii, vilevile, huathiri uongozi. Hiki ndicho chanzo cha kitendawili kinachoshinda mataifa maskini kutegua. Ajabu ni kwamba, mataifa maskini yanazidi kuwa maskini na mataifa matajiri yanazidi kuwa matajiri hata zaidi. (Wamitila 2002: 142).

4.2.5 Utandawazi Kuleta Mabadiliko

Mabadiliko huashiria hali iliyopo baada ya mageuzo. TUKI (2004). Kwa mujibu wa Riwaya Mpya, utandawazi umeweza kuleta mabadiliko chungu nzima. Mabadiliko haya yamechukua mkondo tofauti; hasi na chanya. Mabadiliko haya yameweza kuangaziwa kupitia mbinu mbalimbali ikiwemo fantasia, ucheshi, masihara na uhalisia-ajabu. Scholes na Kellogg (2006) wanakubaliana kuwa utanzu wa Riwaya Mpya ya Kiswahili ni mchanganyiko wa ubunifu na sayansi. Kwa kutumia mbinu ya fantasia, mabadiliko yametazamiwa katika uhusika,

mwingiliano wa wahusika, mwanya wa kisaikolojia katika vichwa vya wahusika na ndoto zinazoingiliana na ukweli wa mambo. Kimsingi, mabadiliko haya yanatokana na: uongozi wa nchi au mataifa yenye uwezo, uongozi wa nchi zinazoendelea, sayansi na teknolojia na utamaduni mpya. Pia, mabadiliko haya yanatokana na utangamano wa kimataifa ya binadamu na taasisi mbalimbali unaorahisishwa na teknolojia ya mawasiliano. Kwa mfano, kuna mabadiliko kama vile: katika mazingira, miundo msingi, tabia za viongozi, ongezeko la utumwa na unyanyasaji, magonjwa, vifo miongoni mwa mengine. Mabadiliko haya yameathiri maisha ya wahusika katika riwaya kwa njia moja au nyingine. Kwa mfano:

4.2.5.1 Mabadiliko ya kimazingira

Mabadiliko yanajitokeza katika hali au mambo yanayomzunguka kiumbe katika sehemu anakoishi au maisha yake. Riwaya Mpya inadhihirisha mazingira yaliyojaa uhai na matumaini ya uhai zaidi. Kulikuwa na miti, mito, visima, mifugo miongoni mwa mengine. Kinyume ni kuwa kumekuwa na mabadiliko makubwa katika kipindi cha sasa. Haya yote yameadimika ama hayako kabisa. Kwa mujibu wa Riwaya Mpya, hii ni kwa sababu ya uongozi wa ubaguzi; kuyapa masuala yasiyo muhimu kipau mbele kama vile kuendeleza biashara za kukata miti kwa lengo la kuuza mbao au kuchoma makaa. Kwa upande mwingine, uvumbuzi wa mashine na mitambo mbalimbali kama bomu yameweza kutatiza uhai wa viumbe na mimea katika mazingira. Aidha hewa safi iliyoshuhudiwa kabla ya miaka ya utandawazi imepotea na kuwa historia. Uvumbuzi huu umeleta mabadiliko katika hali ya anga. Haya yameathiri mazingira na hata hali ya maisha ya wahusika. Kwa mfano, maji kukaushwa kwa sababu ya ukataji miti. Isitoshe, visima na vijito vimekauka na kufanya watu kutafuta maji kwa hali na mali. Athari ya ukame vilevile huathiri mifugo. Wakulima hawajafaulu kamwe na mifugo yao. (Wamitila 2002: 90).

Mabadiliko yameangaziwa katika hali ya anga. Ambapo, ni vugumu sana kutabiri misimu mbalimbali kama ilivyokuwa hapo awali. Mabadiko haya yanazua matatizo zaidi kama vile magonjwa na kuumiza wakazi, mifugo na mimea. Athari yake ni hatari, hata husababisha vifo. Kwa upande mwingine, uchafu, taka za kila aina zinatupwa ovyo: karatasi, sandarasi, plastiki, mipira, matambara, maganda ya matunda, majani makavu na mabichi, unaoelekezwa kwenye mito na maziwa kutoka kwenye viwanda yameweza kuathiri viumbe vya majini kama samaki, (Wamitila 2002: 26). Maji haya yanaathiri wanaotumia kwa kusababisha magonjwa kama vile kipindupindu. Samaki ambao ni chakula cha binadamu huwa adimu na hii huzua njaa na hata kupotea kwa ajira kwa wavuvi.

> Wamemwaga mafuta hapa samaki wafe wapate sababu ya kutuletea makopo. Huko juu wanatupa mabaki ya nyuklia! Huo si utando, ni mafuta yaliyomwagwa. Wanasema ilitokea kama ajali. Sehemu hii haina samaki wanaoishi; wamekufa wote. Kaza macho huko mbele, huko... Je, unaona kitu chochote? (Wamitila 2002: 88, 111). Niliteremka haraka haraka (sehemu yenyewe ilikuwa ni mteremko mkubwa ajabu) hadi nilipotokeza pahali palipokuwa na milima wa uchafu. Niliweza kukiona kikundi cha watoto wengi waliokuwa wakichakura na kukomba vitu kwenye uchafu. (Wamitila 2002: 23).

Kupotea kwa ajira ni chanzo cha umaskini. Aidha, milima ya uchafu imetawala miji ya nchi zinazoendelea. Milima hiyo ya uchafu imekuwa kama tegemeo la wasiojiweza. Hii ni kwa sababu wanatafuta mabaki ya chakula katika takataka hizo na kuvila. Watu hawa hata wakabandikwa jina la ‘chokoraa’ kwa sababu ya kuchokorachokora uchafu kwa lengo la kuishi. (Wamitila 2002: 23). Dunia imezidi kudunika.

4.2.5.2 Mabadiliko ya miundo misingi

Kinyume na matarajio ya wengi kuwa utandawazi ungeleta uimarishaji wa miundo misingi, Riwaya Mpya imeweza kuonyesha kuwa miundo misingi huzidi kudorora. Hakuna kipimo sawa katika maendeleo. Miundo misingi katika miji mikuu ndio huzidi kuimarika. Kwa mfano, barabara, hospitali, na hata vyuo vya elimu. Mashinani barabara hazipitiki na hakuna dawa kwenye zahanati. Kwa mfano, riwaya ya *Babu Alipofufuka* hudhihirisha jinsi barabara zimeharibika. Isitoshe, magari hayapitii tena, sehemu nyingine ni maafa na sehemu nyingine nafuu.

> Ndivyo ilivyo barabara yenyewe. Sehemu nyingine maafa na sehemu nyingine nafuu. ...bomba limepasuka na kubwabwaja maji, sasa karne nzima, na hivi lilivyo kama pua ya ng’ombe, nyekenyeke. (Mohamed 2001: 19).

Miundo misingi imedorora na hakuna maendeleo yoyote yanayoweza kutekelezwa. Hii ni kwa sababu ya uongozi ambao unashinikiza maendeleo katika miji mikuu na kusahau vijiji. Teknolojia na sayansi ambayo ilitarajiwa kuenea mashinani yanakaliwa na viongozi kwa manufaa ya miji na ya kuendeleza makasri yao.

4.2.5.3 Ukosefu wa utu

Kitambo kulikuwa na amani. Watu waliishi kwa udugu, matatizo ya jamii yalisuluhishwa kwa mashauriano. Watu walikuwa wanaheshimu vitu vya wengine. Lakini kwa mujibu wa Riwaya Mpya ya Kiswahili, sasa kumekuwa na mabadiliko chungu nzima. Hakuna heshima na udugu. Hili limesababishwa na ubinafsi, hali ya kutaka kila kitu. Watu wanataka kuwa na sarafu au noti zilizotolewa na kuidhinishwa na serikali au benki kuu bila jasho. Kitambo kulikuwa na dhuluma lakini wezi walikuwa na haya ya kujificha angalau nyuso zao. Lakini siku hizi, hakuna kujificha. Watu wanashikili vitu vya watu kwa mabavu. Desturi ya kistaarabu haipo tena, ile hisia ya mtu mmoja kwa wengine. Kwamba uso umeumbwa na haya na kuna imani na huruma. Hali hii imezua tamaa, na tamaa kuzaa wizi wa kimabavu, unajisi, ushoga, miongoni mwa mengine. Kwa mfano:

> Huyu ndiye aliyegundulikana akifurahia mchezo wa mbwa wake na msichana mmoja. Watu wengine husema kwamba raha ya kutazama inapomnogea, hujigeuza mbwa na kugawana tija na mbwa wake! Virusi vya unajisi wake vimeenea katika miili ya wasichana. Watu wengine husema hata wavulana huchezeshwa mchezo huo aliozoea kuucheza kwa muda mrefu mpaka alipofumaniwa. (Mohamed 2001: 14).

Ukosefu wa utu hudhihirika katika maisha ya wageni wanaozuru nchi zinazoendelea. Kwa mfano, masuala ya ushoga ni masuala ambayo hayakuwa mwanzoni lakini sasa ndio wimbo unaoimbwa na vijana kwenye sehemu za burudani. Hii hutokana na athari ya mahusiano ya watu wenye tamaduni mbalimbali. Isitoshe, wanyama pia hawajaachwa nyuma. Di Livio, mhusika katika riwaya ya *Babu Alipofufuka,* anaendeleza kitendo hiki.

4.3 Tathmini ya Mbinu za Kuangaza Utandawazi

Kwa mintarafu ya madhumuni ya pili: kutathmini mbinu zilizotumika kuangaza utandawazi, uchanganuzi wa deta uliangazia jinsi mbinu hizi zikiwemo kinaya, vurugu la kiwakati, ucheshi na uhalisia-ajabu zilivyotumika kuwasilisha suala la utandawazi. Mihili ya Usasaleo kama vile mwingiliano matini, uasi na vurugu la kiwakati ilirahisisha uchanganuzi wa deta. Ilidhihirika kuwa majukumu ya mbinu hizi zilizotumika katika Riwaya Mpya ni kuepuka makali ya walioathirika na kutashtiti hali ya utandawazi ilivyo katika jamii kwa upya wa kipekee. Williams (1999) anafafanua kuwa mbinu hizi ni mikakati ya kimajaribio katika sanaa na pia hulenga

kuchanganua ukosefu wa udhabiti katika michakato ya kijamii. Kufaulu kwa majaribio haya yalidhihirika katika kutathmini mbinu hizi. Riwaya Mpya ya Kiswahili hujengwa na mbinu hizi:

4.3.1 Uhalisia-ajabu

Katika matumizi ya uhalisia-ajabu, waandishi wamebuni ulimwengu mbadala kwa lengo la kukosoa masuala ambayo uhalisia wa kijamii hutegemea ili kuwepo. Njogu (1987) anaeleza sifa ya uhalisia-ajabu kama matukio yasiyoaminika ya kifantasia. Mambo ya kiajabu huelezwa kwa namna ya moja kwa moja na kuonekana kuwa ya kawaida, hali za kushangaza na kuogofya. Matukio huendelezwa kama kwamba ni ya kawaida, ndoto na uhalisia huchanganywa na wakati hausongi. Haya, hujumuisha kiontotolojia, kisiasa, kijiogorafia au kiutanzu. Kwa mfano, katika Riwaya Mpya, wahusika wengi ni wa roho tu au mizuka. Wanaongozwa na sauti, mwangaza au wanyama fulani katika safari zao. Pia, mambo mengi hufanyika katika ndoto tu. Katika kushughulikia suala la utandawazi, mbinu ya uhalisia-ajabu imetumika ili msomaji aweze kuona picha kamili ya utandawazi: hasi au chanya. Kwa hakika, uhalisia-ajabu umesawiri utandawazi kama ukosefu wa udhabiti wa kijamii, kisiasa na kiuchumi katika mataifa ya Afrika Mashariki.

Uhalisia-ajabu umetumika kuonyesha athari ya utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Katika riwaya ya *Bina-Adamu!*, mhusika Bina-Adamu wakati wa safari yake ndefu, anaongozwa na mbabe, akisaidiwa na sauti ya ajabu, ya mwanamke mwenye sifa zisizo za kibinadamu anayeitwa Hanna, anazuru Ulaya ambayo ‘inaishi jana’, Asia ya viwanda ambayo ‘inaishi kwa matumaini’ na Afrika, ambayo inaishi mwishoni mwa *kijiji cha utandawazi* na imeharibiwa na njaa na vita. Anapokuwa njiani kila pahala anakutana na mambo yanayoonekana hayana mantiki, mambo ambayo hayaelezeki yanayofanywa na P.P mwenye miujiza – Ulaya P.P ameushinda ufashisti lakini bado anaishi imara miongoni mwa wafuasi wake. Mhusika huyu anafanya vitu vingi vya kuleta madhara kwa wanajamii hasa katika nchi zinazoendelea. Kwa mfano, huko Asia alitupa bomu ya Hiroshima, bomu ambalo liliathiri hali ya afya ya walionusurika kifo. Wengine wakaambukizwa magonjwa yasiyotiba. Afrika, alitumia jiwe kuvigonga vichwa vya wanasiasa kuvitoa akili. Huko Urusi, ambako P.P alizuru kwa muda mfupi, haitambuliki alifanya nini kwa sababu anamwogopa Stalin. P.P anaiuza Afrika kwa watalii wa kigeni, anaharibu bahari kwa mafuta na mabaki machafu ya ‘radioactive’.

Mwishoni mwa safari yake mbabe aligundua Amerika–Bustani ya Adeni ya pili, ambamo wakazi wa nchi zinazoendelea, wakidai kwamba wanaishi leo na tena wanaishi katika uhalisia wa mambo. Uhalisia-ajabu umetumika kuonyesha jinsi mahusiano kati ya mataifa yaliyo na uwezo

wanatumia nguvu zao, uwezo wao na hata itikadi kunyanyasa nchi changa zinazoendelea. Hivyo utandawazi ni suala ambalo wasomi wengi huchukulia kuwa huleta mataifa ya ulimwengu karibu kwa misingi ya kijamii, kiuchumi na kisiasa lakini kupitia uhalisia-ajabu, ni wazi katika Riwaya Mpya kuwa utandawazi huzorotesha na kugawa mataifa mbalimbali.

Imani potovu imejengwa na viongozi ili kuzidi kuongoza. Mhusika Bina-Adamu katika riwaya ya *Bina-Adamu!* anasema kuwa alipozaliwa aliwakuta watu wakiogopa kiini chao, mpaka leo hii anapoisoma hadithi ya *Bina-Adamu!* bado wanakiogopa. Sababu ya kuogopa kiini cha kijiji ni kwamba mtu ambaye angethubutu kwenda kwenye kiini chake angepatwa na madhara makubwa. Kwa mfano, mwanaume anayekwenda huko anaweza kushtukia amebadilika jinsia na kuwa mwanamke kwa kuwa sharti alizunguke jabali liliko kijijini. Kwa kweli jambo hili si jambo la kawaida bali lilitumika kama mbinu ya kutawala akili na kuwadhibiti wanajamii. Ni wazi kuwa, viongozi wanaotawala huunda visasili vinavyowawezesha kushika hatamu ya uongozi kwa miaka na mikaka. Hivyo, uhalisia-ajabu huangazia kiini cha ubinafsi katika uongozi. Ubinafsi huu ulianzishwa na mabeberu kwa lengo la kuaminiwa na watawaliwa. Mtandao huo wa ubinafsi ukapitishiwa viongozi wa nchi zinazoendelea. Athari yake ikawa unyanyasaji wa wanaotawaliwa kwa lengo la kunufaisha kiongozi. (Wamitila 2002: 7).

Pia, katika riwaya ya *Bina-Adamu!*, kwenye kitovu cha kijiji, uhalisia-ajabu umedhihirishwa pale ambapo mhusika Bina-Adamu anaanza safari ya kutafuta suluhisho katika kijiji chake. Pia, hapo alipoanzia ndipo anapomalizia baada ya safari. Vilevile, katika safari, Bina-Adamu anawatafuta wale huntha (wasichana-wavulana) watatu wanaosemekana ndio chanzo cha laana katika kijiji chake. Ajabu ni kwamba kila mahali alikoenda, aliwasikia wakicheka mara kwa mara lakini hawaonekani. Majina ya huntha hawa alivyoeleza Babu wa Zakongwe ni Abubepar, Binberi na Mwajihawa. Wahusika hawa wanadhihirika tu katika matendo na fikra. Hivyo ni wazi kuwa wanadhihirika katika matendo na fikra za kibepari, ubaguzi wa rangi na ubinafsi: ambazo ni chanzo cha utandawazi. Mwandishi anapitisha ujumbe kuwa, matatizo yanayowakumba nchi za bara la Afrika, suluhisho limo papa hapa barani na suluhisho kwa hakika si utandawazi bali ni utu, mapenzi na kutambua kiini cha kuwako kwao. (Wamitila 2002: 9).

Msafiri amezuru nchi mbalimbali kama vile Ujerumani, Japan na Urusi na pia mabara tofauti tofauti kama vile Afrika, Merekani, Asia na Uropa. Kila mara katika safari yake ya kuwasaka wale wavulana-wasichana, *Bina-Adamu!* alinusa harufu ya beberu. (Wamitila 2002: 14-15). Harufu ya beberu ilijitokeza kila mahali palipokuwa na alama ya maafa yaliyosababishwa na P.P

ambaye ni kiwakilishi cha Marekani. Katika uhalisia wa kawaida, beberu (mbuzi dume) hutoa harufu mbaya hivi kwamba mtu akimkaribia hubaki kunuka ile harufu. Maana ya ‘’beberu’’ katika muktadha wa riwaya ya *Bina-Adamu!* ni mkoloni ambaye pia aliitwa beberu. Kihistoria, harufu yake ni maafa yaliyofanywa na mkoloni ambaye bado yuko ingawa aliondoka. Isitoshe, ni wazi katika muktadha wa riwya mpya kuwa, beberu husimamia wawakilishi wa utandawazi, harufu yake imesambazwa kote ulimwenguni. Popote harufu hiyo imenuswa, lazima kuwe na maafa.

Riwaya ya *Dunia Yao* inaombolezea viongozi wanaowekewa wananchi. Mwandishi amekemea dhana ya utandawazi iliyoingia vichwani mwa viongozi na watu wetu. Ametumia uhalisia-ajabu kuonyesha mhusika kukimbia nafsi yake, familia yake, marafiki, majirani na jamii kwa jumla. Hii inamfanya aishi katika chumba chake bila ya kuzurura. Akili yake huzurura katika ndoto tu. Anaamua kuwa mpenzi wa kompyuta: *mtu-mashine* pekee aliyebaki katika maisha yake anayeweza kumwamini, kuzungumza naye, kushauriana naye, kumtumia kama kiwango cha kuandikia historia na hadithi yake na hadithi za watu wengine na kiwango cha kuweza kuzungumza na binti yake ambaye anaishi London kama mkimbizi njaa, (Mohamed 2006: 11).

Aidha, uhalisia-ajabu hudhihirika wazi katika *wahusika-picha* ambao wanasimama kutoka katika albamu na kuwa viumbe vyenye ngozi, nyama, damu na mifupa. Wanakuwa viumbe wenye uwezo kamili kama binadamu wa kawaida. Hii inamfanya msomaji kutupia jicho kali uhalisia mpya ambao una ukweli wa aina nyingine, uhalisia wenye mkanganyo na utata:

> Sasa aliinuka Yungi katika lile albamu. Bi M akawa kasimama vilevile,
> Hakwenda kulala kwenye bapa la albamu. Alijua bado nina haja naye.
> Itabidi anifungulie mlango usiku wa manane. Na nilipoingia ukumbini tu,
> kabla hata sijatua, alinivamia. (Mohamed 2006: 23).

Pia, kuna mhusika ambaye ni mtoto mkombozi. Tokea siku yake ya kuzaliwa anaonyesha sifa za kiajabuajabu kama vile kusema, kula, kutembea na kuwashauri watu kama mtu mkubwa. Matambiko yanayohusishwa na Miungu ya Kiafrika kama ile ya *kosmolojia* ya Waigbo wa Nigeria ni mifano ya uhalisia-ajabu. Mbinu hii imetumika kuonyesha mporomoko wa kila kitu katika jamii yetu- uchumi, utamaduni, uhusiano wa watu umesambaratika. Kila mtu yu kivyake. Kwa hakika, ni wazi kuwa ‘Mungu kwa wote, kila mtu kivyake’. Mwandishi wa riwaya ya *Dunia Yao*, hurejelea ubinafsi huu kama fensi mpya; ‘carnival ya globalization’, na kwa hivyo,

kila mtu anavaa kivyake, anajirembesha kivyake, anajifurahisha kivyake, anafanya kinyago kivyake. Yaani, kila mtu na vituko vyake. Ubinafsi huu umeleta ukosefu wa adabu, ukosefu wa heshima na hata kufanya watu kutojaliana katika hali mbalimbali ya maisha. Hakuna uhusiano wa karibu wa baba na bintiye. Kwamba hayo ni mambo ya kale maana yameshapitwa na wakati, (Mohamed 2006: 107).

> ***Globalization*** mara ***Americanization***... Likapita kwa kasi na pepo zake za dhoruba likiripuka mandimi ya moto yaliyounguza na kukausha kila kitu: watu, wanyama, barabara,majumba, miji na majiji, mashamba, mazao ya chakula, mazao ya mauzo, miti, maji, hewa, pwani, bahari, nchi kavu, madini, umeme, mafuta, hospitali, madawa, benki, viwanda, biashara, rasilmali zote ...shule, vyuo, desturi, mila, tamaduni na hata uhai, heshima na mustakabali wa watu- hata roho zao. ...Liliingia humo na kutawala na kuamrisha na kulazimisha mambo katika nyumba yake mwenyewe mtu. (Mohamed 2006: 206).

Mwandishi wa *Dunia Yao* ametumia uhalisia-ajabu kukemea utandawazi. Kwake, hurejelea utandawazi kama utandawizi ili kuonyesha uozo na ukosefu wa uthabiti katika michakato ya kijamii kisiasa na kiuchumi. Kwake, utandawazi ni kama giza zito la maangamizo. Anadhihirisha haya kwa kuonyesha athari ya uvumbuzi wa kisayansi kama vile nyuklia, mabomu na vilipuzi vingine. Haya, yameathiri watu, wanyama, barabara, majumba, mashamba na kadhalika.

4.3.2 Vurugu la kiwakati

Vurugu la kiwakati limetumika katika Riwaya Mpya kwa lengo la kujenga kinaya na kusawiri taswira ya utandawazi. Wamitila (2003) anaeleza kuwa nyakati hurudiana, hubadilika na hata kutengana katika mbinu ya vurugu la kiwakati. Katika uchanganuzi wa deta, mbinu hii imetoa mtazamo wa mwandishi kuhusu suala la utandawazi na hata kujenga taswira ya utandawazi kwa njia ya ucheshi au kubeza. Visa kadha vinasawiriwa vyote vikijiri wakati mmoja. Katika kujenga kinaya, waandishi wa Riwaya Mpya walitumia vurugu la kiwakati kuchambua masula ya kabla, wakati na baada ya ukoloni. Hata baada ya kutembea kwa muda mrefu kujua kiini cha matatizo, bado hakuna uvumbuzi. Kiini ni kuwa utandawazi ambao hudhaniwa kuwa huleta maendeleo ndio hubomoa maendeleo ya awali:

> Nilitembea kwa kipindi kirefu ambacho siwezi kujua kama ilikuwa siku nzima, mwongo mmoja au miaka kadha. (Wamitila 2004: 34). Baada ya miaka ya 42 ya udhia hakuna kinachoaminika tena... Nilikuwa kama kitoto kichanga kinachoanza kwenda tata-kitoto cha miaka 42. Niliongozwa na mazoea ya miaka 42 ya kwenda gizani kuliko kweupeni. (Mohamed 2006: 5).

Visa mbalimbali vimesawiriwa vyote vikijiri wakati mmoja. Katika riwaya ya *Musaleo!*, kuna visa mbalimbali ambavyo huelezwa kwa wakati mmoja. Mwishowe, visa hivi vinaingiliana na kukamilishana katika kuonyesha suala la utandawazi. Hadithi tatu kuu zinazosimuliwa ni pamoja na ile ya Mugo Wehu anayosimulia mwenyewe, ya mtunzi wa fasihi Kingunge anayoandika mwenyewe na ile ya mwandishi anaelezea kuhusu wahusika wake mbalimbali.

4.3.3 Mbinu ya Uasi katika Kufafanua Utandawazi

Mbinu hii ni kipengele kikuu katika nadharia ya Usasaleo. Ni mojawapo ya mihimili inayotofautisha Riwaya Mpya na riwaya tangulizi. Wamsley (2006) anaeleza mbinu hii kama hali ya kuvunja au kutofuata sheria zilizopo au zilizokuwepo katika uandishi wa tanzu za fasihi. Uasi huu wa sheria hudunisha mantiki ya muumano wa kazi kama vile msuko, uhusika, matumizi ya lugha na muundo. Aidha, kauli kuwa fasihi huiga au huzingatia yaliyomo maishani yanapingwa. Hivyo matumizi ya mbinu zingine kama vile fantasia, visasili, viroja au vipengele vya bunilizipendwa kama zile za sayansi hutumika. Ni kwa msingi huu ndipo mitazamo ya waandishi kuhusu suala la utandawazi limeshughulikiwa kwa undani ili kuonyesha taswira yake kamili katika nchi zinazoendelea. Kupitia uasi, riwaya hii huchunguza ukweli wa maisha, namna ambayo inatofautiana na mitazamo ya uhalisia wa kimaadili na kihisia wa wanariwaya tangulizi.

Matumizi ya visasili katika Riwaya Mpya ni njia moja ya kuasi sheria za utunzi. Ilikuwa wazi kuwa kazi za fasihi hasa riwaya, lazima zingetumia lugha nathari kuhifadhi amali mbalimbali ya kijamii. Wamitila (2003) anaeleza visasili kama mtindo ambao ulitumika katika masimulizi ya kitambo au bunilizipendwa. Malengo ya visasili yalikuwa ni kueleza asili na kukua kwa maendeleo ya dunia na watu, matukio mbalimbali ya dunia na juu ya matendo ya kishujaa ya majaribosi waliokuwa na nguvu zisizo za kawaida na waliokuwa na uwezo wa kupambana na miungu na mashetani. Hivi watu walikuja kuelewa masuala mazito kama vile kiini chao na sababu yao kuishi. Hata hivyo, Riwaya Mpya imeweza kutumia mbinu hii katika kueleza

masuala yanayokumba jamii. Lengo kuu la matumizi ya visasili katika Riwaya Mpya ni kuzindua mtu na kuwa na mwamko juu ya masuala ya kiitikadi, kisayansi miongoni mwa mengine ili kuondokana na udumavu wa fikra. Kwa mfano, katika riwaya ya *Bina Adamu,* Bina-Adamu anasema kuwa, alipozaliwa aliwakuta watu wakiogopa kiini chao, mpaka leo hii anapoisoma hadithi ya *Bina-Adamu!,* bado wanakiogopa. Sababu ya kuogopa kiini cha kijiji ni kwamba mtu ambaye angethubutu kwenda kwenye kiini chake angepatwa na madhara makubwa. Kwa mfano, mwanaume anayekwenda huko anaweza kushtukia amebadilika jinsia na kuwa mwanamke kwa kuwa sharti alizunguke jabali liliko kijijini. Kisa hiki kinaonyesha jinsi viongozi hubuni visa mbalimbali kwa lengo la kubaki uongozini milele, suala ambalo limesababishwa na utandawazi.

Matumizi ya fantasia katika kueleza visa mbalimbali pia ni mfano wa uasi. Waandishi wa Riwaya Mpya wameeleza visa mbalimbali kwa njia ambayo si ya moja kwa moja. Visa hivi humwezesha msomaji kudadisi mazingira yake. Kwa mfano, mhusika Bina-Adamukatika riwaya ya *Bina-Adamu!* anapoanza safari ya kukiuka visasili, anapewa mkoba na Babu wa Zakongwe uliokuwa na utu, mapenzi na kiini cha kuwa kwake. Pia, anaonywa autunze na asiudharau sababu ya sura yake kwani mwacha asili ni mtumwa. Jambo la uhalisia-ajabu ni kwamba huwezi kutia utu au mapenzi kwenye mkoba. Hii ina maana kuwa utu na mapenzi ndiyo kiini cha maisha mazuri. Fantasia hii hudhihirisha kuwa japo tunatangamana na tamaduni mbalimbali, tusisahau kiini cha tamaduni yetu yaani utu na mapenzi.

Uasi unajidhihirisha katika ule uhuru wa waandishi wa Riwaya Mpya kuweza kujitwika jukumu la kuunda misamiati au istilahi maalum. Pia, kutumia au kufinyanga maneno kwa njia inayokidhi mahitaji yake katika maelezo. Hii ni wazi hasa mwandishi anapotaka kueleza hali fulani, anajiundia neno au maneno ili msomaji aweze kuona au kuhisi hali hiyo. Aidha, dhana fulani huwasilishwa kutokana na misamiati hiyo iliyobuniwa. Kwa mfano, Mohamed (2001: 3, 14, 110) kuna maneno kama vile: neno ‘kimvumeme’ kurejelea chombo cha umeme cha kukaushia nywele kwa mvuke, neno ‘mduma’ kumaanisha anayetisha, ‘mpatapataye’ kurejelea apataye yeyote kwa kinyang’anyiro au bahati nasibu. Maneno mengine ni kama vile: ‘n’kupenda-n’kushuke-kasheshe’, ‘ukofiwatu’, ‘nakuona-wewe-mimi-hunioni’, ‘tumejitoa-tumejitia-wasasa’. Katika riwaya ya *Dunia Yao* kuna maneno kama vile: ‘ki-hybridhybrid’, ‘pangaboi’, ‘superboyswawili’, ‘wauza-tarabizuna’ miongoni mwa mengine. Katika riwaya ya *Bina-Adamu!,* kuna maneno kama vile: ‘*Bina-Adamu!*’, ‘FUJO ASILIA’, UMERO-JAPA’, ‘zakongwe’,

‘binrangi’, riwaya ya *Musaleo!* kuna maneno kama vile: ‘Mzee-mvumbua usomi’, ‘Mzee Mleta Mvua’, ‘Baa-Lini’, ‘Njaamani’ miongoni mwa mengine. Maneno haya yanaashiria mkemeo wa suala la utandawazi. Matumizi yao yameleta dhana ya unyanyasaji, utawala wa udikteta na athari za utandawazi hasa katika nchi zinazoendelea.

Kuna ukiukaji wa sheria za lugha na matumizi mengi ya maneno ya kigeni kuleta dhana ya utandawazi na kusisitiza usomi wa riwaya yenyewe. Kwa mfano, katika *Babu Alipofufuka* kuna maneno kama vile ‘Proteus’, ‘Limonsin’, ‘Neo-casino’, ‘FKK’, ‘CD-ROM’ miongoni mwa mengine. Kuna uvunjaji wa kanuni kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Yao*:

> Baada ya barabara kupanuliwa kupitisha watoto wa utandawazi **a**kiiwemo utalii! El Ninyo **a**mezaliwa. Na**ye** siku hizi kuliko zamani, hudandisha jua ili ardhi ichanike vipande vipande. El Ninyo **h**anyeshi tenaa mvua tu! Sasa na jua pia. Hakuna kinachomea ndani ya tanuri lake. (Mohamed 2006: 62, 65).

Uasi umewasilishwa kwa matumizi ya kutokuwa na uhakika. Kutokuwa na uhakika na jambo lolote kama vile chakula, makazi, elimu, matibabu, heshima ya mtu, heshima ya nchi, uraia wa mtu, heshima ya Uafrika ambapo tokea mwanzo ilikuwa imekandamizwa sana wakati wa ukoloni. Hii humwacha msomaji katika hali ya kutojua kinachozungumziwa. Kwa mfano, katika riwaya ya *Bina-Adamu!* mwandishi anapozungumzia *Structural Adjustment Programmes*, ni vigumu kujua anarejelea nini haswa. Lakini ni wazi kuwa analalamikia na kuhitisha udhalimu wa utandawazi (uk. 137): anasema SAPS zinasapa uhai. Kijiji cha wizi hiki. Dola inakaba na Yen ni kama ya kitanzi.

Uasi ni wazi katika sanaahati (graphic art) ambapo waandishi wanacheza na mwandiko wa maneno ili kutoa hisia fulani ya kimaana au ujumi. Hii inamwezesha msomaji kutilia maanani neno hilo. Sanaahati katika Riwaya Mpya imetumika kwa maksudi ili kutoa taathira za utandawazi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, maneno kama vile *Proteus* na *Limonsin* yameandikwa kwa sanaahati. Katika riwaya ya *Dunia Yao,* maneno kama vile *wewe* na *mimi, superboyswawili* na *ilhamu* ni baadhi tu ya maneno yanayoashiria taathira katika utandawazi.

4.3.4 Kinaya, Masihara na Ucheshi-bwege

Hizi ni baadhi ya mbinu ambazo hubainika sana katika kazi za baada ya usasa. Japo hazikuanza na baada ya usasa, zimetumika sana katika vuguvugu hili. Huhusu kuangaza maswala mazito kwa njia ya mchezo. Mbinu hizi hudhihirika katika uwekaji sambamba na ulinganuzi unaomfanya msomaji kulinganisha sifa za uzuri na za ubaya zinazowekwa pamoja. Ulinganuzi ni ulinganishaji wa vitu viwili vilivyowekwa pamoja ili tathmini halisi iweze kutolewa. Ulinganishaji huu ndio msingi wa kinaya, masihara na ucheshi bwege katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Maudhui mengi yamejengwa kutokana na mbinu hizi. Kwa mfano, viongozi wanapotafuta uongozi wanatoa ahadi ambazo hawatimizi. Wakati huo wanajifanya wazalendo. Riwaya ya *Bina-Adamu!* inafafanua jinsi suala la utandawazi limebinafsisha uongozi. Viongozi wote wanang'ang'ania kukwea paani. Kwa ahadi zao, wanafaulu lakini ni kinaya kuwa wanakaa huko juu paani, huko ndiko wanakochumia matunda kwa urahisi na kuwatupia watu walioko chini ambao ndio waliowashikia ngazi ya kupanda juu. Masihara hutokea kutokubali kushindwa ambapo walioshindwa kutwaa uongozini wanaamua kuchoma nyumba ili kiongozi alyechaguliwa asifurahie matunda ya uongozi wake.

Wasomi ni watu walioheshika katika nchi mbalimbali. Heshima hutokana na ujuzi walionao wa kuvumbua na kuendeleza mawazo mapya. Mawazo haya ya wasomi huchukuliwa kama msingi wa kuboresha maisha na mazingira wanamoishi watu. Kinyume cha matarajio hudhihirika katika riwaya ya *Musaleo!*, mhusika Profesa ambaye ni msomi aliyetegemewa na wananchi katika kukomboa nchi kupitia elimu yake anasaidia kuendeleza uongozi mbaya badala ya kuupinga. Suala la elimu ambalo ni kiini cha utandawazi hukosolewa katika sehemu hii. Mtazamo huu hudhihirisha kuwa baadhi ya wasomi hutumia masomo yao kuendeleza uongozi mbaya ambao huathiri mwananchi wa kawaida. Kwa njia hii inatambulika kuwa matatizo ya mwananchi husababishwa na wasomi ambao wanastahili kutatuta matatizo hayo.

Katika kujenga kinaya, waandishi wa Riwaya Mpya walitumia vurugu la kiwakati kuchambua masula ya kabla, wakati na baada ya ukoloni. Hata baada ya kutembea kwa muda mrefu kujua kiini cha matatizo, bado hakuna uvumbuzi. Kiini ni kuwa utandawazi ambao hudhaniwa kuwa huleta maendeleo ndio hubomoa maendeleo ya awali. Baada ya miaka kadha, hakuna maendeleo katika nyanja mbalimbali. Miundo msingi, afya ya wananchi unazidi kudorora kwa magonjwa yanayotokana na mazingira duni. Kwa kutumia ucheshi bwege, waandishi wa Riwaya Mpya wanajenga taswira halisi ya nchi zinazoendelea:

> Baada ya miaka ya 42 ya udhia hakuna kinachoaminika tena... Nilikuwa kama kitoto kichanga kinachoanza kwenda tata-kitoto cha miaka 42. Niliongozwa na mazoea ya miaka 42 ya kwenda gizani kuliko kweupeni. (Mohamed 2006: 5).

Mambo ya kifo yaliweza kushughulikiwa kama masihara na hisia za kifo kuondolewa kabisa. Kwa mujibu wa Riwaya Mpya, maisha mazuri hutarajiwa baada kifo. Kifo kimekuwa kama mwamko mpya katika utendaji wa utu. Waliohai hawawezi kutambua mambo mengi yanayotokea katika jamii yao. Uwezo wa wafu kuzungumza na kuwapa watu mwelekeo ni thibitisho tosha kuwa baada ya kifo kuna raha. Mhusika Babu katika Riwaya ya *Babu Alipofufuka* ni mfano wa umuhmu wa ufufuzi baada ya kifo. Riwaya Mpya huonyesha matumaini baada ya kifo: uongozi wa utandawazi kuharibu nchi changa zinazoendelea. Suluhisho ni raia kufufuka kupinga unyanyasaji wa utandawazi kisha kujisaili upya na kutambua maana ya maisha. Kufufuka ni kujikomboa kutokana na pingu za historia, kufisha ubinafsi na kufufua matumaini ya udugu kama mwanzo mpya. Pia, lazima watu watambue kiini cha kijiji (utandawazi) kwa kuanza safari ya Bina-Adamu. Safari hii ya binadamu lazima iwe na utu, mapenzi na kutoacha mila na tamaduni ya jamii, haya yameelezwa katika riwaya ya *Bina-Adamu!*. Kutopoteza mkoba wa Mzee (asili ya Uafrika) unaobeba utu, mapenzi na kuweko kwetu. Na hii inahitaji kujiua na kujifufua- mtindo mpya, kujiua kwa maslahi ya nchi nzima; kwa ajili ya vizazi vitakavyokuja baadaye.

4.4 Tathmini ya Mitazamo ya Waandishi kuhusu Utandawazi

Waandishi wa Riwaya Mpya wameweza kuonyesha mitazamo yao kuhusu suala la utandawazi kwa njia mbalimbali. Mitazamo yao huchukua mikondo tofauti japo ni dhahiri kuwa wanakemea suala la utandawazi katika nchi zinazoendelea. Matumizi ya Udenguzi na vipengele vya Usasaleo ni dhihirisho tosha kuwa waandishi wa Riwaya Mpya ya Kiswahili wanamitazamo fulani kuhusu jamii yao. Walibora (2010) na Khamis (2010) wanakubaliana kuwa mabadiliko katika tanzu ya riwaya ni mwondoko wa kutoa sura iliyozoeleka na kwenda sura mpya na pia kuepuka kupooza na kushindwa kushawishi kwa fikra na umbuji. Khamis (2007) ana maoni tofauti kuwa matumizi ya vipengele vya Usasaleo na Udenguzi ni kusawiri ukosefu wa udhabiti wa kijamii, kisiasa na kiuchumi. Katika kuonyesha ukosefu wa udhabiti, waandishi wa Riwaya Mpya ya Kiswahili wameweza kuonyesha mitazamo yao kuhusu utandawazi. Mitazamo yao hudhihirika kutokana na matumizi yao ya lugha wanapoeleza suala zima la utandawazi ikiwemo

lugha ya mkemeo na uundaji au matumizi ya maneno fulani yenye taathira. Aidha, fani mbalimbali za uandishi kama vile mazungumzo, nyimbo, taswira, kinaya na jinsi wahusika wanavyoeleza kuhusu suala zima linaonyesha mitazamo ya waandishi hawa:

4.4.1 Lugha ya Mkemeo

Sanaa ya lugha katika fasihi ni chombo muhimu katika kupitisha ujumbe. Katika Riwaya Mpya matumizi ya lugha yamegawika katika sehemu tatu: matumizi ya lugha kimazingira (lahaja): matumizi ya lugha kimandhari (uteuzi wa misamiati kulingana na muktadha) na matumizi ya lugha kisanaa (tamathali za usemi). Matumizi ya lugha kimandhari yameongoza uteuzi wa misamiati na hii imeleta toni mwafaka katika vitushi vinavyoonyesha mitazamo ya waandishi. Matumizi ya lugha kisanaa yamejenga mitazamo ya waandishi wa Riwaya Mpya hasa kuhusu dhana ya utandawazi. Waandishi wa Riwaya Mpya wameweza kutumia maneno ambayo kwa hakika yanakemea au kuonyesha jinsi utandawazi umeangamiza nchi na wananchi. Maneno haya yametumika kwa maksudi ili taswira kamili na mitazamo yao kuhusu suala zima lidhihirike waziwazi. Lugha ya mkemeo imetumika kusuta uongozi mbaya unaoendelezwa na viongozi walioathirika na mfumo wa ukoloni mamboleo. Uongozi huo uliojaa ubinafsi huzidisha pengo baina ya matajiri na maskini. Haya yanasababisha mgomo kwa wafanyakazi na, wanyonge. Kwa mujibu wa Riwaya Mpya, utandawazi hivyo badala ya kuwaletea watu kazi na mali, umeleta uchoyo, ubinafsi na ufisadi. Mali hazisambazwi kwa njia ya usawa katika maeneo mbalimbali na hivyo sehemu fulani za miji na vijiji zimebaki nyuma kimaendeleo. Lugha hii ya mkemeo ni dhihirisho tosha kuwa waandishi wa Riwaya Mpya wanasuta, tia shaka na kukosoa nia ya utandawazi haswa katika nchi zinazoendelea.

Lugha ya mkemeo imetumika kuonyesha jinsi utandawazi hufanya jamii au binadamu kupoteza utambulisho wake. Kuvunjwa kwa utambulisho kumefanya watu wasijielewe na kutoelewa mazingira yao. Khamis (2007) anaelezea jinsi lugha katika riwaya hii imetumika kuonyesha mvunjiko wa utambulisho. Mtu binafsi amevunjikavunjika kwa sababu hana pahala pa kusimama katika kudai haki zake za msingi. Kwa mfano; kuweza kupata kazi ya kumwendesha maisha yake kwa sababu ya utandawazi kuvuka mipaka. Aidha, kuvunja sheria za taifa kuchukua vyombo vya thamani na kuvitia katika mitaji na utajiri au maslahi ya mataifa yenye nguvu. Viwanda vimenunuliwa, benki zimechukuliwa, machimbo ya madini na rasilmali nyingine zimehodhiwa, vyombo vya huduma vya wananchi kama mashirika ya usambazaji umeme vimebinafsishwa, huduma za maji na mafuta na sehemu ya shule na hospitali hazimo tena

mikononi mwa serikali za wananchi. Maswali mengi ya kifalsafa katika Riwaya Mpya kama vile: mimi nani? Nimetoka wapi? Ninaelekea wapi? Na nini maana ya maisha? Yanalenga kuonyesha mtazamo wa waandishi kuwa utandawazi umechanganya watu mpaka wakakosa kujielewa.

Isitoshe, lugha ya mkemeo imetumiwa na waandishi hawa kuonyesha tabia ya utandawazi kwa nchi zinazoendelea. Waandishi hawa wameunda maneno kueleza jinsi utandawazi unavyowasapa watu uhai. Maneno haya yanatokana na hali ngumu ya maisha ya kiuchumi katika nchi zinazoendelea. Pia, maneno haya yanatoa taswira ya ubabedume, uhimla na hata uwezo walionao nchi zilizoendelea dhidi ya nchi zinazoendelea. Kwa mfano, maneno kama vile 'UMERO-JAPA', 'Binberu', 'Pembetano', 'New World Order', 'FUJO ASILIA', yanaonyesha uwezo, nguvu na ulwa wa nchi hizo. Mtazamo huu huonyesha kuwa utandawazi unaoendelezwa na mataifa yenye uwezo, unanyonya na kutia utumwani nchi zinazoendelea.

Lugha ya mkemeo ilidhihirika katika taswira mbalimbali. Taswira hutokana na jinsi wanavyotumia maneno kueleza matukio mahususi. Picha inayojengwa hapa inaonyesha mitazamo yao. Kwa mfano, katika kueleza jinsi wananchi na viongozi wa nchi zinazoendelea hutegemea misaada kutoka kwa nchi zilizoendelea. Aidha, katika kueleza jinsi nchi hizi zilizoendelea hunyanyasa nchi zinazoendelea. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Yao,* Afrika hurejelewa kama *dunia ya ujalaana, balaa na ushetani.* Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka,* misaada inayopokelewa na viongozi na wananchi katika nchi zinazoendelea huonyesha waziwazi mtazamo wa waandishi hawa kuhusu suala la utandawazi. Kwa mfano, makundi yaliyokusanyika kwenye bonde kubwa lililonyooka na kubeba mikono juu na vibuyu vilivyowazi wakitazama paka wa Kijapani anayeitwa *manekineko,* tai la Kimarekani na *Gwaru* kubwa ajabu la Euro kwa lengo la kuwaabudu na kuomba misaada. Mtazamo huu hudhihirisha kuwa utandawazi huzidisha utegemeaji. Nchi zinazoendelea zinazidi kuwa maskini na hivyo kuzidi kutegemea nchi zilizoendelea. Maswali yanayoibuka ni kuwa; kama utandawazi una nia njema kwa nchi hizi zinazoendelea, kwa nini nchi hizi bado zinategemea misaada kutoka nje?

Mkemeo wa ubinafsi unaosababishwa na utandawazi hujidhihirisha katika Riwaya Mpya. Mtazamo huu hudhihirisha jinsi teknolojia na sayansi zilivyoweza kuzaa ubinafsi. Ubinafsi huu kamwe ni zao la utandawazi. Katika riwaya ya *Dunia Yao,* tete za ubinafsi huonyeshwa jinsi hukua na kuimarishwa na nguvu kubwa, nguvu ya sayansi na teknolojia ambazo nazo zimekuza utashi wa pesa. Hii hurejelewa kama 'narcissism': kufa kwa wengine ndiyo nusura ya wengine.

Wanyonge wapo na hawaishi mbele ya watu wenye nguvu. Mbele ya ubinafsi, sayansi, teknolojia na utashi wa pesa wanyonge ni ombwe tupu, (Mohamed 2006: 47-48).

> Kakwea juu, matunda anakula yeye tu na wenzake wachache, wezi wote! Wanaiba hata na mbegu angaa tungependa na kuongeza idadi ya miti kuhakikisha wengi watafikiwa na matunda. (Mohamed 2006: 91).

Mwandishi anaonyesha picha jinsi utandawazi umefanya kila mtu kujitafutia vyake tu. Kila mtu huvaa kivyake, kujirembesha kivyake, hutafuta raha zake na hata kujifanya kinyago kivyake. Yaani kila mtu na vituko vyake. Mtazamo huu kwa hivyo hudhihirisha kuwa; chanzo cha ubinafsi ni utandawazi na athari ya ubinafsi ni kukosa udugu baina ya wanajamii.

4.4.2 Matumizi ya Mazungumzo

Mazungumzo yametumika katika Riwaya Mpya kuleta dhana halisi ya utandawazi. Kwa mujibu wa Wamitila (2003) mazungumzo ni maongezi yanayopatikana kati ya wahusika wa kifasihi. Mazungumzo haya yanahusisha mambo ambayo ni muhimu tu katika uendelezaji wa msuko. Wahusika huongea baina yao na hivyo kuipa hadithi uhai na huipa hadithi kasi ya kumsisimua msomaji. Licha ya kuvunja usimulizi wa hadithi, mazungumzo humwezesha msomaji kupumzika kutokana na usimulizi mrefu. Kando na mazungumzo, kuna matumizi ya mjadalanafsi au uzungumzinafsia ambapo mwandishi humpa mhusika usemi wa kibinafsi, pengine wa moja kwa moja au wa kimawazo, wa kindanindani. Kupitia mazungumzo na uzungumzinafsia ndipo mwandishi ana uwezo wa kuonyesha mawazo yake fiche. Hii humwezesha msomaji kutambua mtazamo wa mwandishi kuhusu maana kamili ya utandawazi. Kupitia kwa mazungumzo, msomaji anaweza kutambua kama mwandishi ana furaha, huzuni au amekasirika kuhusu suala lengwa. Mazungumzo huonyesha hisia za mwandishi na husaidia kuelewa msimamo wa mwandishi kuhusu suala fulani. Katika Riwaya Mpya, mazungumzo yametumika kujenga kinaya kuhusu sifa, historia au husiano wa utandawazi na nchi zinazoendelea. Mtazamo wao ni bayana kwamba teknolojia ambayo nchi hizi zinajivunia ndiyo chanzo cha uharibifu wa nchi. Kwa mfano,

> Siku hizi wanasema sio neno! Ni matatizo ya kawaida na yanampata kila mtu dunia nzima wanayoiita kijiji, ati *global village*! Hizi harakati wanazoziendeleza siku hizi katika hali yake ya sasa ni maangamizo. Hamna cha pamoja na wakazi wake, tuseme kitu kama *global pillage*...

> Siku kituo kilipofungwa naikumbuka. Ulianza kuimba wimbo wa Mefu. (Wamitila 2002: 87).

Mazungumzo katika Riwaya Mpya yanaonyesha bayana mtazamo wa waandishi kuhusu jinsi nchi zilizoendelea huchukua nafasi ya soko huru kwa kuvumbua na kuwauzia nchi zinazoendelea vitu vibovu visivyohitajika katika nchi zao. Sababu kuu ni viongozi kuendelea kutegemea misaada kutoka kwa wageni badala ya kujitegemea. Wageni kutoka mataifa ya Magharibi ndio hasa wendani wakubwa wa viongozi hawa. Wageni hawa ndio wanaothaminiwa sana na nchi zinazoendelea na ndio wanaoalikwa katika sherehe zote muhimu za kitaifa. Viongozi wa nchi hizi changa wanaamini kwamba watu wa mataifa ya ng'ambo ni watu wenye huruma na ambao huzionea imani nchi zinazoendelea na kupenda kusaidia daima. Mazoea ya kuwategemea wageni katika soko huru, yamewaingia viongozi wa Afrika kiasi kwamba wao huigiza na kununua vitu ovyo na duni muradi tu wataviagiza kutoka nje badala ya kuvitengeneza. Tabia hii kwa hakika imetokana na kasumba ya kutaka kuwaonyesha viongozi wengine kuwa Waafrika wanafuata mtindo wa kisasa (utandawazi). Hii imedhihirika katika aina ya bidhaa zinazopokelewa kutoka kwa nchi zilizoendelea. Pia, sheria na masharti yamewekewa katika vitega uchumi vya nchi hizi changa. Sheria na masharti huwafunga wenye nchi kutokuwa na uhuru wa kutumia rasilmali za nchi yao ipasavyo:

> Kuna nini hapa? Hiki ni kiwanda Cha? Reconditioned cars Mnazitumia? Ahh, deki masen! Haiwezekani asilan. Sheria zetu zinakataza matumizi ya maghari hayo! Basi mnayatengenezea nini. Kuna soko kubwa huko upande wa chini huko ndiko tunakotupa tusivyovihitaji! Mnavitupa, ehh? Mmm, ni hivi tuseme, wanakubali wenyewe, karibuni tutaanza kuwauzia samaki wabichi. (Wamitila 2002: 50).

Si ajabu kuwa kuuziwa bidhaa mbovu imekuwa jambo la kawaida, katika nchi zinazoendelea. Na kila kizazi kinaona hivyo ndivyo hasa. Hii imefifisha kipawa cha kufikiria na uvumbuzi. Aidha, udadisi haupo, umefilisishwa katika nchi zinazoendelea. Wananchi katika nchi hizi zinazoendelea wanaamini kuwa hawakuzaliwa na fikra ya udadasi kabisa. Kwa hivyo, hakuna kubahatisha au kujaribu kufanya kazi bali ni kutegemea tu misaada. Utandawazi ukawa usasa na ufenisi, huku wananchi na viongozi wa nchi zinazoendelea wamekosa msimamo thabiti katika ufenisi huu.

Kupitia kwa maneno ya wahusika katika vikundi, mitazamo ya waandishi kuhusu utandawazi hudhihirishwa. Maneno ya wahusika hao katika Riwaya Mpya yanaonyesha jinsi wananchi wa bara la Afrika ambao wameshuhudia kuja kwa enzi ya ukoloni, kupatikana kwa uhuru na enzi ya utawala wa viongozi Waafrika ambao wameshindwa kutimiza ahadi zilizowekwa wakati mkoloni alipofurushwa kutoka Afrika. Maneno hayo yanaonyesha jinsi viongozi wa bara hili wanavyopoteza wakati wakijisifu na kutangamana na Wazungu kwa ajili ya utandawizi ilhali raia wao wanazidi kuangamia kutokana na maafa ya kimaumbile na pia matatizo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mifano ya malalamiko imo katika riwaya ya *Bina-Adamu!*, ambapo wananchi wanalilia *Structural Adjustment Programmes* (SAPS) kuwasapa uhai kwa sababu ya 'kijiji cha wizi'. Mtazamo unaodhihirika hapa ni kuwa, utandawazi ndio chanzo cha utengano baina ya matajiri na maskini. Maskini wanalalamikia matajiri kuwanyonya nguvu. Wanatajirika kutokana na nguvu za maskini, jambo ambalo linasababishwa na utandawazi.

Utandawazi umezua wizi na ufisadi. Wizi na ufisadi kwa upande mwingine ni kielelezo cha uozo wa jamii katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Ufisadi ni mmojawapo wa magonjwa ya kijamii ambayo, kama saratani, yamekataa kuisha katika nchi zinazoendelea na yanaendelea kuzorotesha maendeleo yake. Kulingana na masimulizi mbalimbali katika riwaya hii mpya, ufisadi umeangamiza mataifa mengi ambamo rasilmali zilizotengewa miradi ya kufaidi jamii kama maji, umeme, kilimo, shule, hospitali, dawa na hata chakula, huishia mifukoni mwa viongozi wachache na kuacha umma ukiteseka na kuangamia kwa dhiki mbalimbali. Ajabu ni kwamba, kwa kutumia kigezo cha dunia kama kijiji, viongozi hawa wanashirikiana na wageni kuwakandamiza wananchi. Ni kutokana na majanga haya ya utandawazi ndipo, wahusika katika vikundi wanaamua kugoma kwa kuonyesha hasira zao. Migomo hii huonyesha kuwa utandawazi huendeleza ufisadi na wizi. Haya yanaendelezwa na viongozi kwa lengo la kujinufaisha wao wenyewe. Kwa mfano, Mohamed (2001: 154) anatambua jinsi wananchi wanaungana kukashifu ufisadi na wizi wa viongozi hawa.

4.4.3 Falsafa ya Ukinzani na Kinaya

Riwaya Mpya imetumia mbinu hii ya kinaya na ukinzani kwa wingi. Hutcheon (1989) na Wamitila (2003) wanathibitisha kuwa, kinaya ni matumizi ya lugha ambapo mwandishi hueleza jambo lililo kinyume cha matarajio ya hadhira yake au jambo ambalo tayari hadhira inalifahamu kuwa ni kinyume cha ukweli ulivyo. Ukinzani nao una maana ya maelezo kuhusu dhana mbili zenye maana zilizo kinyume kabisa. Matumizi ya aina zote mbili za usemi, huleta hali ya

kutatanisha lakini ambayo inaifanya hadhira kutafakari ili kuelewa maana na dhana ya utandawazi inavyohusika. Mitazamo ya waandishi kuhusu suala zima la utandawazi linadhihirika mhusika anapopinga jambo lakini wengine wanakubaliana. Aidha, mtu analipinga jambo lakini hatimaye analifanya. Kwingineko mtu anatarajia jambo lakini linamfika lililo kinyume na matarajio. Kwa mfano, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, mhusika K aliwachukia Wazungu, aliwaita mazimwi, aliwapiga vita. Lakini baadaye huona kuwa sura zao zinafanana na yake na tokea zamani. Hili linampa ujasiri wa kushiriakiana na 'mazimwi' katika kujinufaisha haswa kwenye soko huru. Mtazamo unodhihirishwa hapa ni kuwa, viongozi ndio chanzo cha matatizo yanayokumba nchi zinazoendelea. Wanaendeleza matatizo kama vile unyakuzi wa ardhi, unyanyasaji wa wananchi, kuiba mali za uma miongoni mwa mengine. Haya yanaendelezwa kwa ushirikiano au mahusiano na wageni au mabeberu waliokuja kuendeleza utamaduni wao.

Mtazamo wa waandishi kuhusu suala la utandawazi unadhihirika kwa jinsi viongozi walivyosawiriwa. Kwa hakika, viongozi wana ubinafsi, jambo ambalo linarejelewa kwa njia ya kinaya. Kiini cha ubinafsi huu kulingana na riwaya hii ni utandawazi. Dhana ya 'Mungu kwa wote' na 'kila mtu kivyake' inadhihirishwa kwa njia ya kinaya katika riwaya hii mpya. Viongozi wanapotafuta uongozi wanatoa ahadi ambazo hawatimizi. Wakati huo wanajifanya wazalendo. Riwaya ya *Bina-Adamu!* inafafanua jinsi suala la utandawazi limebinafsisha uongozi. Viongozi wote wanang'ang'ania kukwea paani. Kwa ahadi zao, wanafaulu lakini ni kinaya kuwa wanakaa huko juu paani, huko ndiko wanakochumia matunda kwa urahisi na kuwatupia watu walioko chini ambao ndio waliowashikia ngazi ya kupanda juu. Cha kushangaza ni kuwa walioshindwa kupata uongozi hawakubali bali, wanajiingiza katika uhuni mbalimbali.

> Lakini kuna wengine ambao wanachofanya ni kula wakashiba kwanza kisha kuyatupa makaka, makokwa na maganda huko chini yanakong'ang'aniwa na umati mkubwa ulioko huko. Wengine wanaiba na kuhamishia kwingine, labda ughaibuni. Imekuwa hivi kila wakati. Wote wanang'ang'ania kukwea paani. Walioshindwa wameamua kuichoma nyumba! Sasa hatuna pa kujishikiza... Tutalazimika kuanza mwanzo! Tutabakia kuchekwa milele kutokana na upofu na viongozi! (Wamitila 2002: 67, 73).

Katika riwaya ya *Musaleo!*, suala la elimu lililoletwa na utandawazi hukoselewa. Mhusika Profesa ambaye ni msomi aliyetegemewa na wananchi katika kukomboa nchi kupitia elimu yake

anasaidia kuendeleza uongozi mbaya badala ya kuupinga. Suala la elimu ambalo ni kiini cha utandawazi hupigwa chenga. Mtazamo huu hudhihirisha kuwa baadhi ya wasomi hutumia masomo yao kuendeleza uongozi mbaya ambao huathiri mwananchi wa kawaida. Kwa upande mwingine, kiongozi anatumia nguvu ya polisi kuwanyanyasa raia. Pia, kuitwa kwake OMNIZEE, mtukufu, mkombozi na kwa upande mwingine anabadilisha mwendo. Katika uongozi wake Mzee; Wizara ya Afya, nesi wanaenda sherehe za siku na kuacha hospitali bila wauguzi. Waziri anatumia ambalanzi kwa maslahi ya kibinafsi huku wagonjwa wakikosa huduma yake. Haya yote yanaashiria mtandao wa uongozi ulioletwa na wakoloni katika kuzikomboa nchi za bara la Afrika, ukawa 'utandachungu'.

Ilidhaniwa kwamba utandawazi ungeleta manufaa na nchi kutegemeana na kushirikiana kama kijiji kimoja. Badala yake dunia imejikuta ikigawanyika zaidi kati ya wale walio nacho na wasio nacho. Kinaya ni kwamba, jinsi nchi zinavyoendelea kuvumulia na kungoja kuimarika, ndivyo zinazidi kuumia na kuwa maskini zaidi. Kwa mfano, nchi hizi zinazoendelea hurejelewa katika riwaya ya *Musaleo!* kama *Shamba la Mawe*. Hii ni taashira kumaanisha mahali pa shida. *Majabali* hurejelea mateso na dhiki mbalimbali wanayoyapata watu wengi chini ya uongozi unaotawaliwa na utandawazi kupitia kwa Mzee. Safari ya Mugogo kwenda Shamba la Mawe ni ithibati tosha ya mhusika huyu kutafuta ukweli wa mambo kuhusu hali ngumu ya maisha. Safari hii ni taashira ya kuchimba historia ya nchi za Kiafrika. Riwaya Mpya ilidhihirisha kuwa, changamoto zinazokumba nchi zinazoendelea zinasababishwa na utandawazi na hivyo, suluhisho si utandawazi bali viongozi na wananchi kudadisi historia ya jamii yao kisha kupata suluhisho la kudumu.

> Nini? Hapana, hamna kitu kama hicho! Risasi sehemu hii? Mugogo una nini? Polisi kuua watu? Nchi hii? Labda huko ughaibuni. Hiki ni kisiwa cha amani. Unasikia bwana, kisiwa; tena cha amani katika bahari yenye machafuko ya kila aina! Labada hukulala jana! Lazima unaota wewe. (Wamitila 2004: 6).

Viongozi wa nchi zinazoendelea wana msimamo tofauti kuhusu athari ya utandawazi katika nchi zao. Wanaamini kuwa utandawazi ndio suluhisho la matatizo yanayowakumba. Kinaya ni kuwa, wanakataa kuamini kuwa nchi zao zina matatizo. Kwa mfano, hata kama kuna vita, utawala wao huchukulia kuwa nchi zao ni za amani ambapo hakuna vita baina ya watu wala milio ya bunduki.

Riwaya ya *Musaleo!* inarejelea kauli hii kwa njia ya kinaya kuonyesha kuwa bunduki hutumika tu ughaibuni, Wamitila 2004: 47.

4.4.4 Matukio na Hali za Kiajabu

Mitazamo ya waandishi kuhusu suala la utandawazi imedhihirishwa kupitia matukio mbalimbali na hali za kiajabuajabu. Walibora (2010) anarejelea hali za kiajabu kama sifa moja ya Usasaleo. Hali hizi hujumuisha kujirejelearejelea, uziada uliopinduka, mseto wa vitu, mwingiliano matini, kucheza na kuyumbisha uthabiti wa wahusika na usimulizi. Hii humwezesha msomaji kuweza kujifumbulia na kisha kujiamulia mwenyewe kuhusu uhasi au uchanya wa utandawazi. Hali hizi za kiajabu zinaogofya, kuduwaza na kushangaza japo zinasawiriwa kama matukio ya kawaida. Matukio na hali za kiajabuajabu huchanganua matatizo yanayokumba jamii kwa jicho la ndani. Waandishi wameoanisha sauti mbalimbali katika mchangamano mkubwa usioshikana na mantiki ya wakati na pahala kama hadhira zilivyozoea. Matukio haya yanamwaga na kufufuliza mawazo, falsafa na siasa ya mwandishi na kuyaacha yashikane na mtiririko wa hadithi bila ya kiungo bayana cha ploti.

Hali hii imedhihirisha nyenzo za kuasi kwa kurejelea hali halisi ya udhaifu, kuyumbayumba na ukosefu wa uthabiti na udumifu katika suala la utandawazi. Kwa mfano, riwaya ya *Bina-Adamu!*, kuna hali ya kuogopa kiini cha kijiji. Bina-Adamu anasema alipozaliwa aliwakuta watu wakikiogopa kiini cha kijiji chao na mpaka leo hii unapoisoma hadithi hii bado wanakiogopa, (uk.7). Sababu ya kukiogopa kiini cha kijiji ni kwamba mtu ambaye angethubutu kwenda kwenye kiini chake angepatwa na madhara makubwa. Kwa mfano, mwanaume anayekwenda huko anaweza kushtukia amebadilika jinsia na kuwa mwanamke kwa kuwa sharti alizunguke jabali lililoko kijijini, (uk. 9). Mtazamo wa waandishi ni kuwa jambo hili si la kawaida bali lilitumika kama mbinu ya utawala, ili wanajamii wachache wawatawale wanajamii wengine. Wanaotawala huunda visasili vinavyowawezesha kuendelea kushika hatamu ya uongozi, jambo ambalo limesababishwa na utandawazi.

Bina-Adamu anapoanza safari ya kukiuka visasili, anapewa mkoba na Babu wa Zakongwe uliokuwa na utu, mapenzi na kiini cha kuwa kwake. Pia, anaonywa autunze na asiudharau sababu ya sura yake kwani mwacha asili ni mtumwa. Jambo la uhalisia ajabu ni kwamba huwezi kutia utu au mapenzi kwenye mkoba. Kwa undani wake, *Bina-Adamu!* alikuwa anaonyeshwa kwamba mapenzi na asili yake vimo Afrika kwa hivyo, anapotoka Zakongwe (Afrika) asiyasahau mambo hayo kwani mwacha asili yake ni kama mtumwa sababu alikuwa anaelekea

Ulaya. Kwa hakika, mtazamo wa mwandishi huyu ni kuonya dhidi ya utandawazi. Anamwonya mhusika Bina-Adamu asije akaathiriwa na utamaduni mpya na kusahau asili yake. Mtazamo huu unamwonya mhusika kutokengeushwa na kiasi cha kusahau historia na utamaduni wake. (Wamitila 2002: 19).

Suala la kunyanyaswa na mataifa tajiri kupitia utandawazi pia linadhihirika katika matukio na hali za kiajabu. Mtazamo huu unadhihirika katika safari ya Bina-Adamu. Alikutana na majitu yasiyo na uwezo wa kawaida. Kwa mfano, alikutana na jitu refu ajabu lililokuwa na miguu myembamba ajabu na pia, miguu yake ilikuwa kubwa kama masahani, (uk.64). Jitu hilo lilifananishwa na ‘’hydra’’ na kudai lina vichwa vingi mno (wawakilishi wake katika nchi mbalimnbali). Linaendelea kujigamba kuwa lina uwezo wa kufa na kufufuka. Walipoongea, jitu hili lilimwambia ya kwamba ndilo linalomiliki maisha yake, (uk. 63). Linasema kwamba ndilo chanzo cha furaha katika kijiji cha Bina-Adamu (Afrika) vyakula vyote, ujuzi wote, elimu yote, raha zote na ndoto, (uk.64). Kwa jicho la ndani, mataifa yenye uwezo yamemiliki nchi zisizo na uwezo. Mataifa haya yameweza kuwakilishwa katika nchi hizi kupitia wawakilishi wao. Wawakilishi hawa ndio huendeleza sera za mataifa haya kupitia viongozi na mashirika waliyoyaanzisha. Mtazamo wa waandishi hawa ni kuwa; utandawazi umeingiza mfumo wa utawala unaonyima nchi zinazoendelea uwezo wa kujiamulia au kujiendeleza. Wananchi hawana nguvu wala uwezo wowote katika hali yote ya maisha. Sababu kuu ni majitu haya yenye vichwa vingi na wenye uwezo wa kufisha na kufufisha.

Matukio haya pia huangazia vyakula vya ajabu. Kitamaduni, ni hatia kula aina nyingine ya vyakula hasa katika jamii husika. Utandawazi umeweza kubomoa mipaka ya vyakula na kuendeleza matumizi yao haswa katika hoteli kubwakubwa. Hii imefanya viongozi kuvuka mipaka ya kudhibiti aina ya vyakula ambavyo vinahitajika katika nchi. Kiinchi au kitaifa, utandawazi umevunja nguvu na uwezo wa maamuzi ya nchi. Nchi na taifa lazima lifuate masharti ya vyombo vinavyotetea utandawazi. Mohamed (2001: 28) anaeleza jinsi mhusika K anakaidi utamaduni wake na kuanza kujihusisha na watamaduni wapya. Tukio la ajabu ni kula vyakula vya watamaduni-wapya kama vile chatu, nyoka wa kukaushwa, mende wekundu wa kizamoto miongoni mwa mengine. Mtazamo dhahiri ni kuwa, utandawazi umevunja mipaka ya tamaduni ya jamii. Watu hawana tena sheria zinazoongoza vyakula.

4.4.5 Matumizi ya Nyimbo

Mitazamo ya waandishi wa Riwaya Mpya kuhusu utandawazi hubainika katika nyimbo. Nyimbo ni njia muhimu ya kuwasilishia ujumbe katika kila jamii. Nyimbo ni muhimu hasa katika jamii ya Kiafrika ambamo elimu na taaluma ya uandishi bado inamilikiwa na watu wachache na ambamo masimulizi ni muhimu sana kama njia ya kuwasiliana na kuelimishana. Katika Riwaya Mpya ya Kiswahili, nyimbo zimetumika kuonyesha mtazamo wa waandishi kuhusu utandawazi. Nyimbo hizi ni muhimu katika kupasha ujumbe kwani zinaeleza nia ya mwandishi hasa katika kukemea athari za utandawazi. Kupitia nyimbo hizi, ni dhahiri kwamba wananchi wameshakata tamaa, wamechoka kutawaliwa na uongozi wa wabepari. Kwa mfano, wimbo wa Mefu katika riwaya ya *Bina-Adamu!* ni wimbo ulioimbwa katika ufunguzi wa kituo:

> Shusha, shushaa...thamani ya hela shushaaa! Bana, Banaa...ugavi wa hela banaa. Kata, kataa...matumizi ya hela kataa! Hurisha, hurishaa, soko la hela hurishaa! Punguza, punguzaa...Mishahara duni punguzaa! (Wamitila 2002: 87).

Mwandishi ametumia wimbo huu kuonyesha jinsi utandawazi umezaa matatizo makubwa kwa mwananchi wa kawaida. Matatizo haya yanajumuisha badadiliko katika thamani ya fedha, kupunguza mishahara na kuwekewa masharti ya matumizi ya pesa. Japo watunzi huona kuwa matatizo haya ni matatizo ya kawaida na yanampata kila mtu dunia nzima wanayoiita kijiji, ati *global village.* Mtazamo wao ni kuwa utandawazi ni kiini cha uharibifu wa sayansi yenyewe pamoja na wakazi wake, na kwamba ni *global pillage.* Matokeo ni thamani ya hela kushushwa, ugavi wa hela kubanwa, matumizi ya vituo vya serikali kukatwa au kufungwa, kubinafsisha kampuni za serikali na kisha kupunguza mishahara duni ya wafanyakazi.

Wimbo wa wazee katika riwaya ya *Musaleo!* ni thibitisho kuonyesha mtazamo wa mwandishi kuhusu utandawazi. Wimbo huu ulikuwa maono ya mama tabiri aliyetabiri uhusiano wa watu wa nchi hiyo na wageni. Uhusiano huo ulibadilisha mtindo wa biashara, kubadilishana bidhaa na kuleta matumizi ya sarafu. Huu ukawa mwanzo wa dhiki wa kijiji chao. Matumizi ya sarafu ukawa chanzo cha maafa na matatizo katika mji wa *Masa* (ulimwengu wa sasa). Wimbo huu ukawa wa kuwaonya watu kutoka katika utumwa wa utandawazi kwani malengo ya waanzilishi ni hatari; mioto mifukoni:

> *Jiungeni, jiungeni na msoa. Ombeni, ombeni na tendeni. Mwondoke katika huu utumwa. Yule mama mtabiri aliyasema:Tazameni, tazameni watu waja. Waja waja wenye vingi viroja. Wenye mioto katika yao mifuko. Wanaotembea katika kiini cha bahari. Wanaotoka kwenye tumbo la nyoka wa chuma. Hawa! Wataiharibu nchi hii na bara hili!* (Wamitila 2004:21).

Wimbo huu unaeleza mtazamo wa waandishi wa Riwaya Mpya kuwa, nia ya kuleta sarafu haikuwa nzuri. Huu ulikuwa mwanzo wa utawala wa nchi zenye nguvu na utengano wa watu. Matumizi ya sarafu ndiyo yalizua matatizo mengi yanayotokana na ubinafsi kama vile, wizi na ufisadi. Utabiri katika wimbo huu ulikuwa ni onyo kwa viongozi kutokubali matumizi ya sarafu. Lakini, athari ya kukubali sarafu kulingana na mtazamo wa Riwaya Mpya ni mgawanyiko au utengano wa watu.

4.4.6 Sifa za Wahusika

Mafunzo yote yapatikanayo katika fasihi yameendelezwa kupitia wahusika. Hivyo, katika Riwaya Mpya ya Kiswahili, mitazamo ya waandishi ilidhihirishwa kupitia sifa, tabia, majukumu na hata shughuli za wahusika. Waandishi huwapa majukumu mbalimbali wahusika wao ili kutimiza malengo ya kazi zao. Katika riwaya hii, wahusika waliobuniwa ni wahusika binadamu, binadamu-wadudu/wanyama na mizuka. Waandishi wametumia wahusika waliopewa nguvu za kichawi na miujiza. Hili ni zao la Kiafrika, mbinu za Kimataifa na mbinu ya usasa na kuingia usasabaadaye. Mbinu hii ya uhusika imevumbuliwa na kuumbuliwa upya ili kuonyesha dhana ya historia, dhana ya sasa na dhana ya usoni. Hivyo, wahusika wamebuniwa kuonyesha suala la utandawazi katika historia, utandawazi katika kipindi cha sasa na utandawazi katika kipindi cha usoni. Kwa mfano, wahusika katika riwaya ya *Bina-Adamu!* ni wa kiajabuajabu na wa kufikirika. Pia, uundaji wa majina yao haswa ya alfabeti pekee kama vile K, P.P, X, na M, hubainisha kuwa uhusika wao katika hadithi ni nyeti.

Waandishi wa Riwaya Mpya wamedhihirisha kuwa suala la utandawazi haliwezi likaeleweka na mhusika wa nyama na damu, lazima mtu afe kisha afufuke na awe roho au mzuka ndipo ataweza kuona athari ya utandawazi. Hii ina maana kuwa, mtu lazima awe na uwezo wa kusaili au achanganue jamii yake kwa jicho la ndani ndipo ataelewa jamii yake. Yaani, lazima utoke ndani ya jamii kisha uchunguze kwa umbali ndipo utaelewa yaliyo ndani. Mhusika Babu katika riwaya

ya *Babu Alipofufuka* alikufa kisha akafufuka na kuwa mzuka. Katika hali yake mpya, aliweza kudadisi jamii na kukosoa viongozi kama K waliokuwa wakitawaliwa na mataifa yenye nguvu. Katika uhai wao, viongozi hawa ni wanyanyasaji, wafisadi, wasaliti, wasio na huruma, watalaleshi, wabadhirifu wa mali za umma na wezi. Kwa upande mwingine, mhusika K pia anajitia kitanzi kisha baadaye kujitokeza kwa familia yake akiwa mzuka. Yuko tayari kuwashauri kuhusu maisha. Mtindo huu hudhirisha mtazamo wa waandishi kuwa utandawazi huleta balaa, lakini viongozi wanaotumiwa kuuendeleza hawahisi wala kutambua. Na kama wanatambua, basi wanapuuza.

Katika uwasilishaji, uchanganuzi na ufasiri wa deta, imebainika kuwa utandawazi ni suala ambalo waandishi wa Riwaya Mpya wameshughulikia kwa undani. Katika uwasilisho wao, utandawazi umesawiriwa kama kiini au kisababisho cha matatizo yanayokumba nchi zinazoendelea. Matatizo haya yamedhihirika kama umaskini, mwingiliano wa utamaduni mbalimbali, athari ya uvumbuzi mbalimbali ambayo huchafua mazingira, magonjwa na mengine mengi. Matatizo haya yameendelezwa zaidi kutokana na uongozi mbaya. Viongozi hushirikiana na mataifa yenye nguvu katika kunyakua rasilmali za nchi changa kama vile madini, bahari ambazo zimewekewa masharti kutumiwa na pia, nguvu kazi za nchi. Haya yametambulika kutokana na uhakiki wa maudhui ambayo yana uhusiano na utandawazi. Maudhui haya yanajumuisha Uongozi, sayansi na teknolojia, utamaduni, umaskini na mabadiliko.

Ilibainika kuwa waandishi wa Riwaya Mpya wametumia mbinu mbalimbali katika kuwasilisha mitazamo yao kuhusu suala la utandawazi. Mbinu hizi hujumuisha; uhalisia-ajabu, mwingiliano-matini, vurugu la kiwakati na uasi. Kupitia mbinu hizi masuala tofauti yameweza kurejelewa kama vile ufisadi, wizi wa mali ya umma, ubinafsi, utawala wa kiimla, uchoyo, ukatili na mengine mengi. Pia, mitazamo yao imeweza kudhihirika kupitia ufundi wa lugha ya mkemeo, mazungumzo, falsafa ya ukinzani na kinaya, matumizi ya hali za kiajabu, matumizi ya nyimbo na pia sifa na majukumu ya wahusika. Ni dhahiri kuwa, utandawazi umezaa ubinafsi miongoni mwa viongozi, umeleta uhalifu kwa sababu ya sarafu, utamaduni umezorota, pengo kati ya matajiri na maskini ni mkubwa na unazidi kupanuka kwa kasi.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti amejishughulisha na muhtasari wa matokeo ya utafiti kama yalivyoibuka kutokana na uchanganuzi wa Riwaya za: *Musaleo!*, *Dunia Yao*, *Bina-Adamu!* na *Babu Alipofufuka*. Pia, ameangazia manufaa ya utafiti huu na hali kadhalika, matatizo yaliyokumba utafiti huu. Kwa kutamatisha, amependekeza tafiti zingine zinazoweza kufanywa kuhusiana na utafiti huu.

5.2 Muhtasari wa Matokeo

Sehemu hii inatoa matokeo ya utafiti huu kwa muhtsari kwa kuegemea madhumuni matatu ya uchanganuzi. Madhumuni ya kwanza yalihusu uhakiki wa maudhui ya kitandawazi. Pili, ni kutathmini mbinu zilizotumika kuangaza utandawazi na tatu tathmini ya mitazamo ya waandishi kuhusu utandawazi.

Utafiti huu ulibaini kuwa uwakilishi wa utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili ni dhahiri katika maudhui mbalimbali yaliyoshugulikiwa na waandishi. Maudhui haya yana uhusiano mkubwa katika utandawazi. Aidha, yanaingiliana na kukamilishana katika kuelewa suala zima la utandawazi. Hujumuisha: uongozi, sayansi na teknolojia, utamaduni, umaskini pamoja na mabadiliko.

Kwa mfano, uhuru wa bendera ulizaa ukoloni mamboleo. Sera za uongozi na mitindo ya uongozi katika nchi changa zikaundwa na wakoloni kupitia kwa viongozi wao wenyewe. Mhusika K katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* ni kielelezo cha viongozi hao. Viongozi wakawaahidi maendeleo chungu nzima katika nchi zao, nao wakamiliki ardhi walizoacha wakoloni kwa ajili ya kujinufaisha wao wenyewe. Kupitia ahadi zao na sera zao, waliweza kuwatawala Waafrika tena. Wakarudi katika uongozi tena na kuunda mtandao baina yao na nchi zao. Utawala wao wenye uwezo ukateka nyara utawala hafifu wa mataifa changa. Wakawa ‘Wasamaria wema’. Riwaya Mpya inadhihirisha kuwa lengo lao lilikiwa kuwanyonya, kuwanyanyasa, kuwadharau na kunyakua tena rasilmali za nchi hizo kwa kutumia mtindo mpya au tamaduni mpya.

Athari ya wakoloni wapya wenye tamaduni mpya ikadhihirika wazi katika nchi zinazoendelea. Kwa mfano, ushirikiano wao na viongozi ukawapa nafasi ya kununua mashamba yenye rutuba na kufanyia ukulima huku mazao yakipelekwa kwao, wakauziwa rasilmali za nchi ambazo ni

vitega uchumi vya nchi kama vile machimbo ya madini, bahari kubadilishwa ya kimataifa na watu kuwekewa masharti ya kuvua samaki. Isitoshe, wakaendeleza biashara ghushi katika nchi hizi hasa kwa kuvumbua soko huru. Kwa mfano, kuchukua bidhaa kwa bei rahisi na kuuza katika nchi zao kwa bei ya juu, kuleta bidhaa ambazo hazitumiki kwa nchi zao na kuwauzia watu wa huku kwa bei ghali kwa jina la soko huru. Isitoshe, utangamano nao ukawafanya wenyeji watumwa wao, kuwafanyia kazi na kulipwa mishahara duni. Wenyeji wakaanza kuishi katika dunia duni kwa sababu ya utangamano wa watu uliorahisishwa na taasisi ya uongozi (utandawazi).

Uhakiki wa maudhui ya utandawazi ilibainisha kuwa kupitia mabadiliko haya katika Riwaya Mpya, waandishi wametumia namna mpya ya kuchunguza ukweli wa maisha, namna ambayo inatofautiana na mitazamo ya uhalisia wa kimaadili na kihalisia wa wanariwaya tangulizi. Namna mpya ya kisanaa ya riwaya hii haijajikita katika kunyenyekea, kuustajabu na kuucha ubinafsi katika jicho la kibepari. Lengo la riwaya hii mpya halikuwa kutalii ubinafsi na kuulekeza kwenye utumwa na utegemezi. Badala yake, maudhui ya riwaya hii imejikita katika kuumba kielelezo cha mtu wa kawaida ambaye anaeenda, anakula, anavaa na kujiheshimu kama mtu wa kawaida na pia, kumtalii mtu binafsi, kumwokoa kutokana na pingu za kinyonyaji na kumwanzishia maisha ya amani na neema. Kupitia kwa riwaya hii, jamii inachochewa kugutuka na kuelewa mazingira yao. Ukombozi huletwa na wanajamii wenyewe, lazima wasimame imara dhidi ya uongozi mbaya ili kuimarisha hali ya maisha yao. Riwaya hii huleta matumaini kwa wanajamii hasa inapotambulika kuwa wananchi ndio wenye nguvu na uwezo wa kubadilisha na kuimarisha hali yao.

Kwa mintarafu ya madhumuni ya pili, ilibainika kuwa waandishi wa Riwaya Mpya walitumia mbinu mbalimbali kusawiri suala zima la utandawazi. Aidha, ilibainika kuwa, mbinu hizi zilibeba ukweli fulani kwa njia ya kutisha, kustaajabisha, kuchekesha, kudhihaki au kwa njia ya kukera. Baadhi ya mbinu zilizotawala ni pamoja na uhalisia-ajabu, mwingiliano matini, vurugu la kiwakati pamoja na uasi.

Kwa mfano, mbinu ya uhalisia-ajabu ilitumika kukosoa masuala ambayo uhalisia wa kijamii hutegemea kuwepo. Ilibainika kwamba matukio yasiyoaminika ya kifantasia yalitumika katika Riwaya Mpya kukosoa au kusawiri suala la utandawazi. Mambo ya kiajabu yasiyo ya kawaida,

ndoto mbalimbali, wakati kutosonga ni miongoni tu mwa uhalisia-ajabu katika Riwaya Mpya. Mbinu hii imedhihirisha kiini cha utandawazi hasa katika nchi zinazoendelea. Kiini cha utandawazi kilibainika kuwa ni zao la mahusiano na wakoloni. Mbinu ya uhalisia-ajabu imetumika kukashifu mtindo na sera za uongozi barani Afrika, sera hizo zimejengeka katika utawala wa wakoloni wa kukandamiza na kunyanyasa watu. Isitoshe, uhalisia-ajabu umetumika kuonyesha jinsi mahusiano kati ya mataifa yaliyo na uwezo yanatumia nguvu zao, uwezo na itikadi zao kuwanyanyasa na kudunisha nchi zinazoendelea. Hii imezua ukosefu wa uthabiti katika michakato ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mbinu ya mwingiliano matini pia imebainisha uwakilishi wa utandawazi katika Riwaya Mpya. Ilibainika kuwa riwaya hii mpya ina mwingiliano matini katika uhusika, usimulizi na ujumbe. Suala ambalo ni dhahiri katika riwaya hii ni suala la kitovu cha kijiji. Suala hili limeleta migogoro baina ya wahusika mbalimbali. Migogoro hii huzua usaili na udadisi wa kisaikolojia katika akili ya wahusika mbalimbali. Mgogoro wazi ni mgogoro kuhusu maana ya maisha, hasa kulingana na kiini cha dunia kuwa kijiji. Katika kusawiri utandawazi, mwingiliano matini wa majina ya wahusika umebuniwa ili kuwakilisha tabia za viongozi na utawala ambao wanawakilisha. Ilibainika kuwa mbinu ya vurugu la kiwakati ilitumika kuangazia uwasilishi wa utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Mbinu hii ilitumika kuzua kinaya katika kueleza athari za utandawazi hasa katika nchi zinazoendelea. Katika matumizi yake, ilibainika kuwa nyakati hurudiana, hubadilika na hata kutengana. Kilichowazi ni kuwa mbinu hii ilibeza na kuzua ucheshi hasa katika matukio mbalimbali katika Riwaya Mpya. Mbinu hii ilidhihirisha kuwa hata baada ya uhuru wa bendera, matatizo yanayokumba Waafrika ni yale yale tu: njaa, magonjwa, vifo, makazi duni na kadhalika.

Uwakilishi wa utandawazi katika Riwaya Mpya ulidhihirika katika mbinu ya uasi. Waandishi wa Riwaya Mpya walitumia mbinu hii kuasi sheria za utunzi, hasa sheria zinazoongoza utunzi wa riwaya. Waliamua kutumia fantasia, visasili, viroja na vipengele vya bunilizi pendwa kama zile za sayansi. Usimulizi ambao hutumika katika fasihi simulizi ulikithiri katika Riwaya Mpya. Yaliyodhihirisha uwakilishi wa utandawazi yalihusu kuundwa maneno na mwandishi. Hii ni wazi hasa mwandishi anapotaka kueleza hali fulani, anajiundia au kutumia neno fulani kwa njia tofauti ili msomaji aweze kuona au kuhisi hali hiyo. Uasi ulidhihirika katika kuvunja kanuni za lugha na pia kutumia maneno mengi ya kigeni kuleta dhana ya utandawazi na

Kwa mintarafu ya madhumuni ya tatu, ilibainika kuwa waandishi wa Riwaya Mpya walitumia tamathali na njia mbalimbali kuonyesha mitazamo yao kuhusu suala la utandawazi. Haya ni pamoja na lugha ya mkemeo, matumizi ya mazungumzo, falsafa ya ukinzani, matukio na hali za kiajabu, matumizi ya nyimbo, urejeleo wa kazi nyingine na sifa za wahusika. Kwa mfano, katika lugha ya mkemeo, ilibainika kwamba waandishi walitumia maelezo mbalimbali kuzua taswira kuhusu ujumbe lengwa. Ufundi huu wa lugha ulibainisha kuwa madhara ya utandawazi ni mengi kuliko faida zake. Aidha, lugha hii imebainisha tabia ya utandawazi katika nchi zinazoendelea.

Mazungumzo kwa upande mwingine, uongozi mbaya, ufisadi, ukatili, biashara ghushi, hisia za wahusika kuhusu utandawazi, mtindo mpya na sera za uongozi uliweza kudhihirika. Mazungumzo ilionyesha mtazamo wa utengano baina wanajamii. Utengano huu ulisababishwa na uongozi uliotawaliwa na mataifa yenye nguvu.

5.3 Matatizo yaliyomkumba Mtafiti

Utafiti huu ulikabiliwa na matatizo. Miongoni mwa matatizo ni changamoto ya kufasiri tashtiti, visasili, fantasia na hata istilahi zingine katika Riwaya Mpya. Aidha, tafsiri ya baadhi ya mapitio ya maandishi ilikuwa changamoto kwa sababu yalikuwa katika lugha ya Kingereza. Maneno mengine yalikosa tafsiri ya Kiswahili ikabidi mtafiti kutoa maelezo marefu ili kueleweka.

5.4 Mapendekezo ya Ujumbe

Kutokana na utafiti huu, utandawazi katika Riwaya Mpya umewakilishwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Waandishi wa riwaya hii wameweza kutumia mbinu kama vile uhalisia-ajabu, uasi, mwingiliano matini, na vurugu la kiwakati kuwasilisha ujumbe. Matumizi ya lugha ya kiufundi na ya kibunifu yalijenga taswira na kuonyesha mwelekeo na msimamo wa waandishi kuhusu suala la utandawazi. Kwa hivyo, kutokana na uwakilishi huu wa utandawazi katika Riwaya Mpya kupitia vipengele na lugha ya kiubunifu, mtafiti anapendekeza masuala yafuatayo:

Kwa jumla, uwakilishi wa utandawazi katika Riwaya Mpya umesheheni vipengele vingi vinavyofanana na kuingiliana. Vipengele hivi ni vya kiujumi, kimtindo na kimaudhui. Uwakilishi huu umefanikishwa kwa kuzingatia kaida na kunga za Usasaleo ambao umejenga jumuiya pana na inayoendelea kupanuka katika fasihi ya Kiswahili. Aidha, kwa kutumia maudhui haya kukemea suala la utandwazi ni jambo zuri. Hata hivyo, waandishi wa Riwaya Mpya wanachanganya hadhira hasa wanapokemea athari za utandawazi katika nchi zao, ilhali wao wameathirika na utandawazi katika kazi zao. Utafiti huu hivyo unapendekezea waandishi chipukizi wa fasihi kwa jumla waweze kuenzi na kusifu mabadiliko yanayochipuka katika fasihi

ya Kiswahili. Vilevile, waimarishe uandishi wao kwa kusoma kazi nyingi, si tu za fasihi ya Kiswahili, bali pia fasihi ya lugha zingine na kisha kutumia mitindo mipya katika kazi za fasihi ya Kiswahili. Isitoshe, michango ya mitindo hiyo itambulike na ienziwe.

Lengo la vipengele hivi vya usasaleo vilivyotumika kuwakilisha utandawazi ni kuweza kutikiza ulimwengu wa ndoto na kuwasilisha ulimwengu mwingine wa makadirio. Utikisaji huu kwa hakika ni wa uchokozi na wa kubainisha dunia kwa uwazi zaidi. Uwazi huu huwezesha jamii kutambua jinsi utandawazi unavyoweza kumwingilia mtu hata asiweze kujitanzua kutokana nayo. Aidha, vipengele hivi vimeweza kuunda ulimwengu wa riwaya na msuko wake, na umbo lake na muundo wake ukawa si wa kawaida. Vipengele hivi vinabainisha kuwa utandawazi umezua utata na kuunda dunia ovyo, dunia iliyojaa kilio, dunia inayoendeleza mauti na hata kuonyesha utamu wa kifo na uchungu wa uhai. Utafiti huu hivyo, unapendekezea waandishi wa fasihi kwa jumla, kuweza kubobea katika mtindo huu ili hadhira izame katika kufikiria masuala kwa undani na kuelewa matukio mbalimbali katika jamii kwa jicho la ndani na kwa mtindo mpya.

Hali kadhalika, ari ya waandishi wa Riwaya Mpya kutumia vipengele vya Usasaleo ni kuonyesha jinsi waandishi walivyoimarika katika kujadili mambo nyeti kuhusu jamii yao na mataifa. Ujasiri huu unabainika katika uhuru wa kisanaa na fikra. Hili linamwezesha mwandishi kuelea katika uhuru wa kusema masuala ya kijamii kama vile ya kisiasa, kiuchumi, kiteknolojia, uongozi miongoni mwa mengine bila kushurutishwa kinyume na mbinu ya uhalisia. Utafiti huu unapendekeza kuwa ujasiri huu unafaa uhimizwe kupitia vitabu vya fasihi vya viwango vya chini ili waweze kutambua matatizo yanayokumba nchi yao kwa njia mpya. Washikadau waweze kuwahimiza ili mbegu ya ujasiri ipandwe katika umri mdogo.

Matumizi ya lugha kisanaa ni njia mojawapo ya kuonyesha hisia za ndani za mwandishi. Hii imebainika katika kutathmini mitazamo ya waandishi wa Riwaya Mpya kuhusu suala la utandawazi. Matumizi ya lugha ya mkemeo, ukinzani na kinaya na mazungumzo zilizotumika. Ilibainika kuwa msimamo wa mwandishi kuhusu suala fulani hubainika kutokana na matumizi ya lugha. Ujumbe unaowasilishwa hukolea kwa fikra ya hadhira kutokana na ufundi wa lugha. Hivyo, mtafiti anapendekeza kuwa matumizi ya lugha katika kazi za fasihi lazima yaimarike kwa kutumia tamathali mbalimbali katika kueleza suala fulani. Hivi, kazi hizi zitavutia watu wengi na kuendeleza fasihi ya Kiswahili kwa jumla.

5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Utafiti huu ulitathmini uwakilishi wa utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Uwakilishi wa utandawazi katika Riwaya Mpya ulidhihirika kupitia maudhui ambayo yalikuwa na uhusiano na utandawazi. Katika kueleza uwakilishi huu kupitia maudhui, waandishi waliweza kupitisha ujumbe wao kwa kutumia mbinu mbalimbali za Usasaleo. Hivyo, mitazamo yao kuhusu suala la utandawazi ulibainika kupitia matumizi yao ya lugha na tamathali tofauti tofauti. Hata hivyo, kuna masuala yaliyojitokeza katika utafiti huu ambayo yanahitaji utafiti zaidi. Kwa hivyo, mtafiti anapendekeza kufanywa kwa tafiti zaidi kuhusu:

i. Tathmini mtindo wa uundaji majina ya wahusika katika Riwaya Mpya Kiswahili. Ilibainika katika utafiti huu kuwa ubunaji wa majina ya wahusika katika Riwaya Mpya umebomolewa. Ubanaji huu ni ule wa kutumia herufi au ufupisho fulani. Katika riwaya tangulizi, majina halisi yalikuwa yanatumika kurejelea wahusika, kwa mfano, Maksudi, Musa, Waridi, Amani. Hata hivyo, mtindo mpya umezuka katika riwaya hii mpya, kwa mfano, majina ya wahusika nikama vile X, K, Ndi, P.P, M, Ye, miongoni mwa mengine. Utafiti huu unapendekeza utafiti zaidi kuhusu nia ya mabadiliko kwenye mtindo wa uundaji majina ya wahusika.

ii. Suala la kifo na ufufuzi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Kifo na ufufuzi katika Riwaya Mpya ni jambo la kawaida, masimulizi katika Riwaya Mpya hukinzana na imani ya baadhi ya jamii hasa kuhusu masuala ya kifo na ufufuzi. Baadhi ya wanajamii huamini kuwa ufufuzi wa wafu ni baada ya siku ya kiama na tena mahala pa ufufuzi hulingana na mienendo ya mtu hasa alipokuwa hai. Mawazo haya ni tofauti na yale ya Riwaya Mpya. Maswali kama vile: nini maana ya kifo? Nini hufanyika wakati mtu amekufa? Je, wafu wangali wanaishi? Je, dhana ya kufa na kufufuka ina falsafa gani katika Riwaya Mpya ya Kiswahili? Kwa nini wafu waliofufuka hutambua mambo mengi katika jamii kushinda wanaoishi? Je, wanapata ujasiri wapi wa kukosoa masuala mbalimbali katika jamii ilhali walipokuwa hai hawakuweza kuikosoa jamii? Hivyo, utafiti huu unapendekeza utafiti zaidi kuhusu dhima ya kifo na ufufuzi wa wafu katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya hii.

iii. Nafasi ya mhusika wa kike katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Majukumu ya kiumbe kike katika tanzu mbalimbali za fasihi yamekuwa duni. Kwa hakika kiumbe kike amedhalilishwa katika baadhi ya tanzu hizi. Nafasi ya kiumbe kike inaonekana kubadilika katika Riwaya Mpya. Kiumbe kike amepewa uwezo wa kiungu na hata kutawala wanaume. Wanauwezo wa kufanya miujiza na hata kuadhibu wanaume. Kwa mfano katika riwaya ya *Bina-Adamu!*, kuna wasichana-wavulana watatu wanaotambulika kama Huntha, wanaaminika kujua kiini cha kitovu cha dunia, aidha kuna mwanamke wa ajabu ambaye alimwongoza Msafiri katika safari yake. Mwanamke huyu aliyetambulika kama Hanna, alifanana na mke wake. Hivyo, utafiti huu unapendekeza utafiti zaidi kuhusu nafasi ya kiumbe kike katika Riwaya Mpya ya Kiswahili.

5.6 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, madhumuni yote matatu yalifikiwa. Maudhui mbalimbali yaliyohakikiwa; uongozi, sayansi na teknolojia, utamaduni, umaskini na mabadiliko, yalibainisha kuwa yana uhusuano kwa njia moja au nyingine na suala la utandawazi. Kila maudhui yalijengwa katika msingi wa utandawazi. Hivyo, uwakilishi wa utandawazi katika Riwaya Mpya unadhihirika katika maudhui ya riwaya hii. Ilibainika kuwa maudhui haya ya kitandawazi huonyesha madhara ya utandawazi katika nchi zinazoendelea. Madhara haya yalikuwa wazi katika hali ya maisha ya mwananchi wa kawaida na viongozi wao. Madhumuni ya pili yalitathmini mbinu zilizotumika kuangaza utandawazi. Matokeo yalionyesha kuwa mbinu kama vile uhalisia-ajabu, mwingilianomatini, uasi na vurugu la kiwakati ziliweza kuonyesha kiini cha utandawazi. Aidha, mbinu hizi zilitumika kusawiri uwakilishi wa utandawazi katika mataifa mbalimbali. Ilibainika kuwa mbinu hizi zilikashifu mtindo na sera za uongozi barani Afrika, sera hizo zilijengeka katika utawala wa wakoloni wa kukandamiza na kunyanyasa watu. Isitoshe, zilionyesha jinsi mahusiano kati ya mataifa yaliyo na uwezo yalitumia nguvu zao, uwezo na itikadi zao kuwanyanyasa na kudunisha nchi zinazoendelea. Hii ilizua ukosefu wa uthabiti katika michakato ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Madhumuni ya tatu ya kutathmini mitazamo ya waandishi kuhusu suala la utandawazi, ilifikiwa baada ya uchanganuzi wa tamathali za usemi zilizotumiwa na waandishi hawa. Kwa mfano, lugha ya mkemeo, falsafa ya kinaya na ukinzani, nyimbo, mazungumzo, matukio na visasili mbalimbali, urejeleo wa kazi nyingine, pamoja na sifa

za wahusika. Mtazamo mkuu ulikuwa ni kutia shaka, kukemea na kisha kukosoa suala la utandawazi.

MAREJELEO

Ameir, I. (1983). *Misingi ya Nadharia ya Uhakiki*. Dar es Salaam, TUKI.

Bernard, H. (2002). *Research Methods in Anthropology: Qualitative and quantitative methods*. 3rd edition. California: AltaMira Press ,Walnut Creek.

Barthelme, D. (1983). Literary Movement. Available from http://www.en.m.wikipedia.org retrieved on 7/3/2013.

Beerkens, E. (2006). Globalisation: Definitions and perspectives. Retrieved from http://www.edu.globalisation.co.uk on 15th May, 2013.

Bergonzi, B. (1972). *The Situation of The Novel*. London, Nenguin Publishers.

Butler, C. (2003). *Postmodernism*: *A very short introduction*. New York. Oxford University.

Chachage, S. L. (2008). *Utandawazi Ndani ya Ubongo*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Sosholojia.

Christian, G. (2010). Utandawazi Wasababisha Mabadiliko Makubwa Katika maisha ya Mwanadamu. Retrieved from http://www.dw.de on 21/03/2013 5:50.

Cooper, D. (1999). *Existentialism*. Oxford, Blackwell Publishers.

Cooper, C. (2003). *Globalisation and its Discontent: A concern About Growth and Globalisation.* London, Blackwell Publishing Ltd.

Crafts, N. (2000). Globalisation and Growth in 20th Centuary. Washingtone DC, IMF, Working Paper WP/00/44.

Cuddon, J. A. (1991). A *Dictionary of Literary Terms and Literary Theory*. London, Blackwell Publishers.

Derrida, J. (1976). *Grammatology and Writing Difference*. John Hopkins UP, Baltimore Trans. Gayatri Hakravotry Spivac.

Diegner L. (2005). Mahojiano Mafupi na Lutz Diegner Juu ya Riwaya ya Bina-Adamu! Swahili Forum 12: 95-97.

Foucault, M. (Ed.) (1984). *The Foucault Reader*. Paul Rabinow. New York, Pantheon.

Goldenberg, P. (1997). *Writing a Study Paper*. New York. Sadlier Oxford.

Gromov, M. D. (1998). Nagona and Mzingile Novels, Tale or Parable. Swahili ForumVAAP No. 55.

Husseini, S. A. (2010). Contested Meanings of Globalisation. Available at http://globalalternatives, wordpress.com2010/3/19. Retrieved on 29 /5/2013. 11:26.

Hutcheon, L. (1989). *The Politics of Postmodernism*. London & New York. Routledge.

International Labour Force and Information Group. (1998). *An Alternative View of Globalisation*. Cape Town, ILRIG.

Jauch, H. (ed.). (2001). *Playing the Globalisation Game: The Implications of Economic Liberalisation for Namibia.* Windhoek, Labour Resource and Study Institute.

Kanore, A. O. (2004). Effects of lobalisation At http://www.buzzle.com/author. Retrieved on 31/3/2013, 5:00.

King'ei, K. G. (2005). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi, Kenya Literature Bereau.

———— (2002). "Fantasy and Realism in the Modern Kiswahili Novel: A Critical look at *Babu Alipofufuka* by S. A. Mohamed."- Unpublished literary review.

_____(1987). "Usanifu wa lugha katika uandishi wa Ebrahim Hussein." Mulika 19, TUKI.

Kezilahabi, E. (1985). *African Philosophy and the Problem of Literary Interpretation*. Madison, University of Winsconsin.

———— (1974). *Kichwamaji*. Nairobi: East African Publishing House.

———— (1975). *Dunia Uwanja wa fujo*. Arusha: Eastern Africa Publication Limited.

———— (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

———— (1991). *Mzingile*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Khamis, S. A. M. (2005). "Vionjo Vya Riwaya Mpya ya Kiswahili." Research in AfricanLiteratures 36/1: 92-108. Bayreuth: Bayreuth University.

_____(2007). "Utandawazi au Utandawizi: Jinsi lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili Inavyodai." African Journalism Online Vol 70: SWAHILI FORUM 14: 165-180

Kulkarni, A. (2011). Positive Effects of Globalisation. At http://www.buzzle.com/author. retrieved on 4/10/2012, 10:30am.

Lyotard, J. F. (1979). The Postmodernism Condition. At http://www.marxist.org. Retrieved on 3/02/2013, 2:30pm.

Madumulla J. S (2009). *Riwaya ya Kiswahili. Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi.* Phoenix Publishers Nairobi Kenya.

Malamg, K.(2001). Globolisation and Its Impact. Retrieved at http://malamg01.hubpages.com.on 3/2/13.

Mbogo, E (1996). *Vipuli vya figo*. Nairobi. East African Educational Publishers.

Mkangi, K (1995). *Walenisi.* Nairobi. East African Educational Publishers.

Mkufya,W. E. (1999). *Ziraili na zirani*, Dar-es-salaam, Hekima Publishers.

Mohamed, S. A. (1981). ‘‘Kupatana na Riwaya zangu.’’ Mwamko 2. Jarida la Chama cha Kiswahili Chuo Kikuu cha Nairobi.

_____ (1995). *Amezidi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

_____ (2000). *Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Nairobi: Oxford University Press.

_____ (2002). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: J. K. Foundation.

_____(2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press

Murray, A. (2000). *Public Sector Restructuring in Namibia – Commercialisation, Privatisation and Outsourcing: Implication for Organised Labour*. Windhoek, Labour Resource and Study Institute .

Mugenda, M.O. na Mugenda, G.A. (1999). *Study Methods*. Nairobi, Acts Press.

Naik, A. (2011). Disadvantages of Globalisation. At http://www.buzzle.com/author. retrived on 12/12/12,4:30pm.

Njogu, K. (1987). “Maudhui ya Mapinduzi katika Riwaya za Visiwani Zanzibar.” Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Fasihi*. Rock Island, Augustana College.

Nyerere, J. (1962). *Hotuba kuhusu utamaduni.* Retrieved http://www.lukomwalange.blogspot.com on 13/3/2013, 1:30pm.

Offiong, D.A. (2001). *Globalisation: Post-Neodependency and Poverty in Africa*. Enugu Nigeria, Fourth Dimension Publishing Company.

Oxfam at http://www.freedomfromhunger.org. Retrived on 3/12/2013, 3:30am.

Pillai, P. (2011). Negative Effects of Globalisation. At http://www.buzzle.com/author. retrieved on 13/2/2013, 12:20pm.

Ruigrok, W. na R van Tulder. (1995). *The Logic of International Restructuring*. London/New York, Outledge.

Scholes R. and Kellogg R. (2006). *The Nature of Narrative: Revised and Expanded.* USA, Oxford U niversity Press.

The Daily Publications (2012). *Gross Domestic Product*. Canada.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford University Press.

TUKI (2006). *English –Swahili Dictionary*. University of Dar es Salam, Institute of Kiswahili Study.

Tylor, B. (2004). PostmodernismTheory. At http://www.buzzle.com/author. Retrieved on 12/2/2014.

UNICTAD (2012). Least Developing Countries. At http://unactad.org. Retrieved on 15/2/2013.

Walibora, K. (1996). *Siku Njema*. Nairobi: Longhorn Kenya.

_____ (2010). "Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha kati ya *Dunia Yao* na *The Tin Drum*." SWAHILI FORUM 17. Uk 143-157. Mainz: Johannes Gutenberg University.

Walmsley, C. (2006). Postmodernism: Simulations and the loss of the 'real'.pp.412-413.

Wamitila, K.W. (2002). *Bina-Adamu!*. Nairobi, Phoenix Publishers.

_____ (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na nadharia.* Nairobi, Focus Publishers.

_____(2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*.Nairobi, Focus Publishers.

_____(2003). Influence or Intertextuality?A Comparative Study of Kezilahabi's Nagona and Mzingile and Juan Rulfo's Pedro Paroma. Kiswahili 66:49-48.

_____ (2004). *Musaleo!*. Vide –Muwa Publishers.

Waugh, P. (2006) *An Oxford Guide: Literary Theory and Criticism.* London: University Press.

Wellek, R. and Warren, A. (1986). *Theory of Literature*. London: Oxford University press.

Williams, R, (1999). *Maxism and Literature*. New York: New York University Press.